*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## BUNGE LA KUMI NA MOJA

## MKUTANO WA TISA

## Kikao cha Pili – Tarehe 8 Novemba, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):**

Taarifa ya Mwaka ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa Mwaka 2015/2016 *(The Annual Report of the University of Dodoma for the Year 2015/2016).*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na swali Ofisi ya Waziri Mkuu la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika.

Na. 15

### Kuondoa Kodi Katika Mafuta ya Ngozi kwa Watu Wenye Ualbino

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Mafuta ya ngozi kwa watu wenye Ualbino huingizwa kama mafuta ya kawaida na kutozwa kodi na kufanya watu hao kushindwa kumudu kuyanunua:-

Je, Serikali iko tayari kuondoa kodi katika mafuta hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ulinzi na fadhili zake na rehema kwangu. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa nafasi hii ambayo ameniamini katika Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye Ualbino hutumia mafuta kinga *(sunscreen lotion)* ili kulainisha ngozi zao zisikauke na hutumika kwa maelekezo ya wataalam wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto zinazowakabili watu wenye Ualbino na imechukua hatua kadhaa ikiwemo kusambaza vifaa mbalimbali vinavyotumiwa na watu wenye Ualbino. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesambaza miwani ya jua 50, mafuta kinga boksi 100 na tayari Bohari Kuu ya Dawa Nchini *(MSD)* imejumuisha katika orodha ya madawa mafuta kinga kwa ajili ya kuzuia miale ya jua kwa watu wenye Ualbino na mafuta hayo hutolewa bila malipo katika hospitali za Serikali hapa nchini. Vilevile, Serikali inaandaa Mwongozo wa Msamaha wa Matibabu *(National Health Exemption)* kwa watu wenye ulemavu wakiwemo watu wenye Ualbino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napenda kuwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini, kuhakikisha kuwa wanaweka katika orodha mafuta haya wakati wanapoagiza dawa nyingine kutoka *MSD.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeondoa kodi kwa nyenzo za kujimudu kwa watu wenye Ualbino *(Technical Aids/ Appliances)* yakiwemo mafuta kinga kwa bidhaa zinazozalishwa nje na ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kadika.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imeondosha kodi ya vifaa hivyo lakini utafiti wa mitandaoni unaonesha watu wenye Ualbino katika nchi yetu hawapungui 17,000 na waliofanyiwa uhakiki ni 7,000 tu na vifaa vilivyopelekwa *MSD* ni boksi 100 na miwani 50. Je, Serikali haioni vifaa hivi bado havijatosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, baada ya kugawa vifaa hivi, je, Serikali inachukua hatua gani kwa wafanyabiashara wale wanaouza mafuta haya kwa bei ya juu ili kulikomesha kabisa tatizo hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mahitaji ya watu wenye ulemavu hapa nchini na imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba mahitaji haya yanapatiwa ufumbuzi. Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba kadiri ambavyo bajeti itakuwa inaongezeka basi mahitaji ya watu wenye ulemavu yataendelea kupatiwa mwarobaini wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ambalo amesema kwamba kuna watu ambao wanauza kwa bei ya juu hizi *lotion* za watu wenye ualbino; niseme kwamba Serikali itaendelea kufuatilia suala hili kwa maana si sahihi kwamba kama vitu vinaingizwa bila kodi halafu mtu auze kwa bei ya juu. Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili litafanyiwa kazi na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amina Mollel, jiandae Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. AMINA S. MOLELL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Tatizo la watu wenye *albinism* na hasa wa vijijini kutokana na uhaba wa mafuta haya wengi wamekuwa wakifa kwa ugonjwa wa saratani. Pamoja na majibu hayo, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuokoa maisha ya watu wenye *albinism* hasa wale wa vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi na kama ambavyo

nimewaagiza Wakurugenzi wote wahakikishe wanaweka haya mafuta kwenye orodha ya dawa wanazoagiza. Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati wa Serikali kwamba itaendelea kuagiza mafuta haya kadiri inavyotakikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii na nimpongeze Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba swali la msingi linahusu huduma za kuwapatia watu wenye *albinism* vifaa vyao lakini utakubaliana nami kwamba watu hawa wenye *albinism* wanaishi katika maisha hatarishi na Serikali kwa muda mrefu imekuwa ikifuatilia lakini bado watu wenye *albinism* wamekuwa wakiuawa hasa kwa sababu ya masuala mazima ya ushirikina. Je, Serikali ina utaratibu gani kuhakikisha masuala haya yanakwisha ili hata hivi vifaa vinavyoletwa basi viweze kuwahudumia hasa hawa watu wenye *albinism? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU)** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hizi imani za kishirikina, Serikali imepiga marufuku utolewaji wa vibali kwa waganga wanaopiga ramli chonganishi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lyimo hilo ndilo jibu langu la msingi na ndiyo jibu la Serikali kwamba tayari imeshapiga marufuku utoaji wa vibali kwa waganga wa jadi wanaopiga ramli chonganishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, umejibu vizuri sana, hongera sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dokta Christine Gabriel Ishengoma.

Na. 16

**Hospitali ya Wilaya ya Morogoro Haina Umeme na Maji**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Morogoro umekamilika lakini haina umeme wala maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme na maji katika hospitali hiyo ili ianze kutumika na kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Rufaa ya Morogoro?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya mifumo ya umeme na maji katika Hospitali mpya ya Wilaya ya Morogoro. Ifikapo tarehe 15 Novemba, 2017, Sh.25,240,969.33 zitakuwa zimelipwa kwa ajili ya kuingiza umeme hospitalini hapo. Hadi sasa *TANESCO* wameshaweka nguzo na mfumo wa umeme katika jengo la hospitali, kazi iliyobaki ni kufunga transfoma ili umeme uweze kuwashwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu ya maji hospitalini hapo utakaogharimu shilingi milioni 50 unaendelea. Kati ya hizo, shilingi milioni 21 zimeshapelekwa kulipia kazi zinazoendelea. Mifumo ya huduma ya maji itakuwa imekamilika ifikapo mwishoni mwa Januari, 2018.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pia nashukuru kwa majibu mazuri

ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa ni sera na mpango wa Serikali kila wilaya kuwa na hospitali, je, ni lini ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini utaanza licha ya jitihada nyingi za Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mvomero utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) :** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ni sera ya Serikali kujenga hospitali moja kila wilaya na napenda nimhakikishie Mheshimiwa Dokta Ishengoma na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Serikali itaendelea kuwezesha ujenzi wa hospitali moja kila wilaya kwa awamu. Katika Mkoa wa Morogoro tumeanza na Manispaa ya Morogoro na tutaendelea na wilaya nyingine kwa awamu zinazofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika mwenyewe, kubwa lao. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, katika sehemu ya pili ya swali lake Mheshimiwa Dokta Ishengoma kuhusu Hospitali ya Mvomero na bahati nzuri tulikuwa pale Mvomero tukabaini baadhi ya upungufu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshatenga fedha ya kumalizia jengo lile baada ya kuona upungufu ule na imani yangu ni kwamba kabla ya mwezi Januari hospitali ile itakuwa imekamilika ili wananchi wa Mvomero waweze kupata huduma vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Majimbo ya Longido na Ngorongoro ni majimbo ambayo yapo kwenye mazingira magumu sana na upatikanaji wa huduma za afya si wa uhakika. Wilaya ya Ngorongoro haina hospitali ya wilaya, Wilaya ya Longido imetengwa kwenye bajeti lakini utekelezaji bado. Je, ni lini Serikali itaweka mkazo kwenye majimbo haya ambayo kwa kweli yana mazingira magumu ya kijiografia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema mwenyewe kwamba Majimbo ya Longido na Ngorongoro yapo katika mazingira magumu na Wilaya ya Longido hakuna hospitali na Wilaya ya Ngorongoro tayari iko katika bajeti. Naomba ushirikiano wake mara fedha ambazo zipo kwenye bajeti zitakapopelekwa, ashiriki kikamilifu katika kusimamia ili matumizi ya fedha zile yawe mazuri kama ambavyo ilikusudiwa. Mwaka ujao wa fedha tushirikiane naye kuhakikisha kwamba Longido nao tunawawekea bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tabora Manispaa tuna tatizo kubwa la msongamano wa wagonjwa katika Hospitali Teule ya Kitete na kwa kuzingatia hilo, Tabora Halmashauri kwa kushirikiana na Madiwani pamoja na wananchi wengine tumetenga eneo kwa ajili ya kujengwa Hospitali ya Wilaya ambayo mpaka sasa hivi ujenzi wake unasuasua kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Je, Serikali inajipanga vipi katika kusaidia uwezeshaji wa kuweza kujenga hospitali hiyo ya wilaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Mwakasaka pamoja na Waheshimiwa Madiwani katika Manispaa ya Tabora kwa kutenga eneo la kujenga Hospitali mpya kwenye Manispaa ya Tabora ambayo itakuwa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huohuo, kwa kuzingatia kwamba Hospitali ya Kitete ni kweli imezidiwa na mzigo maana yake ndiyo hospitali pekee ya rufaa ya mkoa, Serikali inaahidi na namwomba ushirikiano wake, wakati tutakapokuwa tunaweka kwenye bajeti tushirikiane ili tuweze kupitisha kwa pamoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri, tunaendelea Waheshimiwa na Wizara hiyohiyo na swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

Na. 17

**Hitaji la Eneo la Kilimo Kijiji cha Sitalike**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kijiji cha Mtisi katika Kata ya Sitalike hakuna eneo la kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa wananchi hao maeneo kwa ajili ya kilimo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Mtisi kilichopo katika Kata Sitalike, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kina eneo la ardhi lenye jumla ya hekta 1,066.86. Kati ya hizo, hekta 1,043.86 ni sehemu ya Hifadhi ya Msitu wa Msaginya unaomilikiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS).* Maana yake ni kwamba, jumla ya kaya 589 zenye wakazi 3,416 wa kijiji hicho wamebakia na eneo la hekta 23 tu wanaloruhusiwa kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mahitaji ya ardhi ya kilimo katika kijiji hicho ni hekta 919.4, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, ifikapo mwishoni mwa Novemba, 2017, itakuwa imewapatia ardhi wakazi hao kutoka katika Kijiji cha Stalike (Makao Makuu ya Kata ya Sitalike) chenye ardhi ya ziada hekta 2,950.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wananchi wa Kijiji cha Mtisi wanapata shida sana, hawana kabisa eneo la kilimo. Nafikiri umeona kabisa hapa jinsi gani eneo la hifadhi ni kubwa zaidi kuliko eneo la kilimo na kaya zimeonekana hapa. Naishukuru Serikali imepanga kuwapa ardhi Novemba mwishoni lakini wananchi wa Mtisi wanahitaji kulima sasa, sasa hivi ndiyo kipindi cha maandalizi ya kilimo, wanatakiwa waandae mashamba yao. Je, Serikali haioni ni vema kubadilisha hii Novemba mwishoni wafanye Novemba hii mwanzoni ili wananchi wale waweze kupata maeneo ya kilimo waweze kupata chakula ndani ya familia zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ndani ya Kata hii ya Sitalike kwenye Vijiji vya Matandalani na Igongwe kutokana na ardhi ndogo wako ndani ya ramani toka 1972, lakini Serikali ilienda kuwabomolea nyumba zao na mpaka leo hii imekuwa tafrani, wala hawaelewi hatma ya maisha yao. Je, Serikali ina mpango gani na wananchi wa Matandalani na Igongwe? Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda kwenye Kata ya Sitalike kuona adha hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurejea majibu yangu ya swali la msingi katika kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Anna Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba ifikapo mwishoni lakini hadi sasa kazi za kuwapatia ardhi wananchi hao zinaendelea. Hadi jana kaya 200 zilikuwa zimeshatambuliwa na zilikuwa zimeshatengewa eneo maalum. Kwa hiyo, bado zoezi hilo linaendelea ile mwishoni mwa Novemba ni kumalizia kazi, kazi itakuwa imekamilika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili amesema kwamba wananchi wa Kijiji cha Matandalani na Igongwe walibomolewa nyumba ni kwa sababu walikuwa kwenye hifadhi. Natoa wito kwa wananchi ambao wako kwenye maeneo ya hifadhi kwamba wanatakiwa waondoke wenyewe badala ya kusubiri kuondolewa kwa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa shida hiyo iliyopo kule Matandalani na Igongwe na Halmashauri ya Nsimbo kwa ujumla, nilipita juzi lakini niko tayari kwenda tena kama matatizo yataendelea kuzidi kuwepo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso, jiandae Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mkoa wa Katavi ni kimbilio la wananchi wengi ambao wamekosa ardhi ya kilimo na wakati huohuo ardhi iliyopo Mkoa wa Katavi asilimia themanini imemilikiwa na misitu ya Serikali kiasi kwamba wananchi walio wengi wamekosa kupata nafasi ya kufanya shughuli zao za kiuchumi kupitia sekta ya kilimo hasa katika kata za Sibwesa, Kasekese, Katuma, Bulamata ambako kuna

migogoro mingi ya ardhi. Je, Serikali imejipanga vipi kutatua kero ya ukosefu wa ardhi ili wananchi waweze kuitumia ipasavyo kujikwamua kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, jiandae Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyozungumza katika Mkoa wa Katavi sehemu kubwa ya ardhi ni misitu na maeneo ya hifadhi. Ni lengo la Serikali kuendeleza maeneo hayo katika msingi wa kuendeleza misitu na hifadhi kwa ajili ya ustawi wa mazingira lakini vilevile kwa ajili ya kuendeleza ile hali nzuri ya hewa ikiwemo mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba katika halmashauri na vijiji vyote tuendelee kuhakikisha kwamba kila kijiji kinakuwa na mpango ardhi wa eneo lake ambao unaainisha maeneo ya kulima, maeneo ya kuishi kama kijiji, maeneo ya mifugo na malisho ili kusudi tuwe na mipango endelevu ya maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo jibu langu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Siha kwenye Kata Ngarenairobi na Ndumeti wananchi hawana maeneo ya kulima pamoja na makazi, wamekaa kwenye mabonde wakati wamezungukwa na heka zaidi ya elfu hamsini na sita za Serikali lakini kukiwepo na mashamba makubwa sana ya ushirika ndani ya Wilaya ya Siha ambayo hayatumiki kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwomba Waziri kama atakuwa tayari kufuatana na mimi baada ya Bunge hili tukatizame mazingira ya Wilaya ya Siha na huko Ndumeti pamoja Ngarenairobi na maeneo mengine tuweze kuamua

namna ya kupanga hiyo ardhi kubwa sana iliyoko Siha kwa matumizi ya wananchi kwa ajili ya kilimo, makazi lakini vilevile kutenga maeneo ya viwanda na uwekezaji mwingine kwa ajli ya Serikali na sera iliyopo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, ni ndiyo au hapana tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la Siha na maeneo kama hayo ni uwekezaji mkubwa ambao unafanywa na wananchi wachache. Kwa hiyo, tungependa tupate kwanza mpango wa Halmashauri yake halafu ndiyo tuweze kuufanyia kazi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, kwa niaba yake Mheshimiwa Marwa Ryoba.

Na.18

**Ujenzi wa Barabara ya Kasulu Kiwango cha Lami**

**MHE. MARWA R. CHAHA (K.n.y. MHE. SABREENA H. SUNGURA)** aliuliza:-

Akiwa katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2025 Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara ya lami (Kasulu *Road*) ili kufungua Mji wa Ujiji:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania aliahidi ujenzi wa kilomita10 za barabara kwa kiwango cha lami ndani ya Manispaa ya Kigoma Ujiji. Kutokana na ahadi hiyo, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji imeamua kujenga barabara ya Ujiji – Bulenga - Bangwe yenye urefu wa kilomita 7.5 ambapo usanifu umekamilika na itagharimu shilingi bilioni 11.6 ambapo ujenzi unaweza kuanza mwaka wa fedha 2018/2019 na barabara ya Ujiji hadi Daraja la Mngonya yenye urefu wa kilomita 2.5, hivyo kufanya jumla ya kilomita10 ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili uunganishe na ile barabara ya kutoka Kasulu lazima upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hiyo ufanyike kuunganisha kutoka Daraja la Mungonya hadi barabara Kigoma - Kasulu katika eneo la Msimba lenye urefu wa kilomita tatu. Kipande hicho cha kutoka Daraja la Mngonya hadi Msimba hakijafanyiwa upembuzi yakinifu. Kwa hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inashauriwa kuweka kipaumbele na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kutoka Daraja la Mto Mngonya hadi Msimba kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Marwa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri anasema ujenzi unaweza kuanza mwaka 2018/2019, unaweza kuanza. Sasa wananchi wa Mji wa Ujiji na Kasulu kwa ujumla wanataka kupata uhakika, yaani ile *commitment* ya uhakika kwamba utaanza 2018 au unaweza maana ukisema unaweza, unaweza usianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Mji wa Mugumu tulipewa kilomita mbili mwaka wa fedha uliopita lakini kilomita mbili hizi tumetangaza mara tatu hazijapata mkandarasi kwa sababu ya kilometa chache. Je, Wizara iko tayari kwa mwaka ujao wa fedha kutuongezea kilomita iwe rahisi kwa ajili ya wakandarasi kufanya *mobilization?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumesema kwamba ujenzi unaweza ukaanza kwa sababu bajeti haijapitishwa na Bunge. Naomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane naye kupitisha kwanza bajeti ndiyo ujenzi uweze kufanyika vinginevyo kama Bunge halitapitisha bajeti hiyo, ujenzi hauwezi kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili amesema kwamba wamepata ugumu kupata mkandarasi kwa sababu ya ufupi wa barabara ya kilomita. Ningemwomba Mheshimiwa Mbunge amshauri Mkurugenzi wake wa Halmashauri aweze kutembelea Halmashauri za jirani ambazo zimeweza kujenga hizo hizo kilomita mbili na zimepata wakandarasi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje, jiandae Mheshimiwa Sugu.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mwaka 2015 wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais alituahidi kilomita10 Mpwapwa Mjini na kwa kuwa bajeti iliyopita tumepewa kilomita moja tu, hata Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo analifahau hilo. Je, Mheshimiwa Waziri ataahidi wananchi wa Mji wa Mpwapwa kwamba hizo kilomita 10 zitakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, Mheshimiwa Waziri mhusika, Mheshimiwa Naibu Waziri kaa, bosi wako kasimama. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Naibu wangu kwa ufafanuzi mzuri wa maswali ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika swali la Mheshimiwa Lubeleje, ni kweli anachozungumza na mimi na yeye tulikuwa pamoja pale Mpwapwa Mjini kukagua barabara na ndiyo maana tumempelekea injinia mzuri sana kupitia *TARURA* na injinia yule wakati tunafanya ukaguzi wa Shule ya Sekondari ya Mpwapwa nilimpa maelekezo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Lubeleje ule ujenzi wa lami unaoendelea pale Mpwapwa Mjini tutaukamilisha na itakapofika 2020 Mheshimiwa Lubeleje awe na uhakika kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais itakuwa imekamilika na kuthibitisha kwamba Mbunge wao amefanya vyema kusimamia eneo hilo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hizi kilomita 10 Mheshimiwa Rais aliahidi maeneo mengi sana. Nashauri *data* zote za kilomita 10 ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi ili wamkumbushe kwa sababu kwa Jiji langu la Mbeya aliahidi pia kilomita ikiwemo barabara ya Mapelele, Kata ya Ilemi lakini mpaka leo hatuoni mchakato wowote na hatujapata nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Rais kwa sababu hajawahi kuja Mbeya toka amechaguliwa zaidi anarudi tu Kanda ya Ziwa. Mara ya mwisho ilikuwa aje Mbeya juzi kwenye *ALAT,* lakini waka-*cancel* siku mbili kabla ya siku ya *ALAT* kufanyika…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu uliza swali.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Rais aje Mbeya pia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la rafiki yangu Mheshimiwa Sugu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunazo takwimu zote za nchi nzima za ahadi za Mheshimiwa Rais za ujenzi wa miundombinu ya lami lakini na maeneo mengine. Mheshimiwa Sugu anafahamu pale katika Jiji la Mbeya kupitia Ofisi yetu tumepata *investment* kubwa ya kujenga barabara za lami katika Jiji la Mbeya. Siyo barabara za lami peke yake tumefanya uboreshaji, zile barabara zote tunazifunga taa na kujenga *damp* za kisasa kupitia mradi wa *Strategic City Project.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili ni *commitment* ya Serikali na tumefanya vizuri Jiji la Mbeya, Tanga na Arusha na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba ahadi zote ambazo Mheshimiwa Rais alizizungumza katika Halmashauri mbalimbali tutazitekeleza kupitia miradi yetu na kuhakikisha kwamba ikifika 2020 viporo hivi tutakuwa tumevimaliza hakuna shida ya aina yoyote.

**MWENYEKITI:** Barabara nzuri mpaka hoteli zinajengwa. Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kuna barabara ambazo upembuzi yakinifu ulishakamilika toka mwaka 2015/2016. Kwa mfano, barabara ya kutoka Nyororo - Igohole mpaka Mtwango upembuzi yakinifu ulishafanyika. Ni lini sasa Serikali itaanza utekelezaji wa kujenga barabara ile kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kigola anafahamu tulipokuwa Wilayani kwake tulizunguka maeneo mbalimbali na barabara anayoizungumzia ilikuwa ni barabara ya *TANROADS* na kulikuwa na barabara zingine za Halmashauri ambazo *TARURA* itashughulikia na zile barabara za Kimkoa ambazo *TANROADS* itashughulikia. Najua wazi kwamba mazoezi ya upembuzi yakinifu katika maeneo mbalimbali yanafanyika na kwa vile ile ilikuwa

katika ahadi na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, naomba nimhakikishie kwamba Serikali ni moja, tutahakikisha jukumu la Serikali tunalifanya ili barabara ile ya Nyororo iweze kujengwa kwa kadri iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, kwa niaba yake Mheshimiwa Serukamba.

Na. 19

**Kukauka kwa Vyanzo vya Maji Nchini**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA (K.n.y. MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** aliuliza:-

Athari za mazingira ni kubwa na vyanzo vingi vya mito *(water sources)* vimeathirika sana (mfano Mto Makere):-

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na mrefu wa kukabili hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, napenda nichukue fursa hii ya mwanzo kabisa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kwenye Baraza lake. Nishukuru pia Wabunge wenzangu ambao wamenipa ushirikiano na wewe mwenyewe Mwenyekiti ulikuwa mjumbe mwenzangu wa Tume kwenye Utumishi wa Bunge, nakushukuru sana kwa ushirikiano ulionipa. Niwashukuru wananchi wa Mwibara pia kwa kunifanya Mbunge wao na Rais akaniona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji, Serikali ilipitisha Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2006. Mkakati huu umeainisha hatua za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu za kukabiliana na uharibifu wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji. Aidha, mwaka 2008, Serikali iliandaa Mkakati wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Maziwa, Mabwawa na Mito ili kuhifadhi maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012, Serikali ilipitisha kwa ajili utekelezaji Mkakati wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, mwaka 2016, Serikali ilielekeza utekelezaji wa Programu ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na pia Serikali inakusudia kuzuia matumizi ya kuni kwenye taasisi za umma ili zianze kutumia nishati mbadala. Mikakati yote hii inalenga kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za muda mfupi zilizoainishwa na mkakati wa mwaka 2006 ni pamoja na kuwaondoa wafugaji waliovamia mabonde na maeneo ya vyanzo vya maji; kusimamisha shughuli zote za kilimo na kuwaondoa wavamizi kwenye maeneo yaliyoharibika sana; kuzitaka taasisi na watumiaji wengine wakubwa wa miti, kuni na mkaa kuwa na mshamba yao ya miti; kudhibiti shughuli za umwagiliaji usio endelevu na kuzitaka wilaya zote kubainisha vyanzo vya maji na kufanya tathmini ya hali ya mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zingine ni kudhibiti matukio ya uchomaji moto wa misitu; kupiga marufuku upandaji wa miti isiyofaa katika maeneo ya vyanzo vya maji; kuendeleza Kampeni ya Taifa na Kupanda na Kutunza Miti; Kuendeleza Program ya Kitaifa ya Elimu ya Mazingira kwa Umma; kuwa na programu za hifadhi ya mazingira na mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi kwa kila wilaya na kutekeleza na kupiga marufuku uchimbaji holela wa madini kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za muda wa kati ni pamoja na kujenga na kuendeleza malambo, visima na mabwawa katika maeneo ya wafugaji na wakulima; kuhuisha na kusambaza kwa mpango kabambe wa matumizi ya ardhi ili uanze kutumika mara moja na kuianisha na kuondoa miti isiyofaa kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za muda mrefu ni pamoja na kuendeleza teknolojia sahihi za kuvuna, kuhifadhi na kusambaza maji ya mvua na ya ardhini, kuharakisha matumizi ya njia mbadala za kuzalisha umeme ili kupunguza gharama za umeme kwa watumiaji na hatimaye kupunguza mahitaji ya kuni na mkaa. Aidha, Serikali imeanzisha Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti. Lengo la tuzo hii ni kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji. Tuzo hii hutolewa kila baada ya miaka miwili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majawabu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Mto Makere hali yake ni mbaya sana pamoja na Mto Malagarasi, lakini sababu kubwa kuna mifugo mingi sana imeingia huko na hakuna anayeitoa. Nataka kujua ni lini sasa Serikali tutakwenda kutoa mifugo iliyovamia kwenye vyanzo vya Mto Makere pamoja na Mto Malagarasi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla sijajibu swali la nyongeza, nitoe maelezo ya utangulizi. Wananchi wote nchi nzima kwa mujibu wa Sheria yetu ya Na.20 ya mwaka 2004 ya Usimamizi wa Uhifadhi wa Mazingira kila Mtanzania ana wajibu wa kutunza na kuhifadhi mazingira. Sheria yetu pia inatoa haki kwa kila Mtanzania aishi katika mazingira safi, salama na ya kiafya. Kwa hiyo, sheria inazuia watu wengine wasiwakere watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Makere ni kweli kabisa kwamba mto ule kwenye vyanzo vyake ulivamiwa lakini uvamizi ule ulikuwa unafanywa na wale wahamiaji haramu ambao wanakuja kule Kasulu, wanawakodi wananchi wa Kasulu halafu wengine wanaenda wanakata miti usiku wengine wanalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Halmashauri ya Mji wa Kasulu na Wilaya ya Kasulu tumeweza kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo yamevamiwa na kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi mifugo yote tumeiondoa na hata hivyo kuhusu miti; Nyarugusu, Makere yenyewe, Kwamba, Mwadivano na Kalimungoma, katika maeneo yote yale wamepanda miti zaidi ya 50,500,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Watanzania pamoja na vyombo vya habari wameanza kupotosha kauli ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa jana kule Kagera kwamba sasa wananchi ni ruksa kwenda kuvamia maeneo oevu, maeneo ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kauli ya Rais isije ikapotoshwa wananchi wakaenda kuvamia maeneo ya mito na kuanza kulima. Kauli aliyoitoa Mheshimiwa Rais Watanzania waelewe vyanzo vya maji ndivyo uhai wetu, mito yote itakauka, hakuna anayeruhusiwa kwenda kwenye chanzo cha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira, Rais ametumia kifungu cha 57 cha sheria hiyo kwamba pale ambapo kunakuwa na changamoto, wananchi wale ambao wako Karagwe wamekuwepo pale hawana ardhi, Rais ametuomba tushirikiane na uongozi wa mkoa kuhakikisha wale wananchi wanapatiwa maeneo mengine lakini siyo kuwaondoa.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Kwa hiyo, hamruhusiwi na msije mkasema kwamba Rais amewaruhusu wananchi kinyume na sheria. Ahsante.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** *Order*, *order, order*. Sasa Waheshimiwa majibu yanatolewa ninyi mnapiga makelele mtaelewa vipi?

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Subirini kwanza, kaeni kwanza, Mheshimiwa Obama na Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Uharibifu wa vyanzo vya maji katika Taifa letu la Tanzania ni mkubwa mno. Namshukuru Mheshimiwa Waziri amesema vizuri kwamba sheria tunazo lakini namna ya kusimamia hizo sheria ili vyanzo visiharibike ndiyo hafifu. Je, Wizara sasa inajipambanua vipi kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa kwa nguvu zote hapa nchini Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna wakati ambao Serikali ya Awamu ya Tano imejipambanua kulinda vyanzo vya maji kwa nguvu zote ni Serikali ya Mheshimiwa Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie wewe na Watanzania wote wanaotusikiliza, Mheshimiwa Makamu wa Rais aliunda *Task Force* ikaenda kwenye *Great Ruaha* ambako walikuwa wanaharibu vyanzo vya maji kuhakikisha kwamba wanafanya usimamizi, kutoa mafunzo na kuwaelekeza wananchi. Pia tumeenda Bonde la Usangu na Ihefu, tumeondoa wafugaji wote kwa maana ya kutumia nguvu kubwa kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vinaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Januari Makamba, ule Mto wa pale Katavi ambao ulikuwa umeziba kabisa, Mto Kachima, aliienda pale akakuta mkulima mmoja ameweka banio amezuia maji viboko wanataka kufa njaa na watumiaji wengine hawana maji, akazibua na sasa maji yanaendelea kutoka. Kwa hiyo, tutaendelea kutumia nguvu na sheria kuhakikisha kwamba hakuna atakayevunja sheria. Yeyote atakayevunja sheria hatasalimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenu ninyi nitoe darasa la MEMKWA kwa wale walioikosa yaani Mpango Maalum kwa Walioikosa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria niliyoisema Na.20 ya mwaka 2004, kifungu cha 57, Waziri anaweza akatoa kibali kwenye maeneo ya mita 60 kutokana na changamoto aliyoiona. Ndiyo maana wakati mwingine mnaona hoteli zinajengwa ndani ya mita 60 ni kutokana na vibali. Kwa hiyo, Rais wetu hajavunja sheria na ninyi mtakapowachochea wananchi kuvunja sheria, sheria ya Rais Magufuli itapambana na ninyi. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msigwa

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa niipongeze Wizara imekuwa mara nyingi ikihamasisha tutunze mazingira na sisi kama wawakilishi wa wananchi tumekuwa tukifanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi kama wawakilishi wa wananchi tumsikilize Rais au tumsikilize Waziri? Mara nyingi tumeambiwa Rais akisema ni sheria. Rais jana amewatangazia wananchi kwamba walime, waingie kwenye mabonde mpaka mvua itakapowatoa na hii sheria ya Rais anayoisema Mheshimiwa Waziri inahusu tu Kanda ya Ziwa na ni sheria namba ngapi kwa sababu anazungumza

kila siku kwenye Kanda ya Ziwa, analeta upendeleo wa wazi. Je, tumsikilize Rais au tumsikilize Waziri? Kwa nini kila wakati Rais akienda Kanda ya Ziwa...

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msigwa ambaye alikuwa *commissioner* mwenzangu sasa nime-*retire,* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haiongozwi kwa kupendelea wananchi wa eneo moja. Nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria na Katiba. Nimhakikishie na nirudie tena, alichokisema Rais wetu kule Kagera hajavunja sheria nimekwambia kifungu cha 57 kasome ambacho kinatoa mamlaka ya kuruhusu na hata wewe Mheshimiwa Msigwa kama una shughuli zako unataka kuzifanya kando kando ya ziwa au mto lete Ofisini kwetu utapata kibali.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Mheshimiwa Msigwa mimi nimeenda Kihansi nimekuta wananchi kule Kihansi pamoja Mufindi na Ifakara wanalima kwenye bonde la Mto Kihansi na tumewasaidia kabisa wananchi wale kwenye mradi wetu ili waendeleze lile bonde kwa kilimo. Hii inaonyesha dhahiri kwamba hatubagui, wananchi wote wako sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, wananchi ambao wamezoea kuchezea sheria, Serikali ya Awamu ya Tano haitamfumbia macho yeyote ama kwa kuchochea wananchi wavunje sheria ama yeye mwenyewe kuvunja sheria watapambana na mkono wa sheria na sheria hii inatoa adhabu kwa wanaochochea. Ahsante sana. *(Makofi/ Vigelegele)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Waziri mhusika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yamedhihirisha kwamba katika kipindi kifupi ambacho ameshika nafasi hii kwa kweli amejua mambo kwa haraka na kwa uzuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee mambo mawili, kwanza, Serikali kupitia Ofisi yetu iliziagiza lakini napenda nirudie kutoa agizo tena upya kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Halmashauri zetu kuorodhesha vyanzo vyote vya maji katika maeneo yao na kuvileta kwetu na kuelezea hatua ambazo zinachukuliwa katika kuvilinda, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kifungu cha 57 cha Sheria ya Mazingira, Na.20 ya mwaka 2004, kipengele cha (1) kinaweka zuio la kufanya shughuli mita 60 kwenye kingo za mito, fukwe na maziwa lakini kifungu kinachofuatia cha (2) kinasema, Waziri anaweza kuweka miongozo ya kuendesha shughuli za binadamu ndani ya maeneo yaliyoelezwa kwa mujibu wa kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya maelekezo mahsusi ya eneo mahsusi alilokuwepo Mheshimiwa Rais, kazi yetu sisi sasa ni kutengeneza mwongozo wa namna ya kufanya shughuli ile katika eneo lile lakini hapo hapo kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niliweke sawa kwa namna hiyo kwamba kutokana na maelekezo yaliyotolewa, sisi sasa sheria inatuelekeza kuweka mwongozo

wa pale mahali ambapo wale watu waliomba kufanya ile shughuli namna ya kufanya ile shughuli bila kuathiri mazingira. Kwa hiyo, hakuna *blanket permission* ya kuvamia vyanzo vya maji na kingo za mito kote nchini. Tutaendelea kufuata sheria kwa sababu sheria bado ipo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuweka kumbukumbu sawa kwenye jambo moja huku nikipongeza majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri pamoja na Waziri mwenye dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo hili lililosemwa kwamba Rais anapendelea Kanda ya Ziwa, nataka niweke kumbukumbu sawa kwamba Mheshimiwa Rais siyo kwamba anapendelea Kanda ya Ziwa, isipokuwa Rais amekuwa akisikiliza vilio vya wananchi pale anapokuwa katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya jambo ambalo nataka nitumie kumbukumbu, Mheshimiwa Rais alipokuwa Bagamoyo, wananchi walipolilia eneo la Magereza alilitoa hapo hapo huku sheria ikiwa inataka eneo lile litumike kwa ajili ya Magereza, lakini kwa kuwa kilio cha wananchi kilikuwa kikubwa na huko siyo Kanda ya Ziwa ni Pwani, hapo hapo wala hata hakusubiri maelekezo ya Wizara kukaa kama alivyosema Kanda ya Ziwa, pale aliamua hapo hapo akasema wananchi hawa wapewe eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo ambavyo nasemea ni kwamba anakuwa anatolea utatuzi changamoto za wananchi na hicho ndicho kilichomfanya achaguliwe na yuko kwa ajili hiyo. Siku atakapokuwa Ruvuma atatoa majibu hayo hayo kwenye kilio cha wananchi, siku akiwa Arusha atatoa majibu hivyo hivyo na maeneo mengine mengi ameshafanya shughuli za aina hiyo, hivyo tusije tukapotosha utekelezaji wa kazi za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, swali hili limetuchukulia muda mwingi sana, sasa tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na swali la Mheshimiwa Mary Muro.

Na. 20

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Mradi wa Umeme Kiluvya-Chalinze**

**MHE. MARY D. MURO** aliuliza:-

Tangu mwaka 2014 *TANESCO* iliweka alama ya X kwenye maeneo ya Kiluvya, Kibaha hadi Chalinze kupisha ujenzi wa kupitisha umeme wa Gridi ya Taifa lakini hadi sasa hakuna fidia iliyolipwa kwa wananchi hao na pia wanashindwa kufanya uendelezaji wa maeneo hayo.

Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia stahiki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Kinyerezi Dar es Salaam kupitia Chalinze, Segera hadi Arusha yenye urefu wa kilometa 600. Pia mradi huo utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wenye msongo wa kilovoti 220 kutoka Kibaha hadi Bagamoyo yenye urefu wa kilometa 40 na kutoka Segera hadi Tanga yenye urefu wa kilometa 60. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa vituo vya kupoozea umeme vya Chalinze, Segera, Kange na Zinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya mradi huu ni kuongeza upatikanaji wa umeme katika Ukanda wa Mashariki na Kaskazini mwa nchi kutoka kwenye mitambo ya kuzalisha

umeme ya Kinyerezi. Gharama za mradi huo ni dola za Marekani milioni 693 ambazo zitagharamiwa kwa mkopo kutoka benki ya *Exim-China* kwa asilimia 85 na Serikali ya Tanzania asilimia 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kutathmini mali za wananchi watakaopisha mradi huo kutoka Kibaha hadi Chalinze imekamilika na kuidhinishwa na Mtathmini Mkuu wa Serikali. Jumla ya shilingi bilioni 21.6 zitahitajika kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wapatao 855 wa Halmashauri za Kisarawe, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini, Bagamoyo ikiwemo eneo la Kiluvya. Fidia hiyo italipwa na Serikali na fedha hizo zimetengwa katika bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/2018. Taratibu zote za uandaaji taarifa na majedwali ya malipo ya fidia zimekamilika na malipo yamepangwa kulipwa katika mwaka huu wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muro.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Pwani, tangu alama ya X zilivyowekwa Serikali haijarudi kutoa mrejesho kwamba kitu gani kinaendelea na wananchi wale kujua tathmini hiyo watalipwa kiasi gani. Je, ni lini watarejesha mrejesho kwa wananchi ili waweze kujua malipo yao yatakuwa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali iliweka alama za X mwaka 2015 na sasa hivi tunaelekea 2018. Wananchi wanauliza watalipwa kwa tathmini ile au uthamini utafanywa mwingine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ameuliza ni lini Serikali itapeleka mrejesho, naomba nimtaarifu muda si mrefu Serikali itapeleka mrejesho wa namna ambavyo malipo haya ya bilioni 21.6

kwa wakazi wa maeneo haya inakojengwa msongo huu wa kilovoti 400. Kwa kuwa mimi na yeye ni Wabunge tunaotoka Mkoa wa Pwani na niwataarifu pia Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Koka na Mheshimiwa Ridhiwani maana nao wamekuwa wakifuatilia, kwa hiyo muda si mrefu tutawapelekea mrejesho na taarifa wataipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwamba kwa kuwa tathmini ilifanyika mwaka 2015 na tunaelekea mwaka 2018, naomba tu nimtaarifu kwamba malipo ya fidia yatalipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja ya kulipa fidia watu wanaopisha mradi wa *TANESCO* inafanana na watu ambao walichomewa moto mashamba yao wakati wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam katika Kijiji cha Kilangala. Bahati *TPDC* kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Lindi waliunda Tume ya kwenda kuhakiki yale madai ya kuunguziwa moto mashamba yao mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tathmini imeshafanyika na kinachosubiriwa ni kulipwa tu lakini tuliahidiwa wananchi wale wangelipwa mwezi wa Julai. Naomba *commitment* ya Serikali, ni lini wananchi wa Kilangala watalipwa hizi fedha zao ambazo zilitokana na wao kuchomewa moto mashamba yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli tathmini ilifanyika na naomba nimtaarifu kwamba wananchi wa Kijiji cha Kilangali watalipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri. Wananchi wa Jimbo la Segerea, Kata ya Kinyerezi, Mtaa wa Kifulu nao pia walitoa maeneo yao kwa ajili ya kuipisha *TANESCO* na mpaka sasa hivi hawajalipwa tangu Machi, 2016. Nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri ni lini wananchi wa Kinyerezi watalipwa pesa hizo kwa ajili ya maeneo yao waliyotoa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tathmini ya maeneo ya Kinyerezi ambapo maeneo yao yametolewa kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa Kinyerezi imekamilika na kiasi cha Sh.10,475,603,000 zinahitajika. Kwa hiyo, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake kwamba fidia hii italipwa kwa bajeti zinazokuja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Kigola.

Na.21

**Mradi wa Maji Katika Kata ya Mtwango**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza kujenga Mradi wa Maji kwa Kata ya Mtwango katika Vijiji vya Sawala, Mtwango, Rufuna na Kibao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Sawala, Mtwango, Rufana na Kibao katika Kata ya Mtwango ni miongoni mwa vijiji 12 vilivyopendekezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kupatiwa huduma ya maji kupitia Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Utelekezaji wa mradi ulipangwa kufanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Ujenzi wa mradi huo ulianza tarehe 01 Juni, 2015 na ulitakiwa kukamilika tarehe 01 Juni, 2016 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.36. Awamu ya kwanza ilikuwa ni ujenzi wa miundombinu ya maji katika Kijii cha Sawala pekee ambapo hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Novemba 2016 mkandarasi alikuwa hajakamilisha kazi na hivyo Halmashauri kuamua kuvunja mkataba. Halmashauri ilitangaza upya zabuni kwa ajili ya ukamilishaji wa kazi zilizobaki. Mkandarasi mwingine amepatikana na utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2017 kwa muda wa miezi 12 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.81. Serikali katika mwaka wa 2017/2018 imetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.56 kwa ajili ya Halmashauri ya Mufindi ili kukamilisha mradi huo katika Vijiji vyote vya Sawala, Mtwango, Rufuna na Kibao na kuendelea na utekelezaji wa miradi mingine ya vijijini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa vile mradi huu ni wa siku nyingi unaenda miaka saba sasa na Serikali imetoa *commitment* kwamba mwezi Desemba, 2017 itaanza utekelezaji. Sasa kwa sababu ni wa muda mrefu mwezi Desemba isipoanza utekelezaji nini kifanyike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Waziri wa Maji tuliwasiliana naye kuhusiana na maji Kata za Igohole, Nyololo na Mninga na niliagizwa kwamba tupeleke andiko linaloonyesha gharama za utekelezaji wa maji katika vijiji hivi nilivyotaja na andiko lile nimeshapeleka na gharama zote, liko kwa Katibu Mkuu. Sasa lini utekelezaji wa maji katika Vijiji vya Igohole na Nyololo utafanyika kwa sababu hawana maji kabisa na hivi ninavyoongea hawana maji. Ni lini Serikali itatekeleza? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji na kwa kuwa maji ni uhai na pasipo maji hakuna uhai, labda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama ilivyoahidiwa kwamba mwezi Desemba mradi ule unatekelezwa na mimi kama Mheshimiwa Waziri nitasimamia na kusukuma kuhakikisha kwamba mradi ule unatekelezwa ili wananchi wa eneo lile waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili kuhusu andiko na umuhimu wa suala la maji labda nimwombe sana Mheshimiwa Mbunge kama anavyowapigania wananchi wake baada ya kikao cha Bunge tukutane na mimi nipate nafasi ya kupitia andiko lile tuangalie namna ya kuweza kuwasaidia wananchi wa Igohole na Nyololo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Naibu Waziri. Mheshimiwa Sonia Magogo.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa tatizo la wananchi wa Mufindi Kusini linafanana kabisa na tatizo linalowakumba wananchi wa Handeni Mkoani Tanga. Je, Serikali ina mpango gani kuondoa au kupunguza adha hii ya maji inayowakuta wananchi wa Handeni? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jiandae Mheshimiwa Mgumba, Waheshimiwa nawaona lakini muda wetu umekwenda sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwanza katika bajeti ya mwaka 2017/2018 kumetengwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa maji. Pia wananchi wa Handeni wapo katika mradi ule wa *HTM.* Sisi kama Wizara tutasimamia mradi huu wa maji ili uweze kutekelezwa wananchi waweze kupata maji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgumba, jiandae Mheshimiwa Mkamia.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Matatizo yaliyopo katika Jimbo la Mufindi Kusini yanafanana kabisa na matatizo yaliyoko katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki. Tuna mradi wa maji katika vijiji vitano una miaka zaidi ya tisa. Serikali imejitahidi kujenga miundominu yote ya kuhifadhi na kusambaza maji kwa kutegemea chanzo cha Mto Ruvu katika mradi wa *Chalinze III* lakini mpaka leo maji hayatoki. Nataka kujua ni lini Vijiji hivi vitano vya Maseyu, Kinonko, Kidugalo, Ngerengere, Sinyaulime pamoja na kambi mbili zetu za Jeshi za Kizuka na Sangasanga vitapata maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Mheshimiwa Mgumba kwa namna ya kipekee anavyowapigania wananchi wake. Kwa kuwa suala la maji ni maisha ya watu, labda nimwombe Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge na mimi nipate nafasi ya kuweza kufika Morogoro Kusini Mashariki ili tuweze kuzungumza na wananchi na kuangalia namna gani tunaweza kuchukua hatua za haraka ili kuweza kuwasaidia wananchi wale kuondokana na adha ya maji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Mawaziri wapya hawa wanajibu vizuri, kwa kifupi na kwa ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Mradi wa Ntomoko ambao ulipangwa kuhudumia Wilaya za Kondoa na Chemba unaonekana dhahiri ni kama umechezewa. Je, Serikali iko tayari sasa kupokea ushauri wangu kwanza kusimamisha malipo ya mkandarasi aliyekuwepo na ifanye ukaguzi wa kutosha kwa sababu mradi huu ni kama hauna manufaa yoyote kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, jiandae Mheshimiwa Heche. Waziri mhusika karibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwamba tayari nimesimamisha malipo, hakuna malipo mengine yatakayolipwa katika mradi wa Ntomoko na mkandarasi alikuwa anadai shilingi milioni 700, nimesimamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili tumefanya kikao cha pamoja kati ya TAMISEMI, Wizara ya Maji na Mamlaka ya Maji ya Dodoma wanapitia usanifu kwa muda wa mwezi mmoja na nimekabidhi huo mradi baada ya hapo utatekelezwa na Mamlaka ya Maji ya Dodoma yaani *DUWASA.* Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kwamba ule mradi umechezewa, hatua nyingine zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria kwa wale wote ambao wamechezea huo mradi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Rais alipokuja kufanya kampeni yake katika Mji Mdogo wa Nyamongo ambao una wakazi karibia 45,000 aliahidi kuwapatia maji. Kwenye kitabu cha

bajeti ya mwaka jana ilioneshwa kwamba upo mradi kwa ajili ya kutoa maji Mto Mara na kupeleka kwenye Mji wa Nyamongo ambao vyanzo vyake vyote vya maji vimechafuliwa na mgodi na sumu ambazo zimeingia mgodini samaki wanakufa na watu hawana maji ya kutumia. Serikali imefikia wapi kuwapelekea watu wa Nyamongo maji kwa sababu ni ahadi ya Rais na ilikuwa kwenye mpango wa Serikali wa mwaka uliopita? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakamilisha usanifu wa mradi mkubwa utakaotoa maji Ziwa Victoria kupeleka mpaka Tarime kupitia kwenye eneo la Nyamongo. Kwa hiyo, tuko kwenye hatua nzuri, Mheshimiwa asubiri tu tunakamilisha na kutafuta fedha na tutatekeleza mradi huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Gregory Massay.

Na. 22

**Ahadi ya Kupeleka Mradi wa Maji Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Serikali kupitia Mradi wa Vijijini kumi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia iliahidi kupeleka maji Maretadu, Labay, Gidmadoy, Qamtananat, Garbabi, Magana Juu na Qatabela:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika Halmashauri zote nchini. Utekelezaji wa programu hii unafanyika kwa awamu. Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji kwa Halmashauri ya Mbulu Vijiji vya Singu, Masieda, Arri-Harsha, Dongobesh, Mongahay, Tumati, Haydom na Moringa vilihusika. Hadi sasa miradi ya maji katika Vijiji vya Singu na Masieda imekamilika na ujenzi unaendelea katika vijiji vilivyobaki. Serikali katika kuhakikisha inakamilisha miradi ya maji na kuanzisha mingine mipya kiasi cha shilingi bilioni 2.09 zimetengwa kwa Wilaya hiyo katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya pili ya utekelezaji wa *WSDP* iliyoanza Julai, 2016, Halmashauri zote nchini ikiwemo ya Mbulu zimewasilisha mipango ya utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha miaka mitano (5) kwa maana 2016/2017 - 2020/2021 ambapo miradi mingi ya maji itatekelezwa kulingana na mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu vilivyopo katika mpango huo ni Maretadi, Labay, Didmadoy, Quantananat, Garbabi, Magana Juu na Qutabela. Kwa kuanzia Vijiji vya Meretadu, Labay na Garbabi vimepewa kipaumbele katika mwaka wa fedha 2017/2018 ikiwa ni pamoja na Vijiji vya Genda, Ng'orat na Endahagichan. Vijiji vingine katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu vitaendelea kutekelezwa kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kutaja vizuri vijiji hivi, nina swali la nyongeza. Mwaka jana bajeti yetu ilikuwa shilingi bilioni 2.4 ikarudi na sasa hivi Mheshimiwa Waziri amesema tumetengewa shilingi bilioni

2.09, tatizo lililoko pale ni kwamba wakandarasi wanaojenga miradi hiyo baadhi yao hawako *site* ndiyo maana bajeti mwaka jana imerudi na kadri inavyoendelea hivi bajeti ya mwaka huu kuna wasiwasi wa kurudi. Je, atanisaidiaje kusukuma sasa bajeti hii iishe kwa kuwa wakandarasi wengi hawako *site*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mradi wa Haydom mpaka sasa una tatizo la kwisha pamoja miradi hii ambayo ameitaja mwenyewe ya Arri-Harsha, Barshai, Quantananat na mradi wa Mongahay kuja Tumati. Je, atakuja lini kule na kuwaahidi wananchi wangu ili aweze kuona jinsi ambavyo wakandarasi wanawadanganya kutomaliza miradi na pesa za maendeleo kurudi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ya pekee anavyowapigania wananchi wake wa Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kabisa nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji, si maji tu bali ni maji safi na yenye kutosheleza. Hata hivyo, imeonekana baadhi ya wakandarasi wamekuwa wakikwamisha jitihada za Serikali. Labda niziagize tu Halmashauri kwa wakandarasi ambao wanakwamisha miradi ya Halmashauri waondolewe mara moja kwa mujibu wa mikataba yao waliyoingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niwaombe sana Wakurugenzi wasiwape kazi wakandarasi kishemejishemeji au kiujombaujomba, wananchi wanapata tabu wakati Serikali inatoa fedha. Kikubwa naomba wale wakandarasi wanaokwamisha miradi waondolewe mara moja wapatikane wapya ili wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, kuhusu suala la mimi kufanya ziara katika Jimbo la Mbulu, nipo tayari baada ya Bunge tunaweza tukaongozana pamoja kwenda kuzungumza na wananchi wa Mbulu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nagu, jiandae Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pia naishukuru Serikali kuchimba visima vya Dumbeta, Waranga, Hirbadaw, Gidika na Dawar lakini ndiyo imebakia hivyohivyo wamechimba visima lakini havitumiki kwa sababu hawakuweka pampu na hatukusambaza maji. Naomba niiulize Wizara ya Maji watasaidiaje Wilaya yangu ya Hanang kuona kwamba hivi visima vilivyochimbwa vinawapatia maji wananchi kwa sababu wanayasubiri na lile ni eneo kame sana? Naomba jibu la swali hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumechimba visima na maji yamepatikana kinachofuatia sasa hivi ni suala la kitaalam, wanafanya *pamp test* kuhakikisha kwamba maji yaliyopo yana utoshelevu wa kutosha na ili waweze ku-*design* miundombinu itakayowezesha hasa kujenga matenki na mtandao wa mabomba ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maagizo yangu baada ya maji kupatikana Halmashauri sasa waanze kufanya kazi hiyo ili tuweze kutekeleza hiyo miradi na ndiyo utaratibu wetu, huwezi kutekeleza miradi bila kuanza kupata chanzo cha maji. Kwa hiyo, nimpongeze Mheshimiwa kwamba chanzo cha maji sasa amepata kinachofuatia ni kuweka miundombinu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Waziri wa Maji na Waziri wa TAMISEMI kwa kuteua Bodi ya Maji na pili kuwatuma wataalam kule Mbulu kwa ajili ya suala hili la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Mbulu na hasa Mji wa Mbulu, hali ya maji imekuwa mbaya kwa takribani sasa miezi sita. Katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 tulitenga fedha shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya utafiti na usanifu wa maji katika Mji wa Mbulu. Je, ni lini mpango huu sasa Wizara itatusaidia ili tuweze kupata maji ya uhakika kuepukana na adha hii ya ukosefu wa maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubaini upungufu katika Halmashauri yake nilimwelekeza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji *BAWASA,* ameenda kule kuangalia, akagundua matatizo mengine ni madogo sana, ni pampu tu zimekufa zinahitaji matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari ameshaandaa *quotation* na wiki hii nakutana naye ili tuweze kumpatia hela akafanye kwanza ufufuaji mdogo ili wananchi wapate maji, lakini baada ya hapo tutatekeleza mradi mkubwa kuhakikisha kwamba Halmashauri yake na kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi tunapata asilimia 95 ya huduma ya maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Na. 23

## Ahadi ya Kukarabati Malambo – Jimbo la Bunda

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kukarabati malambo ya Vijiji vya Makomariro 2, Kyandege, Mugeta, Mariwanda, Kihumbu, Kisangwa, Sanzete, Salama A, Salama Kati na Nyangaranga ambayo yamejaa magugu maji na mengine kina chake kimepungua?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilichimba malambo katika Vijiji vya Makomariro 2, Kyandege, Mugeta, Mariwanda, Kihumbu, Kisangwa, Sanzete, Salama A, Salama Kati na Nyangaranga kwa ajili ya kutatua matatizo ya ukosefu wa maji ya kunyweshea mifugo na kwa matumizi ya binadamu. Ni kweli malambo hayo kwa sasa yamejaa magugu maji na tope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imekuwa ikiwahamasisha wananchi wa vijiji husika kuyaweka malambo hayo katika mipango yao ya bajeti na kuiwasilisha Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ili yawekwe na kutengewa fedha kwenye mpango wa bajeti ya mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa malambo hayo, Halmashauri ya Bunda ilifanya tathmini ili kujua gharama halisi ya ukarabati unaohitajika kwa ajili ya kuweka kwenye bajeti ya mwaka 2018/2019. Ukarabati huo utagharimu jumla ya Sh.36,825,600 kwa mchanganuo ufuatao: Lambo la Kyandege litahitaji Sh.25,618,350, Mugeta Sh.97,870,400, Sanzete Sh.36,286,000, Salama A Sh.25,926,000,

Salama Kati Sh.46,315,850, Makomariro Sh.25,926,000, na Kihumbu Sh.108,883,000. Ukarabati wa malambo haya umepangwa kufanywa katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili malambo yaliyochimbwa au kukarabatiwa yaweze kuwa endelevu, Serikali inatoa ushauri kwa vijiji husika kuunda Kamati za Uendelezaji wa Malambo ambazo zitahusika na utungaji wa Sheria ndogondogo za utunzaji wa malambo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya kuridhisha, lakini naomba tunapouliza maswali haya tuwe tuna kumbukumbu ya majibu. Swali hili nimeshaliuliza zaidi ya mara ya tatu, katika bajeti ya mwaka 2017/2018 nimeuliza swali hili hapa Bungeni, Naibu Waziri wa Maji na sasa Waziri alijibu kwamba kwa mwaka wa bajeti 2016/2017 malambo haya yangefanyiwa ukarabati na bajeti ya Halmashauri ikaletwa hapa Bungeni sasa tena kipindi hiki wanasema bajeti itakuwa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimshukuru Naibu Waziri wa Maji ambaye sasa ni Waziri alikuja kwenye Jimbo langu akaangalia miradi akamuuliza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kwa hali iliyoko hapa Bunda unajua bajeti kiasi gani ya maji unayo. Mkurugenzi akasema haelewi, akatuambia ana bilioni 1.7 ya Halmashauri ya Bunda kwa ajili ya maji. Ni kwa nini hizi hela zisitumike kutengeneza haya malambo wakati yanahitaji shilingi milioni 350? Naomba Waziri atoe tamko la kutengeneza malambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tuna mradi mkubwa sana Mkoa wa Mara unatoka Mgango unakwenda Butiama lakini Vijiji vya Kata za Nyamswa, Kitare, Nyamamta na Salama viko jirani kilomita tatu kutoka kwenye mradi huu. Naomba Serikali ione namna gani inaweza kufanya vijiji hivyo viingie kwenye mradi mkubwa kutoka Ziwa Victoria. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Getere kwa jinsi ambavyo anahudumia jimbo lake na alishawahi kunichukua tukaenda mpaka jimboni kuangalia matatizo ya miradi hii ya maji. Alichokisema ni kweli bajeti ya mwaka 2016/2017 Halmashauri yake hawakutumia hata senti tano, fedha yote ikarudi wakati wana matatizo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Jafo, Waziri wa TAMISEMI aniruhusu niagize Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bunda na Mwenyekiti, siku ya Jumatano wiki ijayo waje tukutane pamoja na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kutatua matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, tumetangaza *tender* kwa ajili ya kuweka bomba kubwa jipya la mradi wa Mgango-Kyabakari. Kwa hiyo, wakati wanaweka bomba hilo Mheshimiwa Mbunge nitaomba tuwasiliane ili tuweze kuainisha na hivyo vijiji vitatu alivyovisema navyo vipate maji kutoka Mgango. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo na swali la Mheshimiwa John Mipata.

Na. 24

**Elimu ya Ufugaji Samaki**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Suala la ufugaji samaki lina faida nyingi kwa wananchi kama kujiongezea kipato na kupata kitoweo lakini wananchi wa Kata za Ninde, Kala, Wampembe na Kizumbi walioko kando ya Ziwa Tanganyika hawafugi samaki kwa kukosa elimu:-

Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam kutoa elimu ya ufugaji samaki?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa shughuli za ufugaji wa samaki zina faida nyingi kwa wananchi zikiwemo kujipatia ajira, lishe na kipato. Wilaya ya Nkasi ni moja ya Wilaya zenye mazingira na maeneo mazuri kwa ajili ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina wataalam wa uvuvi saba, wawili kati ya hao wana shahada ya ukuzaji wa viumbe kwenye maji na watano wana diploma zinazohusiana na masuala ya uvuvi na ufugaji wa samaki. Aidha, Kituo cha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (doria) cha Kipili kilichopo katika Wilaya ya Nkasi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kina wataalam watano. Pamoja na shughuli za usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Tanganyika, watumishi hao wana jukumu la kusimamia shughuli za ufugaji wa samaki ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya utoaji elimu ya ufugaji wa samaki katika ukanda wa mwambao mwa Ziwa Tanganyika, Serikali kupitia Wakala wa Elimu ya Mafunzo ya Uvuvi *(FETA)* ilianzisha kituo cha *FETA* Kibirizi – Kigoma ambapo mwaka 2015/2016 kilidahili wanafunzi 59 na wanafunzi 29 walihitimu masomo yao na katika mwaka 2016/2017 walidahili wanafunzi 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kituo cha Ukuzaji Viumbe kwenye Maji kilichopo Manispaa ya Kigoma kwa kushirikiana na Halmashauri zilizoko kwenye ukanda huo kimehamasisha ufugaji wa samaki na kuzalisha vifaranga vya samaki 31,404, ambapo katika mwaka 2016/2017, Wilaya ya

Nkasi jumla ya wananchi 70 walipata elimu ya ufugaji wa samaki katika Vijiji vitatu vya Ninde, Msamba, Namansi ambao wameanzisha kikundi kimoja katika Kitongoji cha Chele. Katika Kata ya Kala jumla ya watu 270 kutoka Vijiji sita vya Kala, Tundu, Kilambo, King'ombe na Mlambo wamepata elimu ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na viongozi wenzake katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi katika kuweka vipaumbele na uhamasishaji wa ufugaji wa samaki ili wataalam waliopo waendelee kuhamasisha ufugaji wa samaki katika maeneo yaliyoainishwa na watumishi kutoka Wizarani tutahakikisha kwamba tunakwenda Nkasi kushirikiana nao katika kutoa huduma za ugani katika masuala ya ufugaji wa samaki. Aidha, vijana washauriwe kujiunga na mafunzo ya ufugaji wa samaki katika Kituo cha Wakala wa Elimu Mafunzo ya Ufundi (*FETA)* kilichopo Kibirizi – Kigoma na hatimaye waweze kujiajiri katika shughuli za ufugaji wa samaki kwa lengo la kujipatia ajira, lishe na kipato.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mipata, jiandae Mheshimiwa Dkt. Sware na Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja na ombi moja kwa Serikali. Naanza na swali, maeneo mengi nchini hususan maeneo haya niliyoyataja ya Kata ya Kala, Ninde, Wampembe na Kizumbi yanayoendeleza shughuli za kilimo wananchi wake wanaishi maisha duni. Pamoja na mkakati uliosemwa na Serikali juu ya uendelezaji wa shughuli hiyo ya uvuvi wa kisasa na ufugaji wa samaki lakini bado maeneo haya niliyotaja umaskini haupungui kwa kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, kwa vile na yeye mwenyewe ni mtaalam katika eneo hilo la ufugaji wa samaki, yuko tayari kututembelea katika Kata hizi nne ambazo ni maarufu sana kwa uvuvi ili kuhimiza ufugaji wa samaki na kunusuru wananchi kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni ombi kwa Serikali. Takribani wananchi 1,000 wa Vijiji vya Kasu, Milundikwa, Kantala pamoja na Kisura wanakabiliwa na ukosefu mkubwa wa ardhi uliosababishwa na eneo lao kuchukuliwa na jeshi. Licha ya kwamba Serikali ilitoa eneo hili kwa wananchi kihalali lakini sasa hivi jeshi limetwaa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itume mtu au kiongozi mahsusi akauangalie mgogoro huu ili wananchi wapate mahali pa kulima kwa sababu sasa hivi wana sintofahamu kubwa sana na mvua sasa zimeanza kunyesha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi napenda nimpongeze Mheshimiwa Mipata lakini naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu mpenzi Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mkakati mkubwa kabisa wa Serikali hii ya Awamu ya Tano ambayo inatambua kwamba jamii ya wavuvi walio wengi katika nchi yetu ni jamii maskini ndiyo maana imeamua kuirejesha Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Huu umekuwa ndiyo mkakati mahsusi ili sasa tuweze kufika kwa wafugaji na wavuvi nchi nzima tukahamishe na kuwasimamia katika kuhakikisha kwamba wanapiga hatua ya kimaendeleo yao wenyewe kiuchumi lakini pia vilevile kupiga hatua kuwa katika mchango mahsusi kabisa wa pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba sisi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi tuko tayari, tutakwenda Nkasi na tutafika kote katika nchi hii walipo wafugaji na wavuvi. Kauli mbiu yetu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ufugaji ni maisha yetu, uvuvi ni maisha yetu na maisha yetu ni ufugaji na uvuvi kwa pamoja. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware, jiandae Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwa kuwa wananchi wengi wanahamasika na ufugaji wa samaki na kwa kuwa kuna uchache wa mbegu bora ya samaki na kusababisha samaki kutoka nje kuagizwa hasa mbegu za sato na hii inaweza kuwa hatarishi kwa samaki wetu asilia nchini. Napenda kujua Serikali inajipanga vipi kuboresha na kuwekeza katika tafiti mahsusi za uzalishaji wa mbegu bora za vifaranga wa samaki na pia kuboresha maeneo mahsusi, hizi *hatcheries* za uzalishaji wa vifaranga vya samaki nchini. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inahamasisha katika ufugaji wa samaki na tunazo taasisi zetu za utafiti mathalani *TAFIRI* na vituo vyetu vya uzalishaji wa vifaranga vya samaki kama kile kituo chetu kilichoko pale Morogoro Kingolwira. Vituo hivi vimejipanga vyema, vina vifaranga wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wafugaji wote wa samaki wawe tayari sasa kuweza kwenda katika vituo vyetu vilivyopo katika *zones* mbalimbali, kimojawapo hiki cha *zone* ya Mashariki hapa Morogoro kwenda kuchukua vifaranga bora kabisa na wataweza kufanya ufugaji huu wa samaki na kujipatia kipato na lishe wao wenyewe bila wasiwasi wowote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Ni ukweli usiopingika kwamba ufugaji wa samaki ni zao linaloweza kuleta matokeo ya haraka kwanza si katika tu suala la ajira lakini vilevile katika kipato cha mfugaji hata yule mwenye kipato cha chini. Hata

hivyo, liko tatizo moja kubwa sana la chakula cha samaki. Taasisi nyingi zikiwemo hizi zetu za Serikali ambazo zinaonesha utafiti wa ufugaji wa samaki wanakuonesha kwamba samaki hasa aina ya *tilapia* anapaswa afugwe ndani ya miezi sita awe ameshafikia uzito usiopungua nusu kilo kwa kula chakula chenye *formula* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza unapokuja kwenye hali halisi wale samaki wanalishwa zaidi mpaka wakati mwingine mwaka mmoja pasipokufikia uzito ule. Kutokana na hali hiyo wakulima au wafugaji wengi wanakata tamaa katika hili zoezi zima la ufugaji wa samaki. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuhakikisha utafiti madhubuti unafanyika ili ile *formula* inayotolewa iweze kuleta tija kwa wafugaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba udhaifu umeonekana kwa samaki wetu wanaofugwa hasa hao *tilapia* ambapo kutokana na chakula wanacholishwa wanachukua muda mrefu lakini ukuaji wao wa kuweza kufikia nusu kilo na sentimeta 50 ili waweze kuvuliwa umekuwa sio wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la ufugaji wa samaki kwa maana ya *aqua culture* katika nchi yetu ni jipya. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa tunayo Kurugenzi mahsusi kabisa inayohusika na jambo hili la *aqua culture* na kupitia tafiti zetu mbalimbali za *TAFIRI* na vyuo vyetu vingine tunafanya jitihada za kuhakikisha tunaondoa tatizo hili la chakula cha mifugo hii ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wafugaji wote wa samaki nchini kwamba, baada ya muda siyo mrefu watafiti wetu hawa watabaini na kugundua lishe iliyo bora zaidi ili kuweza kukidhi mahitaji ya soko na mahitaji ya wafugaji wetu. Waendelee kujiandaa na kuendelea kuhamasishana katika ufugaji wa samaki, tatizo la chakula cha mifugo hii ya samaki litakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael.

Na. 25

**Uchakavu wa Gereza la Karanga**

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL** aliuliza:-

Gereza la Karanga ni chakavu na lina uhaba wa samani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulikarabati gereza hilo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha za kutosha za uendeshaji ili kununua samani pamoja na vifaa vingine vitakavyosaidia kutoa huduma kwa wafungwa na mahabusu gerezani hapo?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna maswali matano na muda wetu umekwisha, sasa niwaambie tu kwamba kuanzia sasa hakutakuwa na maswali ya nyongeza zaidi ya maswali ya msingi**.** Swali la Mazingira limechukua muda mwingi sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Gereza la Karanga linakabiliwa na uchakavu wa miundombinu na hali hiyo imetokana na majengo na miundombinu ya gereza hilo kuwa

ya tangu mwaka 1949 likiwa na uwezo wa kuhifadhi wahalifu 814 na wahalifu waliopo sasa ni takriban 1,200. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inatekeleza mpango wa muda mrefu wa kuyaboresha majengo hayo kwa kuyafanyia ukarabati mkubwa unaolenga kuyaimarisha na kuyaboresha pamoja na kuyafanyia upanuzi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na mpango wa kupeleka fedha za maendeleo kwa ajili ya ukarabati na ununuzi wa samani katika magereza yote nchini likiwemo Gereza la Karanga. Aidha, kutokana na ufinyu wa bajeti, fedha hizo zimekuwa zikitolewa kwa awamu katika magereza mbalimbali nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Raphael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Gereza la Karanga lina tatizo kubwa sana la vyombo vya usafiri kwa maana ya magari. Naomba majibu ya Serikali kwamba ina mpango gani wa kununua gari ili kusaidia wafungwa wanaokata rufaa pamoja na askari ili kulinda usalama wa wafungwa kwa sababu gari lililopo ni chakavu sana na hata matairi halina?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Gereza la Karanga limekuwa na tatizo la madeni makubwa kwa matibabu ya wafungwa wanaotibiwa nje ya zahanati ya gereza hilo. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba madeni yanayodaiwa gereza yanalipwa ili wafungwa waendelee kupata huduma ya matibabu? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna matatizo ya upungufu wa magari katika Jeshi la Magereza maeneo mbalimbali nchini ikiwemo kwenye Gereza la Karanga kiasi tumefikia hatua ya kuweza kufikiria uwezekano kuwapatia magari

matano miongoni mwa magari 50 ambayo tunatarajia kuyapokea hivi karibuni kupitia Jeshi la Polisi. Tutalichukua hili suala la Gereza la Karanga tuone kama katika maeneo yaliyo na changamoto kubwa Karanga ni mojawapo ili tuweze kuangalia uwezekano wa kuwapatia gari yatakapokuwa yamewasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la zahanati, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunajitahidi kulipia madeni ya magereza ikiwemo zahanati kadri fedha zitakavyokuwa zinaingia. Pia nataka nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna uwekezaji mkubwa katika Gereza la Karanga wa kiwanda chini ya uwekezaji wa Shirika la *PPF* na moja katika mpango ambao tunataka kutekeleza ni ujenzi wa zahanati kubwa na ya kisasa katika gereza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,unaamini kwamba tutakapomaliza ujenzi huo, changamoto hii ya gharama ya matibabu kwa maeneo hayo itasaidia kupatiwa ufumbuzi. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira wakati matatizo haya tunayatatua kwa hatua za muda mfupi na muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Wizara hiyo, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

Na. 26

**Mkandarasi Aliyejenga Vituo vya Polisi Mkokotoni na Madungu**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Tarehe 25/5/2017 Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi akijibu swali Na. 274 kuhusu madai ya mkandarasi aliyejenga vituo vya polisi Mkokotoni Unguja na Madungu alisema, deni tayari limeshahakikiwa na kwamba atalipwa mara fedha zitakapotolewa lakini huu ni mwaka wa tano deni hilo halijalipwa:-

(a) Je, Serikali ina nia thabiti ya kumlipa mkandarasi?

(b) Je, Serikali inasubiri ipelekwe Mahakamani ndipo ilipe deni hilo?

(c) Je, huu ndiyo utawala bora ambao nchi yetu ina dhamira ya kuujenga?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua madeni ya wakandarasi wote akiwemo *Albatna Building Contractor* na ina nia ya dhati ya kuyalipa madeni yote ya wakandarasi na Washauri Elekezi waliohusika katika miradi mbalimbali ikiwemo miradi iliyohusisha Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Jeshi la Polisi limetenga jumla ya shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya kupunguza madeni ya wakandarasi waliotekeleza miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Mkokotoni ambao umetengewa jumla ya shilingi milioni 200 ikiwa ni sehemu ya deni ambalo anadai mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa hakuna deni la mzabuni au mtumishi ambalo halitalipwa kwani madeni yote yaliyohakikiwa yanaendelea kulipwa kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM JAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri wake kwa majibu yao ya umakini kabisa. Naomba kuuliza maswali madogo tu ya nyongeza yenye fungu (a) na (b):-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yako Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la msingi umesema Waziri amesema katika mwaka wa fedha 2017/2018 Jeshi la Polisi limetenga jumla ya shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya kupunguza madeni ya wakandarasi waliotekeleza miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa ujenzi wa huu wa Kituo cha Mkokotoni. Umetenga shilingi milioni 200 na kutenga maana yake ni kitu tayari umekiweka pembeni na huyu mtu ni mgonjwa, hili suala nimelisemea karibu mara nne katika chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini nije naye mguu kwa mguu ili asije akapata usumbufu apate haki yake hii, ili akamalize kituo hiki na yeye mwenyewe apate matibabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa vile deni hili lina muda mrefu kwa nini, Serikali au Wizara haitoi *priority* ikammalizia deni hili, ili kumaliza ujenzi huu wa vituo vyetu vilivyokuwa huko Unguja na Pemba? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kwa niaba ya Serikali kumpa pole sana huyu mkandarasi kutokana na maradhi ambayo ameyapata na tunamuombea Mwenyezi Mungu amjalie aweze kupona haraka. Nimuombe sana Mheshimiwa Mbunge hana haja ya kumhangaisha mkandarasi kuja naye hapa mguu kwa mguu, asiwe na wasiwasi wowote fedha hizi shilingi milioni 200 zimetengwa kwa ajili yake katika bajeti ya mwaka huu na kwa hiyo basi, fedha hizo zitakapokuwa zimeingia tu atalipwa bila hata kumsumbua mkandarasi kwa kuja naye hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kwamba lisiwe kipaumbele. Ni kipaumbele na ndiyo maana tukatenga hizo fedha kwa ajili ya kumlipa. Kwa hiyo, Mheshimiwa

Mbunge tunaomba vile vile awe na subira wakati tukisubiri fedha hizi wakati zitakapokuwa zimeingia na tutamlipa mara moja.

Na. 27

**Serikali Kuhamisha Bomba la Mafuta Eneo la Mji wa Makambako**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Bomba la mafuta la kwenda Zambia limepita katikati ya Mji wa Makambako na barabara ambayo ipo juu ya bomba hilo hairuhusiwi kutengenezwa hivyo kuwa na mashimo mengi na kuhatarisha maisha ya watu wanaoitumia barabara hiyo.

(a) Je, ni lini Serikali italihamisha bomba hilo?

(b) Je, kwa nini barabara hiyo isitengenezwe, ili wananchi waendelee kupita kwa urahisi wakati Serikali inajipanga kulihamisha bomba la mafuta?

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua usumbufu wanaopata wananchi wa Makambako kutokana na bomba la mafuta kwenda Zambia *(TAZAMA)* linalopita katika Mji wa Makambako. Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inawasiliana na Kampuni ya Tanzania na Zambia ya kusafirisha mafuta kutoka Tanzania kwenda Zambia *(TAZAMA Pipeline Limited)* kuainisha hatua stahiki zitakazochukuliwa kuondoa tatizo hilo. Wakati mawasiliano

yanafanyika pamoja na kuainisha hatua za gharama zitakazotumika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania itatengeneza maeneo yaliyoharibika, ili wananchi waweze kutumia barabara hiyo bila matatizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Niulize maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, lakini kabla sijauliza niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwake, vile vile kutokana na majibu mazuri ambayo yamelenga utekelezaji wa Ilani ya CCM kutatua kero za wananchi, kwa majibu haya nimefarijika sana, ni imani yangu kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa sababu eneo hili bomba la mafuta linapita nyuma ya Hospitali yetu ya Mji wa Makambako na linapita eneo la polisi pale na linapita kwenye maeneo ya wananchi kama ambavyo swali la msingi limesema.

Je, sasa kutokana na kwamba amesema atawatuma watu wa *TANROADS* ili waweze kwenda kuona na kushughulikia. Ni lini sasa hao watu wa *TANROADS* waende mapema ili kusudi kabla ya mvua za Disemba hazijaanza kunyesha ili kutatua kero ambayo ipo kwa sababu wananchi wanashindwa kupita na magari katika maeneo haya ambayo nimeyataja?

Mheshimiwa Mweyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi baada ya kumalizika Bunge hili, ili akaone maeneo ambayo yametajwa katika maeneo hayo? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pongezi zake nazipokea, lakini pia eneo hili linalopita

bomba lina changamoto ipo. Pamoja na kuleta shida kwa wananchi kupita katika eneo hili, lakini pia ni hatari ndio maana niseme tu kwamba, nimeagiza mara moja sehemu hii iangaliwe, ili pia tuweze kuepusha hatari kwa sababu kama bomba linapita maeneo ya makazi na huu Mji wa Makambako ni mji ambao unakua kwa haraka, shughuli za kibinadamu nazo zimeongezeka, ili waangalie pamoja na kuona kama kuna hatari yoyote inaweza ikatokea, kitaalam tuweze kulisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge. Nitatembelea Makambako ili pia nione hizi hatua za haraka zimechukuliwa na kwamba tatizo hili linaweza kumalizika. Ahsante.

Na. 28

**Ujenzi wa Barabara ya Kibaya – Kiteto kwenda Kongwa**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Kibaya, Wilayani Kiteto kwenda Ranchi ya *NARCO* iliyoko Kongwa inaharibiwa na magari makubwa yanayobeba mahindi kutoka Kiteto kwenda soko maarufu la Kibaigwa, Kongwa na Serikali ilishaahidi kuijenga kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa ina urefu wa kilometa 430. Barabara hii inaunganisha Mikoa ya Arusha, Manyara na Dodoma, na

lengo la Serikali ni kuijenga kwa kiwango cha lami. Barabara hii itakapokamilika itarahisisha usafirishaji wa mazao na mifugo katika Mikoa ya Arusha, Manyara na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018 Serikali imetenga jumla ya shilingi 1,350,000,000 kwa ajili ya kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii. Aidha, mnamo tarehe 21 Aprili, 2017 Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imesaini mkataba na Mhandisi Mshauri Kampuni ya *Cheil Engineering Company Limited* kutoka Korea ya Kusini ikishirikiana na Kampuni ya *Inter-consult* ya Tanzania kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuikamilisha katika kipindi cha miezi 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya usanifu itakapokamilika na kujua gharama halisi za mradi Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* inaendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii, ili iendelee kupitika kwa urahisi wakati tunaendelea na maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Umbulla.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru sana Serikali kwa juhudi kubwa ya kujenga barabara nyingi za lami hapa nchini, lakini naomba nioneshe masikitiko yangu kuhusu uwiano wa barabara za lami hapa nchini, kwa sababu, tunajua baadhi ya wilaya zina barabara za lami vichochorini hadi katika vijiji mbalimbali. Katika mkoa wetu wa Manyara, hususan Wilaya za Kiteto, Simanjiro na Mbulu, hakuna barabara ya lami inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, labda tukiacha Wilaya ya Hanang ambayo kwa bahati imepitiwa na Barabara ya kutoka Singida, Babati, Arusha, tunaomba kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kuna barabara ambazo Serikali imedhamiria kujenga; kwa nini Serikali isiweke kipaumbele kuhakikisha kwamba, barabara zilizoko kwenye Ilani ya Uchaguzi kwa kulenga zile Wilaya ambazo hakuna barabara za lami zinazounganisha makao makuu ya mkoa na Makao Makuu ya Wilaya? Kwa nini isitoe kipaumbele ikajenga barabara za lami, hususan lami kutoka Wilaya ya Kiteto – Kibaya hadi Makao Makuu Babati? Lami kutoka Mbulu hadi Babati na lami kutoka Simanjiro – Orkesmet hadi Babati? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nilipokee hili suala la kuangalia uwiano kama ushauri, lakini yako mambo ambayo lazima tuyatazame wakati tunakamilisha ujenzi wa barabara, kwa sababu eneo hili analolizungumza Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba kuna uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na mifugo. Mimi nilipata *brief* ya mkoa juu ya *network* ya barabara za Manyara na niseme baada ya Bunge hili pia nitakwenda kwa ajili kuangalia miradi inayoendelea, lakini pia kuweza kuona siku za usoni tuweze kukimbizia hii barabara iweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiri tu kwamba, Serikali ya Awamu hii ya Tano imefanya kazi kubwa, kwa sababu barabara za lami zilizotengenezwa katika kipindi cha miaka miwili zenye urefu wa kilometa 1,500 si haba, kiasi cha shilingi trilioni 1.8 kimetumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kukamilika kwa barabara hizi ni fursa pia, ya kwenda kushughulikia barabara nyingine ambazo tayari shughuli za upembuzi yakinifu zinaendelea, zitakapokamilika tuweze kwenda kujenga barabara hizi. Ahsante.

Na. 29

## Ujenzi wa Soko la Mnanila - Buhigwe

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Soko la Kimataifa la Mnanila – Buhigwe lilikuwa kwenye mpango wa kujengwa mwaka 2012/2013, lakini hadi sasa soko hilo halijajengwa.

Je, ni lini soko hilo litajengwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba nitangulie kumjibu Mheshimiwa Albert Obama na nichukue fursa hii kutambua na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge huyo kwa juhudi zake za kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa Soko la Mnanila–Buhigwe. Mheshimiwa Obama pia aliwahi kuuliza swali kama hili ambalo lilijibiwa Juni, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimeeleza katika jibu langu la awali, Serikali kupitia Mradi wa Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo Wilayani *(District Agriculture Sector Investments Project - DASIP)* ilipanga kujenga masoko saba ya mpakani katika maeneo ya Mnanila - Buhigwe, Mutukula - Misenyi, Kabanga - Ngara, Nkwenda - Kyerwa na Muronga - Kyerwa, Remagwe - Tarime na Busoka - Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ujenzi wa masoko mawili ya Mnanila na Mutukula haukuingia katika mpango wa ujenzi wa masoko hayo kutokana na kucheleweshwa kwa taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi. Mradi wa *DASIP* ulihitimishwa mwaka 2013/2014 na masoko matano yaliyokuwa yanajengwa yalikamilika kwa kiwango cha kati ya asilimia 40 mpaka 60. Wizara ya Kilimo ambayo ndio ilikuwa inasimamia mradi wa *DASIP* inaendelea na juhudi za

kukamilisha ujenzi wa masoko hayo kwa kutumia vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Mradi wa *DASIP* kufikia ukomo Serikali inaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe kuingiza ujenzi wa soko hilo katika Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Halmashauri ili kufanikisha ujenzi wa soko hilo na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itaendelea kutafuta wahisani wa maendeleo, ili kujenga soko la mpakani eneo la Mnanila.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Obama.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii niulize maswali mawili ya nyongeza na ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwamba kuanzia mwaka ule mlipatambua kwamba pana umuhimu wa kuwa na soko la kimataifa na ni ukweli ulio wazi kwamba sisi tuko mpakani na tumepakana kwa ukaribu na tunafanya biashara ya pamoja. Lakini huu mpango mliokuwanao wa masoko ya mpakani bado ni muhimu sana kutekelezwa katika maeneo haya ya Mnanila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu niseme eneo tulilokuwa tumelitoa halikuwa na fidia yoyote. Sasa nataka kujua Wizara sasa itafanyaje kwa sababu umetuomba Halmashauri tuweze kuliweka kwenye mpango, lakini fedha zinazohitajika kujenga soko hili ni kubwa.

Je, Wizara itafanya nini sasa kuhakikisha kwamba, soko hili linajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tumejenga soko lingine la mpakani ambalo liko maeneo ya Kijiji cha Nyamugali; tulikuwa na mpango vilevile Kibande na Kilelema, lakini tuna changamoto ya daraja sasa hivi kwenye Soko la Nyamugali ambalo Wizara yako ilijenga, ili watu wa

Burundi waweze kuingia nchini. Je, Wizara iko tayari kutujengea daraja Nyamugali pale, ili wafanyabiashara waweze kupita kirahisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Obama, kwamba suala la masoko ya mipakani ni suala muhimu na linaongeza tija katika uzalishaji na ukuzaji wa mazao ya viwanda ambayo Serikali yetu ndicho inachokisisitiza. Sasa kama ambavyo nimemueleza awali, ni kwamba nimuombe aweke uhitaji wa soko hilo katika bajeti ya halmashauri, na wakati huo kama tulivyoahidi tutaendelea kuwatafuta wahisani mbalimbali ili kuweza kusaidia ujenzi wa soko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Daraja la Mto Kigale, kama sikosei ulivyotamka, ni kwamba kama ambavyo tunazidi kusisitiza kwamba biashara za mipakani kati ya nchi na nchi mbali tu ya kufanya shughuli za kibiashara zinajenga pia mahusiano na kuziwezesha nchi hizi mbili kuishi vizuri na kuondoa umaskini kwa pamoja. Kwa hiyo, mimi suala hilo nalichukua na litaendelea kufanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mimi nikisimama, ninyi mnakaa.

Waheshimiwa Wabunge, ni kipindi sasa cha wageni ambao wako Bungeni; tunaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika, wageni watatu wa Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye (Mbunge), Naibu Waziri Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni familia yake. Wametokea Jijini Dar es Salaam akiongozwa na mke wake Bi Rosemary Nditiye, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Wabunge Ikupa S. Alex Mbunge, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu ambao ni watumishi wa huduma ya *Sinai Prophet* kutoka Mkoa wa Dar es Salaam.

Pia tunao wageni nane wa Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri Mbunge, ambao ni Wenyeviti wa UVCCM wa Wilaya kutoka Mkoa wa Dodoma, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Aeshi Hilaly Mbunge, ambao ni viongozi kutoka Taasisi ya *Union Trust investment* iliyopo Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Emmanuel P. John Mbunge ambao ni watumishi wa *Red Cross Society Tanzania* kutoka maeneo mbalimbali nchini Tanzania, karibuni Dodoma.

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 94 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari Bwawani iliyoko Mkoani Morogoro, karibuni sana, mmependeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wanaotoka mikoa inayozalisha zao la mahindi, Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi na Iringa mnaombwa mkutane kantini baada ya kuahirisha Bunge, saa 07:00 mchana leo. *(Makofi)*

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wako.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Chacha.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha, Waheshimiwa muda wetu umekwenda, nitachukua wachache tu, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Mlinga na sio wote mkapata vilevile. Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza wakati wachangiaji wakichangia asubuhi ya leo hapa Bungeni; Waheshimiwa Msigwa na mwenzie Sugu wamezungumza sana kuhusiana na suala la Mheshimiwa Rais kufanya ziara Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, kama maneno haya yataruhusiwa kuendelea kuzungumzwa humu Bungeni, yanatukarahisha sana sisi watu wa Kanda ya Ziwa, tunajiona kana kwamba hatuna umuhimu kwa Mheshimiwa Rais wetu kupita Kanda ya Rais. Mimi ni Mwenyekiti wa Chama, bahati nzuri ziara zote zile ninakuwepo, sijawahi kuona Mheshimiwa Rais amekuja kwa ziara tu ambayo haina manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anatembea kwa gari, anapokuja Kanda ya Ziwa anakuwa na ziara pengine Uganda ama Rwanda, anatumia gari katika kubana matumizi. Kutumia *jet* kwenda Kampala au Rwanda ni gharama kubwa kuliko kutumia magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine Mheshimiwa Rais kwao ni Kanda ya Ziwa, sijawahi kuona Marais wengine waliotawala wanapokuwa wanapata likizo ya kusalimia familia zao wanaenda mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza anapopumzika Mheshimiwa Rais wanataka aende Iringa, Mtwara au Serengeti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marais wengine wote wamekuwa wakipumzika makwao, yule mtu ana wazazi na ndugu anahitaji kuzungumza nao. Lakini kila wakisimama humu tunaonekana kana kwamba pengine sisi watu wa Geita kuna tatizo Rais kuja kupumzika kwao. Tuchukue mifano, kama hili ni kosa kuwa Kanda ya Ziwa, Mheshimiwa Rais ameshafanya ziara Arusha, Tanga, Singida, Mtwara, Dodoma na Morogoro, hii yote sio Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hajapanda kanda ya wakina Msigwa ni bora wakawa wastaarabu wakasubiri ili apange kwenda kanda hii, wasitake kuleta hoja humu ndani ya ukanda. Tukianza kuzungumza mambo ya ukanda, watu wamepeana vyeo kwa ushemeji humu na wachumba zao. Sasa wakiendelea kusema mimi nadhani na sisi tunaoumia tuna sababu ya kumtaja kila mtu na *partner* wake aliyemleta humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili ulikemee, linatukaraisha sisi watu wa Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, nakubaliana kabisa na hoja ya Mheshimiwa Musukuma. Bunge hili tuwe na tahadhari; jana Mheshimiwa Spika alitoa tahadhari. Tuwe na tahadhari ya maneno yetu na tujipime tunaposema maneno yetu; Bunge hili lisitumike kugawa Watanzania. Mheshimiwa Rais ana ratiba zake, ratiba zake haziingiliwi na Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ukitazama Mheshimiwa Rais ana ziara nchini Uganda, ameona ni bora aunganishe kanda hiyo pamoja na nchini Uganda ili kupunguza gharama za matumizi ambazo Serikali yake inaisimamia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naomba masuala ya ukanda na masuala ya udini tusiyaendekeze, nchi yetu siku zote imesimama pamoja, Bunge moja, Rais mmoja chini ya Mungu mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ryoba!

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na ile ya 46(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi wakati ninajibiwa swali namba 18 kwa niaba ya Mheshimiwa Sabreena, niliuliza maswali mawili ya nyongeza. Nauliza Mwongozo wangu kwa swali la pili la nyongeza ambalo niliuliza kuhusu Mji wa Mugumu ambapo tulipewa kilometa mbili za lami lakini tumetangaza mara tatu hatujapata mkandarasi kwa sababu ya uchache wa zile kilometa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema mimi niende nikamwambie Mkurugenzi aende sijui akaulize kwa wakurugenzi wenzake huko. Yaani ananiagiza mimi nikamwambie Mkurugenzi, si yeye.

Sasa mimi nilitaka kujua Mkurugenzi anahusikaje na barabara? Tumetunga hapa sheria ambayo imeanzisha chombo kinaitwa *TARURA,* chombo ambacho ni *independent body,* kinahusika na mambo ya barabara, barabara zipo chini ya Mkurugenzi. Sasa ananiambia mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sikujibiwa vizuri, ninaomba swali langu ambalo nimeuliza la nyongeza la pili lijibiwe vizuri kama inavyotakiwa si jinsi alivyoniambia mimi nikamwambie Mkurugenzi, mimi ni nani na nina mahusiano gani mimi na Mkurugenzi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunapoanza Bunge tuna Kanuni, kama Mbunge haridhiki na swali kuna Kanuni ya 46. Ipitie Kanuni 46 itakupa mwongozo wa kupata haki ya jibu lako. Ahsante, Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, natumia Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilivyotaka niulize swali la nyongeza kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani kutoa

tangazo mapema kwamba hutahitaji maswali ya nyongeza na katika hayo maswali ya nyongeza kama kuna Mbunge yoyote awe ana hoja ambayo angehitaji kupata maelezo ya Waziri au Ofisi husika ndio fursa ya kuweza kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako sasa baada ya kuwa umezuia swali la nyongeza kwamba tarehe 24 na tarehe 25 Oktoba, askari wa *FFU* walifunga mtaa wa Mongolandege, Mombasa, Mazizini na Gongolamboto wakapiga watu sana, wakavunja vunja meza za akinamama, wakapiga vijana wa bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haikutosha tarehe 25 wakaamkia tena kazi ileile, wanasimamisha magari kutoka hapa Magereza unashushwa unaruka kichura chura, tunapozungumza kuna watu wamevunjika miguu, wameporwa fedha zao halafu wakachukua watu kama 100 wakawasambaza vituo tofauti tofauti. Tumeuliza wale watu hawajulikani walipo, *OCD* anasema hajui, lakini mpaka leo hakuna kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Mwongozo wako mambo kama haya yakitokea, unapokuwa unazuia maswali ya nyongeza, umeruhusu maswali mengi sana pale nyuma si kwamba sio muhimu lakini muhimu ukaweza kugawa nafasi hizi ili tuweze kupata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wewe kwa sasa unisaidie kwa heshima kubwa unafahamu kwamba sasa pale Ukonga hali ni tete. Sasa wale askari walikuwa wamepanga kwenye nyumba za wananchi, walikuwa na mahusiano mazuri, sasa hivi maaskari wanapaswa kufukuzwa zile nyumba, kuna uhasama mkubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo mawili naomba unisaidie, moja, madhara yaliyofanyika tathmini ifanyike, waliopigwa wakaporwa mali zao akina mama lishe wale wana *VICOBA* wanadaiwa, nani anafidia hiyo hali?

La pili, Wizara yenye dhamana itoe taarifa...

**MWENYEKITI:** Huwezi kuuliza mwongozo mara mbili…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Wamechukua dhamana gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, huwezi kuwa na hoja mbili kwenye mwongozo. Mwongozo wako uwe mmoja tu kwanza kaa chini umeshamaliza. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kiti kikiamua muda wa kuanza na kumaliza hakuna Mbunge mwenye haki ya kuhoji kiti. Swali la mazingira lilichukua muda mwingi sana kwa hiyo ninapoamua swali la msingi kanuni zetu zinatuelekeza swali la msingi ambalo Mbunge huuliza swali la msingi na maswali ya nyongeza mawili, ndio mwenye haki. Haya mengine ni ridhaa ya kiti tu, kiti kikiamua unapata na nimeamua hakuna maswali ya msingi mengine kama ya kwako wewe Waitara. Na leo nimekustahi tu kwa sababu ukikihoji kiti ni matatizo. Hilo lingine Serikali mmelisikia, mtalitafutia majibu ili mumpe Mbunge. Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Taifa letu sasa hivi limekumbwa na janga kubwa la uporomokaji wa maadili, uvunjifu wa sheria na katiba ya nchi. Uporomokaji huo wa maadili unasababishwa na mwenendo mbovu kupita kiasi wa mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mtandao wa *Instagram* umekuwa kitovu kikubwa cha watu kujitangaza kwa biashara za ngono, uhamasishaji wa mapenzi ya jinsia moja, kutoa habari za uzushi, kwa mfao kuna viongozi wanatoa habari za uzushi, kuna mtu aliwahi kujiuzulu *Instagram* akasema amemwandikia barua Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Instagram* imekuwa kitovu kikubwa cha kutoa taarifa za uongo, kutoa taarifa ambazo zinasababisha taharuki katika nchi. Serikali imekuwa wenyewe wanaita kuchamba, Serikali imekuwa ikivuliwa nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WhatsApp* ina makundi sasa hivi ya watu kutangaza biashara za mapenzi (ngono), kurusha picha za utupu, kufundisha yaani shughuli mbalimbali za kuharibu maadili ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba Mwongozo wako, pamoja na mitandao mingine, *TCRA,* Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, lipi ni jukumu lao katika hili? Maana taifa letu maadili yanaporomoka, wanafunzi hawa sasa hivi ukiwaona ni wakubwa kuliko mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mwongozo wako kwenye hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mlinga, Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Mbunge amejikita katika kuona ni namna gani mitandao ya kijamii na teknolojia mbalimbali ambazo zimeingia katika nchi yetu zinavyoweza kutumika ama kujenga au kubomoa maadili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tumesikia; na tunazo taarifa kwamba yapo baadhi ya maswali katika Mkutano huu wa Bunge yameulizwa kwa Serikali yetu kuhusiana na masuala yanayofanana na jambo alilolileta Mheshimiwa Mbunge hapa ndani leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa nafasi mbalimbali Serikali itaendelea kutoa ufafanuzi, maelekezo na pia kutoa ufafanuzi wa kisheria na hivyo basi tutaendelea kuboresha maadili mema katika nchi yetu ya Tanzania kwa kupitia sheria tulizonazo na teknolojia inayozidi kukua katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa kuna wageni waliachwa wa Mheshimiwa Flatey. Ni wageni wanne wadau

wa maendeleo kutoka Jimbo la Mbulu Vijijini wakiongozwa na Ndugu Petro Sule, karibuni. *(Makofi)*

Katibu!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya dharura.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, kaa chini.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya dharura.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kaa chini au unataka kwenda kupima?

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Kuna upendeleo bwana.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**KAULI ZA MAWAZIRI**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi mapana ya wananchi na wanafunzi wa elimu ya juu, naomba kauli ya Serikali iwasilishwe kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uridhie ombi letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Kauli ya Serikali itakuwa kesho kwa maslahi mapana na nimewakubalia.

Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza mjadala wa mpango.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Tukae. Mheshimiwa Hawa Ghasia, ajiandae Mheshimiwa Njeza. Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wizara nzima ya Fedha kwa mwongozo mzuri wa mpango wa mwaka 2018/2019 na kweli unatuonesha mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nijikite zaidi kwenye vipaumbele vile vinne vya mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha kwanza kinaelezea kuhusu viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda na mimi naona hiki ni kipaumbele kizuri sana; lakini ningependa zaidi kuona kwamba hiki kipaumbele kinajikita zaidi kwenye kilimo kwa sababu viwanda vyetu, uchumi wetu wa Tanzania kwa kiasi kikubwa utategemea kilimo ambacho kinaajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja na mpango wake kwa mwaka huo pamoja na bajeti, uangalie ni namna gani utajikita kuinua kilimo Tanzania kwa sababu hiki kilimo ndio kitatupelekea kupata malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu. Nalizungumzia hilo la kilimo kwa sababu kubwa ambayo imejitokeza hivi karibuni. Wakulima kwa kiasi kikubwa wamezalisha sana mazao, hasa nafaka. Hata hivyo leo hii ukiangalia bei ya nafaka hasa mahindi na mbaazi ziko chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ijaribu kuangalia ni namna gani iwasaidie wakulima yale mazao wanayoyazalisha bei iweze kuwa inaeleweka, kuwe na *price stabilization.* Vilevile kuwe na masoko ya uhakika. Tusipokuwa na masoko ya uhakika, bei ya mazao yetu isipoeleweka kwa kweli nchi yetu itakuwa katika hali ambayo sio nzuri na uchumi wetu utakuwa katika hali mbaya kwa sababu bei zetu za mazao ukilinganisha na wenzetu sisi zipo chini sana. Kwa hiyo, ningeomba hapa Serikali iangalie jinsi gani ambavyo tutaanzisha masoko ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimesikiliza kwenye taarifa ya habari walikuwa wanazungumzia kuhusu *commodity exchange market.* Ikianza mapema hiyo nafikiri inaweza kutusaidia sana kuhakikisha kuwa mazao yetu yanakuwa na bei inayoeleweka na vile vile kunakuwa na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kilimo kinahitaji zaidi pembejeo, napenda niishukuru Serikali kwa mpango wake wa kuagiza mbolea kwa jumla *(bulky procurement);* hii imesaidia sana kiasi ambacho mbolea leo za *DAP* bei imeteremka karibu nusu. Kwa kule kwetu *DAP* inanunuliwa kwa shilingi 51,000 kwa mfuko wa kilo 50 na *Urea* inanunuliwa kwa shilingi 41,000 kwa mfuko, hayo ni mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi mbolea kushuka bei namna hiyo bado ninaona kuna njia ambazo

zinaweza kusaidia mbolea ikashuka zaidi; kama tukiboresha zaidi miundombinu ya barabara na miundombinu ya reli. Kwa sehemu ambazo tuko ukanda wa reli ya *TAZARA,* kama *TAZARA* ikiboreshwa, bei ya mbolea inaweza kushuka zaidi. Kwa hiyo, ninaomba katika hiki kipaumbele cha kufunganisha uchumi na maendeleo tuangalie zaidi ni namna gani wananchi wanaweza kufaidi bei ya pembejeo zikawa chini zaidi kwa kuboresha huduma za miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri vilevile Serikali iliangalie suala la afya, hasa miundombinu ya afya. Wananchi wamejenga zahanati nyingi, wamejenga vituo vya afya na bado vipo kwenye mtambaapanya wakitegemea kuwa Serikali itakuja kumalizia. Katika huu mpango unaokuja katika hii bajeti inayokuja ninapendekeza kipaumbele kiwe kumalizia hizi zahanati na vituo vya afya ambavyo kwa kiasi kikubwa wananchi wameshajenga na wengine bado wanaendelea kujenga. Kwa hiyo, upendeleo uwe kwa wananchi wale ambao wameshafikia hatua nzuri, tuweze kuwatia nguvu ili waweze kuendelea kuchangia katika ujenzi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la maji. Maji kwa wananchi wetu hasa vijijini na mijini ni muhimu sana, kwa hiyo, tunapoangalia maendeleo tuangalie ni namna gani hii miundombinu ya maji hasa kwa vijijini itaweza kuboreshwa. Kwa kiasi kikubwa Serikali imewekeza sana kwenye miundombinu, imetoa hela nyingi sana kwa ajili ya miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii miundombinu sehemu nyingi likiwemo Jimbo langu la Mbeya Vijijini bado haifanyi kazi. Ukiangalia kwa kule Mbeya Vijijini tulipata miradi ya vijiji kumi na miradi ile asilimia 80 ya pesa ilishakwenda, lakini mpaka leo ni mradi mmoja tu ndiyo umekabidhiwa. Sasa katika hii bajeti, iangalie ni namna gani hii miradi iweze kukamilika ili tuweze kuanzisha miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika miradi ya maji ninapendekeza kwa kule Mbeya tungeanza na vyanzo vingine

mbadala. Kuna chanzo cha Mto Kiwira, naomba kipaumbele kiwepo cha chanzo cha Mto Kiwira kwa ajili ya kupeleka maji Wilaya yetu ya Mbeya hasa Jimbo la Mbeya Vijijini, nafikiri itatukomboa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linaweza kutusaidia katika mpango mzima wa maji nafikiri ni kuunganisha hizi mamlaka; mamlaka za maji mijini na mamlaka za miji midogo *(clustering).* Kwa hiyo, napendekeza katika mpango wa bajeti unaokuja tuhakikishe kuwa Mamlaka ya Maji Jiji la Mbeya inaunganishwa na Mamlaka ya Maji Mbalizi, lakini vilevile na miji midogo mingine ya Mbeya Vijijini iweze kuunganishwa ili kupata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni kipaumbele ni suala la ujenzi wa mazingira wezeshi, nafikiri hili ni muhimu sana kwa sababu unapojenga uchumi kusipokuwa na mazingira wezeshi kutakuwa na changamoto nyingi sana ili kufikia malengo yetu. Pendekezo langu hapa ni kwamba tungeangalia ni namna gani wakati tunaendelea na ujenzi wa reli ya *standard gauge* na ile miradi mingine ya kimkakati vile vile tuboreshe na reli yetu ya *TAZARA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuboresha reli ya *TAZARA* tunaomba vilevile tujenge bandari kavu ambayo itasaidia kwa mizigo inayoenda nchi za nje; Zambia, Malawi, Kongo, na nchi nyingine zinazotuzunguka ambazo tuna ushindani nazo kwa bandari za Beira Msumbiji, Afrika Kusini na Angola.

Tukiboresha hii *TAZARA* na tukajenga bandari kavu na pia tukajenga reli ambayo itatuunganisha sisi na wenzetu wa Malawi kuanzia pale Mbeya na hii reli vilevile itatusaidia kuboresha huduma za meli mbili ambazo zimeshaundwa na zimeshaanza kufanya kazi kwenye Ziwa letu la Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa mazingira...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Nashukuru sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, ajiandae Mheshimiwa Hassan Masala.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoongoza nchi hii, lakini pia na Baraza zima la Mawaziri, tunawaomba nendeni mkamwambie Mheshimiwa Rais asilegeze uzi. Nchi yetu hii inahitaji mwendo wa Rais sasa, si lelemama na maneno mzahamzaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza na hatua ya kwanza kumuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba mfumo wetu wa ukusanyaji wa mapato utazamwe. Nchi yetu bila mapato ya kutosha kutoka ndani ya nchi hatuwezi kufika mahali popote. Sasa hivi mfumo unaotumika unagandamiza sana wale walipakodi kulingana na mfumo na utaratibu unaotumika. Mimi ninaomba basi, tufanye utaratibu wa Serikali kutazama upya mfumo mzima wa ukusanyaji wa mapato yetu ya Serikali ili walau walipakodi wawe marafiki wa Serikali na wavae moyo wa uzalendo katika kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kutazama upya ahadi za Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ameahidi mambo mengi sana na kama hatutaweka kwenye utaratibu ule wa kawaida wa kuangalia ni namna gani zile ahadi zake zinaanza kutekelezwa kwa awamu kila mwaka ili ziweze kuingia kwenye mfumo wa bajeti ya Serikali, hatuwezi kufika mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo. mimi naona kama kule kwetu Mbulu ahadi zote alizoahidi bado hazijatekelezwa, tunandelea kusubiri Serikali itekeleze kwa sababu tayari viashiria vimeonekana. Naipongeza Serikali

kwa jinsi ambavyo tayari wametangaza tenda ya Daraja la Magara na mwaka huu wa fedha ambao tuko nao watatekeleza ahadi hiyo ya Rais ili kujibu kiu na matarajio ya wananchi wa Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya lami aliyoahidi kule Mjini Mbulu, naona *tender* pia imetangazwa. Tunaishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo *tender* ya ahadi ya Rais kilometa tano pale Mjini Mbulu imetangazwa, na ni imani yangu kuwa itatekelezwa katika mwaka huu wa bajeti kwa kadri ambavyo imetangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani tunaweza kuzungumza mambo mengi sana, lakini bila pesa, bila nchi kuwa na uchumi, hata tukiongea namna gani mafanikio yetu hayatafika mahali popote. Kwa hiyo, katika eneo hili la ahadi za Mheshimiwa Rais, ni imani yangu kuanzia mwaka huu wa fedha tunaouendea kila mahali pataguswa ili iingie kwenye mfumo wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali na iweze kutekelezwa. Mheshimiwa Rais ameahidi mambo mengi na kwa kadri alivyoahidi si rahisi kutekeleza kwa mwaka mmoja, lakini kwa kuwa Serikali ni endelevu na ina miaka mitano, ni imani yangu itatekeleza ahadi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kadri walivyoongelea kilio kikubwa cha bei ya mazao ya wananchi. Kwa sasa wananchi wanahangaika kutafuta masoko yao. Tuone Serikali itumie wataalam na mifumo mbalimbali na marafiki zetu ili kuona ni namna gani tunapata bei nzuri ya mazao ya wananchi ikiwemo mifugo na mazao yanayotokana na kilimo ili kuwezesha mwananchi wa chini kupata uchumi unaoweza kumudu mahitaji na matarajio ya nchi na katika kujihudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninapenda nizungumze kwa ufupi sana kutokana na muda ni eneo la miradi ya maendeleo. Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alianzisha mpango kabambe wa ujenzi wa maabara katika Halmashauri mbalimbali nchini. Hivi sasa bado baadhi ya maeneo mengi

kwenye ujenzi wa zile maabara hakujakamilika na wananchi wamechanga vya kutosha. Tunaomba fedha hizi za ukamilishaji wa maeneo ya viporo ya maendeleo zingeweza kutafutwa kwa kila mwaka kwa awamu ili miradi ile ya maabara iweze kutekelezwa na iweze kufanya vizuri kwa maana ya kuwahudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la elimu tunaomba Wizara ya Elimu iangalie upya mfumo wa wakaguzi wa elimu katika nchi yetu. Wakaguzi wetu wa elimu mara nyingi wanapata wakati mgumu wa kukosa vitendea kazi na fedha za kuwawezesha ili waweze kutekeleza matakwa yale ya kukagua kiwango cha elimu, ubora wa elimu na hali yao ya kutekeleza mipango ya kazi kwa kuwa tunawalipa katika mishahara na kwa kuwa wao tayari tumewaajiri. Mfumo huu ungewekwa kama mfumo ule wa ukaguzi kitaifa kwa maana ya *CAG* hata kwa Taifa letu huu ukaguzi wa elimu ungejengewa mfumo mzuri kutoka ngazi ya Taifa mpaka kwenye Halmashauri zetu ungeweza kufanya vizuri na kuweza kujenga utaratibu unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viporo vingi na kwa kweli kwa kadri ambavyo Serikali imefanya kazi katika mwaka huu mmoja tu wa Serikali wa 2016/2017 kazi nyingi sana zilifanyika na inaonekana tukiendelea kutafuta Wakala wa Maji, tukaendelea kutafuta na mawakala wengine, tukatafuta fedha kwenye vyanzo vya ndani vikaungana na fedha za wabia wa maendeleo, basi tunaweza tukafanya vizuri zaidi ili tuweze kukamilisha miradi iliyokusudiwa na kutoa huduma stahiki kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi niombe utaratibu wa upelekaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika mwaka huu ulioisha wa 2016/2017 haukuweza kukaa vizuri kwa sababu fedha zilikuwa zinapelekwa, lakini hazilingani na asilimia. Tunaomba fedha za miradi ya maendeleo zitolewe kwa asilimia, kama Halmashauri ilikusudiwa bilioni 50 basi kama tunatoa asilimia 30, iwe ni asilimia 30 kwa namna ambavyo kila Halmashauri inapata kwa sababu yule aliyepangiwa fedha nyingi atapata asilimia 30 na yule

ambaye fedha zake kwa mpango wa maendeleo si nyingi atapata zile asilimia 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimemfuatilia Mheshimiwa Rais kwenye ziara yake siku moja, alitoa taarifa ya kwamba fedha za miradi ya maendeleo zimetolewa kwa asilimia 90, naomba tusimdanganye na kumpotosha Mheshimiwa Rais kumpelekea utaratibu wa taarifa isiyo rasmi, tuwe tunapeleka kile halisi ambacho tumepeleka kwa sababu tunaingia mgongano kati yetu sisi na wananchi kwamba zile fedha zimepelekwa wapi, mbona kwenye taarifa ya Rais zimepelekwa zote ama zimepelekwa asilimia 90. Mambo kama haya yanaipa mkanganyiko mamlaka ya kuchaguliwa kwa maana ya Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge na hata viongozi wengine, lakini pia na watendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuliongelea ni eneo hili la uadilifu, uwajibikaji kwenye mifumo ya Serikali; bado kuna baadhi ya watendaji Serikali hawajabadilika. Tunaomba Serikali itazame upya watendaji wake wote kwa kila Wizara ili wabadilike, wawajibike kwa wananchi, watoe kauli nzuri kwa wananchi, waweze kuwahudumia wananchi na waweze kujitambua kwamba wao wana dhamana kama ambavyo wamekabidhiwa na watumie lugha nzuri wanapowahudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika ofisi nyingine majibu wanayopewa watumishi wadogo na wananchi hayalingani kabisa na Serikali ya Awamu ya Tano. Ninaomba sana kama itawezekana Serikali ifungue macho, hasa wale wenye mamlaka ya kusimamia rasilimali viongozi na rasilimali wananchi ili watu ambao wanawajibu wananchi wetu vibaya kwenye ofisi za Serikali, ambao hawataki kuwajibika waweze kuchunguzwa na waondoke kwenye mfumo mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nalizungumza kwa sababu unapoona huku juu Serikali inafanya kazi vizuri sana,

kule kwenye maofisi bado kuna watu wamekaa kwenye ma-*bench* hawawajibiki, kutoa *file* meza moja kwenda meza ya pili inachukua mwezi mzima, hii inatukatisha tamaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeweka nia ya dhati ya kufanya mapitio ya barabara ya Karatu – Mbulu hadi kule Haydom kwa ajili ya kufungua wananchi wa Wilaya ya Mbulu ili waweze kuungana na wananchi wengine kwa mfumo wa barabara ya lami kwa maana ya kuwaunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana, itachochea uchumi kwa Wilaya ya Mbulu na Wilaya za Karatu na Wilaya nyingine za kule Mkalama na Shinyanga kwa sababu ukanda huu wa juu wa bonde la ufa ni kama umezungukwa na uzio ambao umefungwa moja kwa moja na Ukanda wa Bonde la Ufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kuchukua saruji ya Dangote, kama unataka kupeka Mbulu ni lazima kwanza iende Singida, halafu Itoke Singida ije Mbulu. Kwa hiyo gharama yake ni tofauti kabisa na maeneo mengine katika Tanzania yetu kwa kuwa barabara ni ya udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukienda kule Tanga ukachukua saruji kule ukataka kuleta hiyo saruji, ni lazima iende kwanza Mto wa Mbu, ije Karatu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** …ije Mbulu. Kwa hiyo tunaomba sana barabara hii ni ya muhimu sana… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hassan Masala, ajiandae Mheshimiwa Heche.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa katika hotuba yake, na katika vipaumbele ambavyo vimepangwa hivi vinne, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza yeye pamoja na ofisi yake, lakini pia niipongeze Serikali kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wanaifanya kwa ajili ya kuhakikisha Watanzania wanapata maendeleo. Sambamba na haya, yapo maeneo ambayo ninapenda nitumie nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Waziri na wadau wote ambao wanahusika katika kuendelea kutuletea shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapojadili viwanda huwezi kutenganisha na suala zima la kilimo. Moja ya vipaumbele vikubwa ambavyo tumeviweka kwenye mpango ni suala la uendelezaji wa viwanda vyetu. Kazi kubwa Mheshimiwa Rais wetu amekuwa anaifanya ya kuhakikisha tunafufua viwanda ambavyo vime-*cease* kufanya kazi, lakini pia kuhakikisha tunaleta wawekezaji wengine ambao wanafungua viwanda vipya, lakini bado zipo changamoto ambazo nilikuwa naziona; watu wa Wizara ambao wanatuwekea mipango hii lazima pia waangalie vipaumbele vyao waelekeze katika maeneo ambayo tayari tumeshaanza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika upande wa kilimo wa zao la korosho Ukanda wa Kusini, Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa sasa hivi shughuli kubwa ambayo inatuingizia kipato ni zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wengi wako kule, makampuni mengi yako kule, lakini pia hata kipato cha wananchi wetu kwa kipindi kama hiki kinakuwa ni kikubwa sana, lakini uwekezaji gani tumeufanya sisi kama Serikali ninafikiri ni jambo ambalo Wizara lazima sasa waaangalie na waelekeze nguvu zao na macho yao ili kuhakikisha zao hili linafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuishuru Serikali, mwaka jana kuja msimu huu wametusaidia kutua *sulfur* kwa ajili ya kuhakikisha tunafanya uzalishaji mkubwa. Hata hivyo bado ninaomba niishauri Wizara au nimshauri Mheshimiwa Dkt. Mpango waone umuhimu sasa wa kufungua kiwanda ambacho kitakwenda kuzalisha *sulfur* katika Mkoa wa Lindi. *Sulfur* hii itasaidia wakulima wengi wa maeneo yote ya mkoa na wale wote wanaotumia kulima zao hili waweze kupata huduma ya pembejeo kwa karibu na kwa gharama nafuu zaidi. Msimu huu tumepata bure, lakini bado tumekuwa na changamoto ya uchache wa *sulfur* tuliyopokea, lakini pia tumepata changamoto ya kuchelewa kwa *sulfur* ambayo kimsingi imeshusha kidogo uzalishaji wa zao hili kubwa la biashara ambalo sasa hivi angalau tunaweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe katika eneo hili la uwekezaji katika viwanda, moja ya vipaumbele vyetu hebu tuangalie namna ambavyo tunaweza tukatengeneza kiwanda cha *sulfur* na mipango hiyo tayari ilishakuwepo, muhimu ni kuanza utekelezaji. Kwa hiyo katika bajeti zetu na mipango yetu ninaomba hili wazo nililete ili tuweze kulipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili katika kilimo ni suala zima la uanzishwaji pia wa viwanda vya magunia au vifungashio. Sasa hivi tunapata magunia kutoka nje, tunapata magunia kutoka maeneo ya mbali, hii imeleta shida sana pia kwa wakulima wetu katika msimu kama huu. Hii ni fursa nyingine ambayo Serikali ingeweza kutengeneza fedha kubwa sana kupitia utengenezaji wa kiwanda ambacho kitaenda kutoa magunia na kwa sababu mahitaji ni makubwa, basi ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aone umuhimu sasa wa kuelekeza nguvu katika eneo hili la viwanda tuweze kupata kiwanda ambacho kitazalisha magunia na vifungashio vyote ambavyo vitawasaidia wakulima wetu wa zao hili la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu katika kilimo, ninapenda pia kuzungumzia suala la kilimo cha mbaazi. Hili

zao kwa muda mrefu tumekuja hapa Bungeni, tumelalamikia na kutoa maelekezo lakini bado majibu ya kutosheleza mpaka sasa hivi hatujapata. Leo hii ukienda katika Jimbo la Nachingwea kwa msimu mzima wakulima wamejitokeza, wamelima mbaazi nyingi sana ambao sasa hivi hazina soko na hazima kazi yoyote ya kufanya, lakini bado nasikitika kusema Wizara mpaka sasa hivi hawana kauli yoyote ambayo wameitoa juu ya zao hili la mbaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha, lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Tizeba ni muhimu sasa atoke na atoe tamko rasmi la kusema nini hatma ya zao la mbaazi kwa wakulima wetu ambao tuliwahamasisha, wakajitokeza kuchukua muda wao, lakini pia wakaongeza mashamba yao na kulima zao ambalo mikataba imevunjwa, soko hakuna. Sasa hivi mbaaza kilo shilingi 150, shilingi 200, lakini nilitegemea Serikali itasema kwamba kama tumekosa wanunuzi ambao tulikuwa tunawategemea kutoka India nini mbadala wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mwakilishi wa wananchi na kwa sababu wananchi wenyewe wanatusikiliza sasa tunafika wakati tunapata uvivu hata kuwahamasisha wananchi wetu waweze kuitikiwa wito wa kulima zao ambalo halina soko, lakini nilikuwa nataka nitoe ushauri ufuatao ili haya yote yaendane kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza watu wa Wizara ya Kilimo lazima watueleze idara zao zinazohusiana na utafiti zinafanya kazi gani, idara zao zinazohusika na suala la kutafuta masoko zinafanya kazi gani? Kama tulijua India watavunja mkataba wa kununua mbaazi kwa nini hawakutuambia? Na sheria au hatua gani zimechukuliwa pale mkataba unapovunjwa katikati? Ni harasa kiasi gani ambayo wakulima wetu wameipata kwa kuweka mazao yao ya mbaazi ghalani bila kununuliwa mpaka sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba ushauri au kumtaka Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aseme kwa msimu ujao

tuna sababu ya kulima mbaazi? Kama tunakiwa tulime, tulime tani ngapi na tutazipeleka wapi? Vinginevyo hatutakwenda kuwashawishi tena wakulima wetu walime zao ambalo halina faida badala yake ni bora tukaelekeza nguvu kulima kitu ambacho kitaenda kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni eneo la zao la muhogo, Wachina wameshaingia mkataba wa kutaka muhogo kutoka nchi ya Tanzani. Moja maeneo ambayo tunalima mihogo kwa wingi na miogo bora ni pamoja na Mkoa wa Lindi hasa Wilaya ya Nachingwea. Ni vizuri sasa tunapojadili habari ya viwanda lazima tuseme tuna mkakati gani wa kweli kujenga kiwanda kitakachoshughulika na suala nzima la ununuzi wa mihogo na usindikaji wa mihogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi nikiangalia kablasha zote sijaona sehemu yoyote ambako tunaelekezwa au kuna maelekezo ambayo yataonesha nia thabiti ya Serikali katika kwenda kuwekeza ili wakulima wetu wapate sasa mazao mbadala badala ya kung'ang'ania kulima mbaazi ambazo tume-*fail* basi nizuri tukaelekeza nguvu katika mazao kama korosho pamoja na mihogo ambayo tunafikiri itatuletea tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie eneo ambalo linaenda sambamba na viwanda. Huwezi kujadili viwanda, huwezi kujadili uzalishaji wowote kama hatuwezi upatikanaji wa nishati ya uhakika. Bado Mkoa wa Lindi Wilaya ya Nachingwea na maeneo yote yanayozunguka kanda nzima tatizo la umeme limekuwa ni kiwazo kikubwa sana. Leo wananchi wetu hawatuelewi sisi wawakilishi wao, wananchi wetu hawaielewi Serikali inafanya nini ikiwa bado wananchi mpaka sasa hivi tunawahamasisha wafanye shughuli za kiuchumi lakini hawana umeme ambao zitawasaidia kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa heshima na taadhima, tunatambua kazi

inayofanyika na sisi tunathamini, lakini ni muhimu sasa tukalichukua hili kama jambo la dharura. Tumeaidiwa sana kwamba mitambo itafungwa mashine zitanunuliwa; gesi inatoka kwetu lakini bado Mikoa ya Lindi na Mtwara mpaka sasa hivi hali ni mbaya hali ya uchumi inadidimia kwa sababu hakuna umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, kama tatizo ni fedha tunaomba utupatie fedha au uwape watu wa Wizara fedha au uwape watu wa Wizara ya fedha waweze kwenda kurekebisha upatikanaji wa umeme ili wananchi waweze kuzalisha na waweze kufanya shughuli za kiuchumi. Sasa hivi hakuna shughuli inayofanyika ukienda katika maeneo yale, ndani ya dakika mbili umeme unakatika, imekuwa ni kero na ni imekuwa hadha kubwa sana kwa shughuli za maendeleo. Kila Mbunge atakae simama anayetoka kwenye maeneo hayo lazima atazunguza hoja ya umeme. Tunaomba sasa ifike wakati Mheshimiwa Waziri mipango tuayoipanga kikanda ni lazima sasa tuelekeze mambo muhimu ikiwemo hili eneo la nishati ambalo sisi tunafikiri kwetu ni jambo la msingi na ni jambo ambalo litatusaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kujadili viwanda, huwezi kujadili uchumi kama huna mawasiliano ya uhakika na yaliyo safi. Serikali imefanya kazi kubwa mimi natambua, kwa mwaka wa jana na mwaka wa juzi mpaka kufika sasa hivi ziko ahadi ambazo tayari zimeshaanza kutolewa na nina hakika zitatekelezwa. Hata hivyo naomba Mheshimiwa Waziri katika mipango uliyoipanga, ziko barabara za kimkakati na za kiuchumi ambazo huwezi kujadili maendeleo ya nchi hii ukaziacha barabara hizo bila kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunajadili namna ya kuunganisha barabara za Wilayani kwetu, barabara ya kutoka Nachingwea - Masasi, Nachingwea - Nanganga kwa muda mrefu tumehaidiwa kupata fedha lakini bado utekelezaji haujaanza. Kwa mara ya mwisho tayari tumeshaambiwa wakandarasi wamepatikana bado kupitisha tenda kwa ajili ya kwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri jambo hili ni la msingi sana. Leo hii tunatoa tani kwa tani za korosho kutoka Nachingwea kupeleka Mtwara kupeleka Lindi, hakuna sehemu ambako tunazipitisha na zile korosho zikafika kwa usalama. Magari mengi yameacha kufanya kazi kwa sababu barabara ni mbovu. Ni fedha kiasi gani tunapoteza kwa sababu ya ubovu wa barabara? Tunaomba ahadi ya kutengenezewa kwa kiwango cha lami na bahati nzuri matamko ya viongozi wetu yameshatolewa, tunaomba utekelezaji uanze katika mwaka huu wa fedha kwa wale wakandarasi ambao wameshapewa hii kazi. Hapa muhimu ni kupata fedha kwa ajili ya kuanza kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha tulichangiwa au tuliele...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Heche, ajiandae Mheshimiwa Masoud.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba hii kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Mheshimiwa Waziri Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye anatulinda, ambaye yeye si binadamu, yeye anatupenda hata kama wengine wanatuchukia na Mwenyezi Mungu ameokoa maisha ya Tundu Lissu napenda sana kumshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka yangu miwili ambayo nimekaa hapa Bungeni kumekuwa na Mpango wa mwaka 2016/2017 na bajeti yake, kukawepo na Mpango wa mwaka 2017/2018 na sasa Mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2018/2019 na bajeti zinakuwa zinapitishwa. Pia mojawapo ya kazi ambazo Bunge hili limekuwa likifanya ni kutunga sheria na mambo mengine yote ambayo yapo kwa

mujibu wa vitabu na katiba ya nchi hii na sheria zetu kwa ajili ya kufanywa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najiuliza na kila Mbunge hapa aende ajiulize kama kuna sababu yoyote ya kuendelea kuwa tunaleta hiki kinachoitwa mpango, hiki kinachoitwa bajeti na sheria tunatunga humu tunatumia pesa za walipa kodi maskini wakati Serikali na Rais mwenyewe hafuati hiki kinachoitwa mpango, hafuati sheria na hafuati bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mambo ya mwanzo mawili. La kwanza Mheshimiwa Mpango kila kitu mnachopanga kwa ajili ya wananchi mwisho wake kinaishia kwenye vijiji au vitongoji au mitaa. Bahati mbaya hao Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji na Mitaa wanachaguliwa na wananchi, wanapigiwa kura kama sisi Wabunge kama Madiwani na kwa kampeni.

Kwanza jambo la kwanza hawana *security of tenure,* anakwenda tu Mkuu wa Wilaya anaweza akamfukuza Mwenyekiti wa Kijiji aliyechaguliwa na wananchi kwa kumsimamisha. Anamfukuza kazi wakati Mkuu wa Wilaya huyo hajateuliwa, hajui hata kura aliyogombea pengine kura za maoni akapigwa, anamfukuza Mwenyekiti wa Kijiji bila kufuata utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili mmekuwa mkiwaaidi kwenye mipango yote, na mnategemea hawa watu ndio wasimamie kazi zile za kuendeleza maendeleo ili mpande kwenye majukwaa mjisifie. Unamlipa Mtendaji wa Kijiji, unamlipa Mtendaji wa Kata lakini haumlipi Mwenyekiti wa Kijiji ambaye ndiye bosi wa Mtendaji. Kwa hiyo, mimi nataka niwaambiwe Wenyeviti wote wa Vijiji wa CHADEMA na wa CCM; hapa ni *issue* ya maslahi yao, wajue Serikali hii ya CCM haitaki kulipa maslahi yao na inawadharau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni aibu wakati mwingine Serikali inakuja inazungumza hapa na inasema uongo na wananchi kule chini wapo wanaona hivi vitu.

Unajua wakati mwingine kuna vitu mnaweza mkasema tumefanya, ukasema tumenunua ndege kwa pesa zetu wenyewe kumbe umekopa, hiyo wananchi wa kawaida hawatakuewa. Lakini ukija ukasema kuna madawa hospitali na siku hizi bahati nzuri *tv* zipo, wananchi wakiwa hospitali wanaona na wakati hakuna madawa, hivi wewe Mheshimiwa Waziri unavyojibu hapa wale wananchi waliopo kule hospitali wanakuelewaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 13 dereva wangu alikatwa panga saa nne usiku, na mimi nilimpeleka kwenye Hospitali ya Wilaya ya Tarime, hakuna *gloves,* hakuna gozi, hakuna hata sindano ya dawa ya ganzi. Sasa mimi namshangaa Mheshimiwa Waziri wa Afya anakuja hapa anasema madawa yamejaa tele. Sasa labda mtuambie kuna maeneo mnapeleka na maeneo mengine mnayabagua, lakini kama sivyo si vyema mkaja hapa mkazungumza mambo ambayo mnajua Serikali yenu hii imeshindwa na hivyo vitu haviko kule vijijini. Haviko kwenye vituo vya afya, haviko kwenye Hospitali za Wilaya, haviko wala kwenye zahanati na hizi zahanati wanajenga wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Mpango ni mchumi. Huwezi kufanya maendeleo kwa kuharibu maendeleo yaliyokwishafikiwa, yaani huwezi leo ukakuta mtu amejenga nyumba yake, ukabomoa nyumba yake halafu akawa analala barabarani kama watu wa Kimara walivyo sasa hivi na maeneo mengine ya nchi hii, halafu ukasema umefanya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kurudisha watu nyuma. Na unawaambia kwa kiburi kabisa kwamba hakuna fidia yoyote watakayoipata, watu wameishi tangu mwaka 1974, tangu miaka 1980 leo unakuja unapomoa nyumba zao, watoto wa watu wanalala nje. Hebu jiulizeni miongoni mwenu kama ni wewe Mpango kama mtu mwingine yeyote, hebu jaribu kujiweka kwenye hiyo picha, umeangaika umejenga na ndiyo maisha yako yote kesho unajikuta umelala barabarani, jaribu kujiweka hapo kwa sababu sisi pia ni binadamu kama wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekit, miji ya watu inachomwa huko vijijini kwa kisingizio kwamba mnahamisha watu kutoka kwenye mapori. Mnachoma nyumba za watu moto. Watu maskini wamejenga nyumba za miti na majani ma-*DC* wanakwenda wana-*set fire* kwenye miji ya watu, watoto wanabaki wanabaki nje unga unaungua madaso, vitaa na vitanda kama anakagodoro kanaungua anarudi kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ya watu ya watu maskini, alizungumza jana Mheshimiwa Ryoba hapa, wanakamata mifugo, Serikali hii ya CCM inakamata mifugo ya watu. Sisi Wakurya kwa mfano unakuwa na ng'ombe ndiyo unatumia ng'ombe hao kwa kufanyia kazi ya kulima. Unalima chakula, unakuwa nacho kwenye ghala ng'ombe ndiyo wanatoa maziwa unatumia kama mboga. Leo unakamata ng'ombe wa mtu wote unauza, tena kwa shilingi 70,000 na unamshitaki huyo mtu unamfunga na haya yamefanyika mpaka kule Chato mpaka maeneo mengine ya kwa kina Mheshimiwa Doto kule Bukombe wanajua hili ninalolizungumza. Mnarudisha watu kwenye umaskini, ufukara, mnawaambiwa watu mnawaendeleza subiri hasira yake mtaiona mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya yakuwa yanafanyika bila kufuata mpango wa Serikali wala bila kufuata utaratibu. Ukichukua kitabu cha mwaka 2016/2017 zilitengwa pesa shilingi bilioni mbili kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa uwanja wa ndege wa Chato. Juzi nikaona kwenye *tv* kwamba zimeshatolewa shilingi bilioni 39 kwa ajili ya ujenzi wa uwanja na uwanja umejengwa umefikia kiwango cha asilimia 63; *running way* yake ina ukubwa wa kilometa tatu wakati uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Dar es Salamu una running way ya kilometa 3.3; uwanja huu unazidi uwanja wa ndege wa Mkoa wa Kagera, unazidi uwanja wa Dodoma, unazidi uwanja wa Mwanza.

Sasa nataka Mheshimiwa Mpango aje awajibu Watanzania, kama tuna haja ya kuwa na Bunge hili ambalo halijapanga mipango, lakini Serikali ya CCM na Rais

wanatekeleza. Ni lini *tender* ya uwanja ule ilikuwa *floated* na ni nani na nani walishindana kwenye hiyo *tender* ili wapate huo uwanja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa shilingi bilioni 39 zimetoka kwenye bajeti gani ya Serikali ambayo haikupitiwa na Bunge hili? Hizi shilingi bilioni 39 zimetoka kwenye chanzo gani? Tunataka Mheshimiwa Mpango atujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi sina chuki yoyote na uwanja kwenda Geita sina chuki hiyo, wala Chato lakini uwanja huu ungewekwa walau Geita kwenye maeneo ya Geita au...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Taarifa Mwenyekiti.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji anachokizungumza ni kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Geita na kwa nini anatuchagulia sehemu ya kuweka? Tuchukue mifano uwanja wa Mkoa wa Mara uko Musoma, lakini kuna watu wanakaa Nyamongo anakotoka yeye kwanini usingejengwa Tarime ambako ni *center* kubwa?

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo.

**MHE. JOHN W. HECHE** Mheshimiwa Mwenyekiti, sihitaji hata kupokea hiyo taarifa kwa sababu haelewi kwamba uwanja wa Musoma uko Makao Makuu ya Mkoa kama Geita ambapo kama ungewekwa Geita ungekuwa Makao Makuu ya Mkoa ambako ndiko kwenye *economic activites* kubwa zaidi kuliko Chato Wilayani, ambako kwanza labda haelewi, kutoka Mwanza Mjini kwenda Geita ni kilometa 105, ambako kuna uwanja mkubwa. Kutoka Chato kwenda Geita ni kilometa 185. Nini maana ya uwanja huu kupelekwa kule? Wanakwenda kubeba nini? *(Makofi)*

Mnakwenda kubeba ng'ombe mle ndani ndiyo maana mmeweka taa za kuongozea gari barabarani wakati hakuna gari hata tatu zinazopita kwenye ile barabara? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoangalia huu uwanja unatengewa pesa nyingi za watanzania mabilioni nikiwemo mimi. Lazima *values for money* ionekane, lazima uwanja huu uonekane utabeba nini na utazalisha nini, siyo tuchukue uwanja tupeleke kama Mobutu alivyo...

**NAIBU WAZIRI MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Heche.

**NAIBU WAZIRI MADINI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba kumtaarifu ndugu msemaji kwamba Arusha kuna uwanja mkubwa wa ndege na kutoka Arusha kwenda Kia ni kilometa 40 tu kuna uwanja mwingine wa ndege. Kwa hiyo, tunaomba atambue kwamba zaidi ya kilometa180 ni nyingi sana ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Heche taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa *order*. Mwacheni msemaji achangie.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie muda wangu kidogo tafadhali. Huyu ni Naibu Waziri ambaye hajui kwamba *KIA* ni uwanja wa ndege wa Kilimanjaro na uwanja wa Arusha ni wa Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninachojaribu kuzungumza, wala sina chuki na watu wa Geita, ninachozungumza ni kwamba uwanja huu uweze

kufungamanishwa na uchumi, unategemea makao Makuu ya Mkoa ndiko kwenye *economic activities* nyingi; na kama kuna uwanja wa karibu mtu ata-*opt* kushukia Mwanza badala ya kwenda kushukia Chato ambako ni kilometa 180.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nimeshakuongeza muda Mheshimiwa Heche, ahsante. Mheshimiwa Masoud alafu jiandae Mheshimiwa Chumi.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kunijalia uzima na afya njema kuweza kuchangia mapendekezo ya Mpango huu wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze wananchi wangu wa Jimbo la Mtambile kwa kuendelea kuniamini na kunipa baraka zote, halikadhalika nikipongeze Chama Wananchi *CUF* kwa kuendelea kuwa imara katika harakati mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nataka nianze kumwambia ndugu yangu Dkt. Philip Mpango wa Waziri wa Mpango, yeye mwenyewe kwanza alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mipango kwa muda wa miaka kumi, sasa kama si hivyo naomba basi niendelee kwa kusema kwamba mpango huu ambao umetuletea ningependa kujua kwanza tathimini ya mpango uliopita umefikia hatua gani na wakati huu mpango huu mpya, hilo lilikuwa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kile kinachoitwa mkakati wa Tanzania ya viwanda kuelekea uchumi wa kati, ni kwamba Serikali mara kadhaa imekuja hapa Bungeni ikituambia kwamba ina mkakati wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa. Serikali mara kadhaa imekuwa ikituambia viwanda vyote vile ambavyo vilibinafsishwa lakini baadaye

wakapewa wawekezaji ambao hawaviendelezi watatajwa majina yao na kitajulikana nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujielekeza katika viwanda vilivyobinafsishwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, vile viwanda vya korosho, Mheshimiwa Waziri utuambie leo hii viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa ambavyo asili yake/mwanzo wake kulikwepo na mkopo kutoka Italy na Japan kwenye miaka ya 1980 dola milioni 20, zikachukuliwa kujengwa viwanda vile ili kuondokana na tatizo la kuuza korosho ghafi nje ya nchi.

Leo viwanda vimebinafsishwa, vimechukuliwa, mmewapa mliowapa, mmepeana sadaka kwa watu mnaojuana. Mheshimiwa Waziri naomba unipe ujasiri na utuambie hapa viwanda vile mmewapa akina nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi unaonekana mmepeana wenyewe kwa wenyewe kwa bei chee, vigogo wa Serikalini, utuambie ni akina nani na kwa nini haviendelezwi? Leo bei ya korosho ghafi Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na Morogoro imefika shilingi 3,800; lakini mnasema kwamba watu wale mtawaita, mpaka leo hawapo. Mtuambie mmewapa akina nani? Mtuambie Kiwanda cha Lindi Mjini nani anayemiliki? *Newala One* nani anayemiliki? *Newala Two* nani anayemiliki?, *TANITA* yote *One* na *Two* ni nani anayemiliki? Kwa nini hamtuambii? Kwa nini hamko wazi kutuambia viwanda hivyo? Na mnasema kwenye Katiba ukurasa wa 20 kwenye haki na wajibu kuna haki ya usawa, kwamba watu wote ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuulize Mheshimiwa Waziri haki sawa iende kwa nani? Na wale wasiotenda haki? Nashangaa kwamba leo mmesema mtatuletea majina ya watu wote waliochukua viwanda hawaviendelezi, mkasema mko wazi, lakini leo hakuna kitu, wengine mnawataja, wengine hamuwataji, shida! Hilo ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna kiwanda mtuambie cha kusindika samaki *(TAFICO)* Dar es

Salaam hatua yake imefikia wapi? Anayemiliki ni nani? Mtuletee Bungeni mtueleweshe, wananchi wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala zima la wafanyabiashara wadogo wadogo. Kuna malalamiko makubwa ya jinsi gani ya hali ya maisha wakati huu ilivyokuwa ni ngumu. Mzunguko wa pesa umekuwa ni mdogo, wafanyabiashara mbalimbali katika masoko ya vyakula na mboga mboga wamekuwa wakilalamika, Kariakoo maduka yamefungwa wateja wamepungua, Mheshimiwa Waziri Mpango anasema uchumi umeimarika, uchumi kuimarika kuna takwimu zenu mnazosema umeimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi niseme, si muda mrefu hapa Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara au Lindi kule Kusini amezungumzia tatizo la wakulima wa mbaazi. Leo mbaazi kilo shilingi 150, shilingi 200, shilingi 300. Mheshimiwa wewe mwenyewe unajua kwamba kuna Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kifungu cha 43(1) kinaeleza kwamba ikiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazikutosha kutokana na majukumu yake Serikali inaweza kuwasilisha Bungeni bajeti ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli mnawapenda wananchi wa Lindi na Mtwara Serikali mnashindwa nini kuleta hapa Bungeni kuongeza bajeti ya kununua mbaazi za Lindi na Mtwara na maeneo mengine kama ya huko Babati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mnazungumzia MKUKUTA kumbe MKUKUTA wa maneno. Serikali leteni hapa bajeti ya nyongeza ili sisi Wabunge tuweze kuidhinisha ili wakulima wale ambao wamegharamika kwa gharama kubwa ya kulima mbaazi, mbaazi zao zisiharibike, lakini leo wapi maskini! Tuseme nini? Huu ndio wakati maalum wa kuweza kuboresha maisha ya wakulima, lakini nashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista umekaa miaka mingi, washauri wenzako hawa kwamba wakulima wanapata shida sana. Serikali ilete Bungeni tuidhinishe bajeti

ya nyongeza ili mbaazi zinunuliwe ili angalau wakulima wapate manufaa wasiingie kwenye hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mambo kama haya yananitia uchungu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la wavuvi. Serikali mara nyingi imekuwa ikijisifia hapa Bungeni namna ya kuchoma nyavu tu za wavuvi. Mheshimiwa Mpango utuambie una mpango gani wa kuwaboresha wavuvi wadogo wadogo kwa kuwapa mikopo, kuwasaidia wavuvi katika bahari na katika maziwa? Mpango uko wapi? Nimeangalia mpango wako huu na nilikwambia mwanzo, tathmini yako ya mpango uliopita uko wapi kuhusu maeneo mbalimbali? Wavuvi wameachwa, wametupwa, hakuna jambo lolote la kuwasaidia, hakuna mikopo kwa wavuvi wa baharini na wale wa kwenye maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikuombe Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango Waziri wa Mpango utuambie una mkakati gani, una mpango gani hasa wa kuboresha maisha haya ya wavuvi wadogo wadogo? Kuna kurasa kidogo tu umeandika hapa kuhusu wavuvi, lakini tatizo ni kubwa. Mvuvi ambaye ana mtungi wake wa gesi akienda katika maeneo mbalimbali anaambiwa anafanya uvuvi haramu, anakamatwa na anachomewa nyavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mpango atuambie dagaa mchele wale ambao bila shaka nawe umeshawahi kula, wanavuliwa na nyavu ya aina gani? Utuambie. Umekula dagaa mchele wewe, mara nyingi, nasikia unapenda kweli. Tuambie nyavu zile mnazochoma, dagaa mchele winavuliwa na nyavu za aina gani? Mumekuwa mabingwa wa kuchomna nyavu kila wakati mnajisifia, utuambie mikakati yao. Wavuvi mikopo hamuwapi, nyavu zao mnachoma, mikakati ya kuboresha hakuna, Serikali haina mpango wa kununua meli za kisasa na kubwa za kuvua bahari kuu, Serikali haina mpango wowote. Mnakuja na mipango, mna mpango au mna mipangilio? Shida. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyeiti, suala la maji hapa ni kizungumkuti cha muda wa miaka na miaka. Leo wananchi wa Tabora hawa rafiki zangu Wanyamwezi na Wakisukuma ukifika wakati wa uchaguzi kampeni yao kubwa ni maji, wanakwenda kwenye majukwaa; *"nalilomba kura zing'we mnine pye bhose wadugu wanu"* hawa. *(Makofi/Kicheko)*

Leo waambie Tabora, Bwawa la Igombe limekauka, yaani Tabora maji hakuna kabisa. Kuna Mradi wa Ziwa Victoria ni wa muda mrefu, wa muda mfupi uko wapi? Ukienda zako Njombe Mjini, Makambako, Wanging'ombe, Maswa, Buchosa huko kwa Mheshimiwa Waziri kote maji ni shida, ni malalamiko matupu, kwenye *tv* tunaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule Magu tarafa ya Ndagalu maji hakuna, nako waende wakaseme sasa; *"nalilomba kura zing'we mnine pye bhose wadugu wanu"* kauli ndio shida, ndio taabu kama wataipata hawa, hawapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji limekuwa la muda mrefu, tangu enzi na enzi. Sasa mkakati wa muda mrefu ni Ziwa Victoria, mkakati wa muda mfupi wa pale Tabora ni upi? Wale wenye visima vyao ni wachache sana, leo kuna shida kubwa lakini Serikali tukisema sisi eehh jamani! Serikali ichangamke, ihangaike kutafuta maeneo mengine au njia mbadala ya kuweza kupatikana kwa maji. Tatizo hakuna chochote kinachokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie suala la mafao ya wastaafu. Hamgusii mpango endelevu wa mafao ya wastaafu, hakuna, *pension* iliyobakia ni ile ile. Leo walimu uliwaahidi miaka kadhaa kwamba mtawapa *teaching allowance*, posho ya kufundishia lakini hakuna kitu, posho ya kufundishia hakuna kwa walimu na ile ndiyo motisha. Mliahidi tangu mwaka 2012, tena ni ninyi wenyewe Serikali kwamba mtatoa *teaching allowance* kwa walimu; hakuna kitu, mpango uko wapi? Mna mpango wa kweli wa kuboresha maslahi ya walimu? Maana mnasema elimu inashuka, tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani Serikali sasa inagalie mapungufu yake mbalimbali lakini mhakikishe kwamba wastaafu na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante; Mheshimiwa Chumi ajiandae Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nipende kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Mafinga Mjini na Halmashauri ya Mji wa Mafinga, kwamba ni Halmashauri mpya tuna mwaka wa pili tu lakini katika matokeo ya darasa la saba tumeshika nafasi ya tano katika halmashauri zaidi ya 150. Ni jambo ambalo tunajivunia, ni kutokana na ushirikiano kati ya wananchi, mimi Mbunge wao, Waheshimiwa Madiwani, watumishi, walimu na wananchi kwa ujumla na ninaomba tuendelee kushirikiana ili ikiwezekana mwakani tufike tatu bora

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda pia kuishukuru Serikali; tulikuwa na kilio kwa ajili ya bweni la Shule ya Msingi Maalum Makalala; ilituletea fedha milioni mia moja. Na kwa kutumia muundo wa *force account* tumejenga bweni zuri, Mheshimiwa Profesa Ndalichako alifika pale, tena tumetumia shilingi milioni 76 na fedha iliyobaki tutanunua samani kwa ajili ya bweni lile. Haya yote ni ushirikiano kati ya sisi viongozi na wananchi wa Mafinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuishukuru Serikali kwa ajili ya ujenzi unaondelea wa tanki la maji la ujazo wa lita 500,000 pale Kinyanambo. Pia Serikali imetupa kibali tayari mkandarasia atakwenda *site* kuanza kujenga tanki la lita 90,000 pale Kijiji cha Maduma na mradi wa maji kule Bumilayinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imetupatia shilingi milioni 500 ambazo tutaendelea na ujenzi kuimarisha kituo cha afya pale Ihongole. Haya ni mambo ambayo lazima tuyapongeze na kama hiyo haitoshi jana katika taarifa nimeona TAMISEMI inatuletea watumishi wa kada ya afya asiopungua saba ili kuendelea kuimarisha huduma za afya katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga na Hospitali ya Mafinga ambayo inahudumia Wilaya nzima ya Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika *Road Fund* niiombe Serikali, tuna viporo, wakandarasi wamefanyakazi na wanatudai takribani shilingi milioni 212 fedha za mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru wahisani na marafiki mbalimbali ambao wanashirikiana na Ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga katika kuimarisha huduma za afya na elimu. Napenda kuushukuru Ubalozi wa Japan wametupatia fedha tunajenga pale *theatre* ya kisasa kabisa. Sasa niiombe Serikali hususani Wizar ya Fedha; kwa kuwa fedha zile zilikuwa *centralized* sasa *TBA* ambao tumewapa ile kazi *speed* yao inakuwa ndogo kwa sababu bado hawajpelekewa fedha na yule mhisani angependa kuona maendeleo ya ile kazi.

Kwa hiyo, ningeomba Hazina watusaidie *TBA* wapate fedha hizo ili *speed* ya kazi iende sambamba na jinsi ambavyo mhisani yule alikuwa ametuelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba vikundi vya wajasiriamali, kama ulivyokuja ukatuelekeza tuvipike, tumevipika vimeiva, tunakusubiri kwa hamu sana uje utuletee ile mikopo ya riba nafuu.

Sambamba na hilo, wakati tunajadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa, mara zote nimesema, *engine* ya ufanikishaji wa utekelezaji wa mpango ni utumishi wa umma. Kama *morale* ya watumishi wa umma iko chini kama wanavyotumia lugha ya siku hizi kwamba vyuma

vimekaza ni wazi kuwa mafanikio ya kufanikisha Mpango yatakuwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo niipongeze Serikali, kwamba hatimaye baada ya uhakiki wa muda mrefu sasa imeangalia *welfare* ya watumishi, na ninaamini *morale* itapanda kwa sababu nimeona kumetengwa kiasi cha shilingi bilioni 159 kulipa malimbikizo kwa ajili ya watumishi mbalimbali ambao walishapanda vyeo na madaraja, lakini walikuwa hawajalipwa kile ambacho kinastahili kuwalipa. Kwa hiyo, naamini kwamba *morale* ya kazi itaendelea kupanda na kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wengine wanabeza uchumi haukui; ukiangalia takwimu za juzi za *World Bank* yule Mwakilishi Mkazi wa World Bank anasema kwamba; wao kama *World Bank* wali-*project* uchumi wetu utakua kwa asilimia 6.9 lakini umekuwa kwa asilimia 6.8, ni jambo ambalo la kujivunia, ni jambo ala kujipongeza. Hata makusanyo kutoka kukusanya wastani wa asilimia 11 sasa Serikali inakusanya wastani wa asilimia 12.8 na mafanikio haya ni ndani ya miaka miwili. Lengo ni kufikia mwaka 2020/2025 tufikie makusanyo ya asilimia 19 kama ambavyo nchi zingine wameweza kufanikiwa, ni mambo ya kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile uthubutu wa kuanza ujenzi wa reli tena kwa gharama nafuu. Tumeona wenzetu majirani, kilometa moja ni wastani wa dola milioni 8.5, sisi kilometa moja ni chini ya dola milioni 3.5. Ni jambo ambalo unaweza kuona kwamba Serikali iko makini katika kufaya majadiliano ya kufikia makubaliano ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukuaji wa bandari. Sasa hivi tunaona wale waliokuwa wamekimbia wameanza kurejesha imani. Kwa hiyo, ni matarajio kwamba ufanisi katika bandari yetu ambao umeanza kuongezeka utachochea utendaji wa kazi na hivyo kuongeza mapato kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, Tulipitisha hapa Sheria ya Madini, kulikuwa na malalmiko kwanini imekuja *under certificate of urgency,* lakini manufaa yake wote tunayaona. Kile kitakachopatikana maana yake ni kwamba kitakwenda kusaidia kuboresha aya, huduma za jamii kama elimu, ujenzi wa barabara na miundombinu mingineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma katika mpango na ninapongeza jitihada za ujenzi wa Kiwanda kule Mkulazi ambazo zinafanywa kwa ushirikiano wa Mifuko ya Jamii. Lakini nitoe ushauri, sisi mahitaji yetu kwa mwaka ni wastani wa tani 590,000. Katika hizi tani 300,000 ni matumizi *domestic* na tani 170,000 ni ile *sugar for industrial.*

Sasa pamoja na jitihada za uwekezaji huu ambazo zinaendelea, mimi nishauri kwamba tujaribu kuangalia katika yale mabonde muhimu tuwekeze pia kwa mfumo wa *small-medium size* kwamba unakuwa na kiwanda kinaweza kuzalisha tani 5,000 pale Kilombero, kiwanda kinakuwepo Rufiji hata vitatu au vinne, kwa sababu gharama zake za uwekezaji ukizi-*split* unaweza kuvutia wawekezaji wadogo wadogo wengi na hivyo kuongeza uzalishaji lakini pia kuongeza mapato kwa Seriakli pamoja na kupanua wigo wa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivi? Brazil wenzetu wanazalisha tani milioni thelathini na sita kwa mwaka na kwa takwimu hizo, Brazil *globaly* uzalishaji wao ni asilimia 20, lakini katika Soko la Dunia wao wanashika kwa asilimia 40.

Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba sukali bado inahitajika kwa kiwango kikubwa na sisi ili kuimarisha shilingi yetu maana yake ni lazima tuuze nje. Kwa hiyo, licha ya kwamba tuna soko la ndani, lakini pia tuna soko ambalo lipo, limejaa tele katika *global market.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ukienda katika takwimu inaonesha kwamba nchi kama Nigeria yenyewe inaagiza sukari ya thamani ya milioni 500

kwa mwaka, hilo ni soko lipo. Ukienda *South Africa* inaagiza sukari ya thamani ya dola milioni mia tatu na sita, maana yake ni soko lipo, ukienda Ethiopia wanagiza sukari ya dola milioni 188 kwa mwaka, maana yake ni soko lipo. Kwa hiyo pamoja na jitihada za Mkulazi tutafute pia mbinu nyingine ambayo inaweza ikachochea *small-medium size factories* ili tujitosheleze kama soko la ndani lakini pia tupeleke nje kusudi tuweze kuiimarisha shilingi yetu. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nizungumzie pia umuhimu wa kufufua viwanda hususani mradi wa kielelezo hasa wa Mchuchuma na Liganga. Mradi huu kila mara unakuja kwenye vitabu. Sisi watu wa Nyanda za juu Kusini tunadhani kwamba kufanikiwa na kuanza kutekelezwa kwa mradi huu utasaidia sana kuchochea uchumi katika eneo hilo na hivyo si tu kuongeza mapato ya Serikali lakini pia kupanua wigo wa ajira sambamba pia na kuimarisha shilingi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kufufua viwanda tuangalie pia jinsi ya kuwasaidia wawekezaji wa ndani. Kwa mfano mimi kule Mafinga, suala la mazao ya mistu ni jambo ambalo nimekuwa nikilisema mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali hasa Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Viwanda na Biashara, Maliasili na Utalii wanahusika kutupa sisi wawekezaji malighafi, lakini nimesema mara nyingi *MPM* kile wanachopewa wanavuna tu kama theluthi mbili. Sasa ile theluthi moja inayobaki wapewe wawekezaji wetu wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu; bei imeshuka sana. Sisi hapa mbao zetu hauwezi kushindana na mbao inayotoka Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hebu Serikali ijaribu kuangalia bei za misitu kusudi tuone namna gani tunaweza kuwapa wawekezaji wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa; kama nilivyosema wakati Maliasili wanahusika kutoa malighafi, Wizara ya Viwanda na Biashara moja kwa moja inahusika katika kulea hii sekta ya mzao ya misitu. Kuna *potential* kubwa kwenye mzao ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mwijage na Naibu wake, katika miaka mwili nimemwambia sana Mheshimiwa Mwijage uje Mafinga na Mufindi. *Minimum* mtu kawekeza shilingi milioni 500 na tuna viwanda siyo chini ya 40, kuna watu sasa wameanza kuongeza thamani katika mazao wakitengeneza mkaa kutokana na zile pumba zinazotokana na mazao ya misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ile kwanza itatusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Vilevile hawa watu kuna fursa nyingi wangependa kuzifahamu kutoka *TAB,* wangeweza kufahamu mambo mengi kutokana na tozo za *OSHA*, *NEMC*, *TBS* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote tukifanya kongamano la pamoja itatuwezesha sisi kujua ni changamoto gani wanazokabiliana nazo ili tui-*raise* hii sekta iweze kukua, ikuze ajira lakini pia iongeze pato; kwa sababu sasa wanaongeza thamani katika mazao tuuze nje ili tuendelee kuimarisha shilingi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naendelea tena kuiomba Serikali katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 tunaomba kwa ajili ya kuimarisha miundombinu katika Mji wa Mafinga bado hatujapokea fedha kutoka *Road Fund.* Tuna viporo vingi vya kuimarisha barabara ule ni mji unaokuwa kwa kasi tungependa tuwe japo na kilometa mbili, tatu za lami lakini kama hatutapata fedha itatuwia vigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali sambamba na kuomba fedha ambazo zinatakiwa ziende *TBA* kwa ajili ya mradi ule wa ujenzi wa *theatre,* pia ituangalie katika suala la barabara za pale Mjini Mafinga. Pia kwa ajili ya ujenzi wa tanki la mita milioni moja ambalo Mheshimiwa Waziri wa Maji namshukuru sana, ameniahidi kwamba kesho tutaonana naye ili kuweza kujua maendeleo ya kupata kibali cha kutangaza hiyo kazi yamefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, nakushukuru na niwaambie wananchi wa Mafinga nawapenda sana, ushirikiano wetu ndiyo silaha na moto wetu na *slogan* yetu tunasema Mafinga kazi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ghasia, atafuatiwa na Mheshimiwa Dokta Rashid na Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha afya njema na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili na mimi niweze kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumpongeza Waziri wa Mipango pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na Manaibu wake, kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya na pia ushirikiano ambao Kamati ya Bajeti wanaipatia. Napenda niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliahidi kujenga reli ya kati, sasa hivi tayari Mkandarasi wakujenga reli ya kati kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro yuko kazini na Mkandarasi wa kutoka Morogoro hadi Makutupora ameshapatikana, mkataba umesainiwa na kazi imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza tena Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi katika kuendeleza bandari zake. Nimeshiriki katika kuweka jiwe la msingi la upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na sasa hivi Mtwara inajengwa gati yenye urefu wa mita 300. Nina uhakika kabisa ndani ya miaka ya miwili bandari zote mbili upanuzi ukikamilika kwa kweli sekta yetu ya usafirishaji hasa kwa njia ya bahari itakuwa imeboreshwa sana na uchumi wetu utakua kwa sababu korosho zetu na bidhaa nyingine kutoka katika Mkoa wetu wa Mtwara kama saruji kutoka kiwanda cha Dangote itakuwa hakuna matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niipongeze pia Serikali yangu kwa hatua ambayo imefikia katika miradi ya kielelezo ikiwemo mradi wa Liganga na Mchuchuma, ambapo vile vivutio ambavyo wawekezaji walikuwa wanavitaka tayari wamepewa na kazi inaanza. Ninachotaka kuomba kwa Serikali yangu kwamba chuma kutoka Liganga makubaliano kipitie Bandari ya Mtwara, ili kiweze kupitia bandari ya Mtwara hatuwezi kusafirisha chuma kwa kutumia magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe ile reli ya kutoka Mtwara kwenda Liganga na Mchuchuma na Bamba Bay iharakishwe. Kwa sababu upembuzi yakinifu umekamilika, maeneo ambayo yatapita hiyo reli wananchi tayari wameshafanyiwa tathmini ya mali zao. Kwa hiyo, naomba ule mchakato mwingine uendelee ili pale ambapo uzalishaji kule utakuwa tayari na njia za kusafirishia ziwe pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Serikali yangu kwa kuweza kulifufua Shirika letu la Ndege, kwa kununua ndege ambazo wananchi wa Mtwara na hata wa Dodoma kwa sababu unaweza ukatoka Mtwara ukafika Dar es Salaam ukaunganisha kuja Dodoma, ukatoka Dodoma ukaenda Dar es Salaam ukafika Mtwara na ukaenda kupata *lunch* kule kwa watani zetu kule Songea. Kwa kweli naipongeza sana Serikali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kuiomba Serikali sasa hivi kwa kweli bei ya korosho ni nzuri sana na kule kwetu sasa hivi kila mtu ni furaha. Kwa vile wanaojishirikisha katika kilimo cha korosho ni wengi, manufaa yanayopatikana kipindi cha ununuzi wa korosho yanaenda kwa wananchi walio wengi. Sasa niiombe Serikali yangu tufike mahali tuache kuzisafirisha korosho zikiwa ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mpango wetu wa kupitia Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho ambao ulipanga kujenga viwanda vitatu vya kubangua korosho, nimeona juzi wameanza kule Tunduru. Kwa hiyo, naomba na maeneo mengine ambayo walipanga wafanye ili tupate manufaa ya bei ya korosho iendane pamoja na ajira za viwandani kutoka katika viwanda vya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza tena Serikali kwa kuanza mradi wa umeme wa *Stigler's Gorge,* kama tunavyofahamu tunajenga reli ambayo itatumia umeme lakini tumeanza uchumi wa viwanda vyote hivyo vitahitaji umeme mkubwa, hivyo uanzishaji wa mradi wa *Stiegler's Gorge* nadhani umekuja kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza tena kwa Serikali tunayo gesi nyingi inayozalishwa, tunaomba pia itumike pia katika kuboresha viwanda vyetu na pia katika kuhakikisha tunapata umeme wa kutosha. Katika Mkoa wetu wa Mtwara tumeahidiwa kujengewa megawati 300, tunaomba huo mradi uharakishwe kwa sababu sasa hivi Mtwara kuna changamoto kubwa sana ya umeme. Tumeahidiwa kuletewa megawati 20, lakini megawati 20 nina uhakika ndani ya miaka wiwili ijayo zitakuwa hazitoshi, kwa hiyo suluhisho la kudumu ni megawati 300. Kwa hiyo, tunaomba miradi hiyo yote iende sambamba kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za Shirika la Kuhudumia Watoto (*UNICEF)* zinaonesha ifikapo mwaka 2050 tutakuwa na watoto chini ya umri wa miaka 18 wafikao milioni 58. Watanzania kwa ujumla watakuwa milioni 108.

Je, tumejiandaa kuweza kuwasomesha watoto hao, kuweza kuwalisha watoto hao na kuweza kuwatibu watoto hao? Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha kwamba ongezeko la watu linaenda sambamba na ukuaji wetu wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kuna watu wanasimama wanaulizia pesa katika maeneo yao, lakini baadhi yao ni walewale ambao waliikataa bajeti iliyopita. Swali langu kwao, hizo pesa wanazoziulizia kwenda katka maeneo yao ni zile walizozikataa au kuna bajeti nyingine waliipitisha huko? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama una watoto wanne...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpatia Mheshimiwa Hawa Ghasia taarifa kwamba, Wabunge tunaongozwa kwa mujibu wa Kanuni Katiba na Sheria ya nchi. Tukipitia bajeti huwa tunaichambua, tunarekebisha mahali ambapo panahitaji kurekebisha na tunapoenda kupiga kura siyo lazima Wabunge wote waseme ndiyo. Kuna mambo tuliyaona hayastahiki kusema ndiyo na tukasema hapana, lakini mwisho kuomba maji kuomba kila kitu ni fedha ambazo ni fedha ambazo ni kodi za wananchi ni wajibu wa Serikali kuleta na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wapiga kura wake wamemsikia na ndicho alichokuwa anataka. Swali langu nililoliuliza hakulijibu. Nimeuliza bajeti ambayo wao wanataka iende katika maeneo yao, ni ile waliyoikataa au nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu katika Mabunge kuna njia tatu za...

**TAARIFA**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba pesa ambazo zinaleta maendeleo ni kodi za Watanzania ambazo kila mtu anatoa katika nchi hii, wala sio pesa ambazo tunatoka nazo nyumbani kwake mzungumzaji, kwa hiyo ajifunze kuzungumza...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu amepewa kazi yake, kuna waliopewa kazi ya kukusanya pesa na sisi tumepewa kazi ya kuidhinisha pesa. Kama wewe hujaidhinisha hizo pesa, unategemea zinafika kwao kwa mitindo gani? Wao hawakuidhinisha pesa na kama Waswahili wanavyosema asiyetwanga na asile, wao wamezikataa pesa, tupeni sisi tulioidhinisha pesa hiyo ndiyo taarifa ninayompa. Hata hivyo, nafurahi sana ukizungumza halafu wanawake kwa waume wakasimama kukupa taarifa maana yake taarifa yako imefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitisha bajeti unaweza ukakataa, unaweza ukakubali, unaweza ukasema huna maamuzi. Sasa kwa wao ambao walikikubali hiki wakakataa kile wangesema sina maamuzi, lakini wao wamekataa, ndio maana nikasema watafute maneno ya kwenda kuwaambia wapiga kura wao ni kwamba wao bajeti waliikataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja na naomba Waziri wa Fedha miradi yangu ambayo nimeiomba kwenye Jimbo langu nipelekewe pesa kwa sababu niliunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Dokta Rashidi Chuachua, ajiandae, Mheshimiwa Bura.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Serikali kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kutoa pongezi kwa Waziri pamoja na Mawaziri wote kwa sababu mpango ni shughuli shirikishi, wamefanya kazi kubwa katika kuandaa dira hii ambayo sasa tunaichangia ili tuweze kuiimarisha zaidi, iweze kutupeleka kule tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji na usimamizi wa miradi mikubwa ambayo inaendelea mpaka sasa. Mradi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge* ni kazi kubwa, kuimarisha pia Shirika letu la Ndege ni kazi kubwa, kuendelea kuisimamia na kuimarisha sekta ya madini nayo ni kazi kubwa inayohitaji pongezi kubwa sana kwa Serikali, kuimarisha sekta ya usafirishaji pia ni kazi kubwa sana kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, pia kusimamia nidhamu kazini na kuendeleza ujenzi wa viwanja mbalimbali vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti nianze kwa kusema tu kwamba tunaingia katika utaratibu wa utekelezaji wa bajeti wa mwaka 2017/2018 ambao tumeshauanza, lakini pia tunazungumzia mpango kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka unakuja. Lipo jambo ambalo tunapaswa pia tuliulize na Serikali iendelee kulifanyia kazi kutokana na utekelezaji hafifu wa bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma mpango katika ukurasa wa 20 inaonesha kwamba katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni asilimia 55 tu ya fedha ya miradi ya maendeleo zilizokwenda kwenye miradi yetu. Hii inaleta picha ifuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana tunapaswa kuongeza upya vyanzo vyetu vya mapato, lakini inawezekana pia kuna mahali ambapo tunazo sheria zinazotukwaza katika usimamizi wa fedha lakini tunahitaji kuongeza juhudi kubwa

katika kusimamia na kudhibiti matumizi na mapato ya Serikali. Naikumbusha Serikali kwamba katika bajeti ya 2016/2017 ilikuwa ime-*allocate* fedha katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Baadhi ya fedha bado hazijafika katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali iweke msisitizo mkubwa katika mpango huu kwa kuhakikisha kwanza tunakwenda kuimarisha au kutatua kero za wananchi kwa ile miradi ambayo inagusa huduma za jamii, hususani maji, umeme na afya. Haya ni mambo ambayo napenda Serikali yangu iyape kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuikumbusha Serikali kwamba bado ina kazi ya kuendelea kusambaza fedha za miradi ambayo iliahidiwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017. Katika mwaka 2016/2017 Halmashauri ya Mji wangu ilitengewa fedha shilingi milioni 599 kwa ajili ya uchimbaji wa mifereji na usambazaji wa maji ya bomba, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi tunavyozungumza fedha hizo hazijafika katika Halmashauri ya Mji wa Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inachelewaesha kuanza kwa mradi lakini inaongeza kero kwa wananchi kwa sababu tayari wameshachimba mifereji na sasa wanasubiri fedha. Nimezungumza na Waziri wa Maji amesema kwamba fedha hizo tayari ameshazi-*approve* kutoka Wizarani lakini zimekwama Hazina. Namwomba Mheshimiwa Mpango ahakikishe fedha hizi zinakwenda haraka kwa sababu mvua zikinyesha mifereji ambayo walichimba wananchi kwa njia ya kujitolea itaziba, hatimaye tutaanza tena kupigizana kelele na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na suala la maji kuna suala la umeme, kila Mbunge anayetoka Kanda ya Kusini lazima azungumze kuhusiana na suala la umeme. Tuna kero kubwa sana katika eneo hili tumezungumza mara nyingi na Waziri, tumezungumza mara nyingi na Watendaji wa *TANESCO*. Ukweli ni kwamba hali ya umeme katika Mikoa ya

Kusini ni mbaya sana na ubaya zaidi kwamba ni kipindi sasa cha takribani miaka miwili ahadi ambazo tumekuwa tukipewa ili kuondoa tatizo la umeme hazikamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Naibu Waziri amezungumza kwamba mwisho itakuwa mwezi wa Disemba tatizo la umeme litakuwa limekwisha. Tunaomba Waziri wa Fedha, tunaomba Waziri wa Nishati ahakikishe kwamba tatizo hili kweli linakwisha kwa sababu wananchi wanashindwa kufanya biashara, wananchi wanashindwa kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji kwa sababu tatizo la umeme ni kubwa sana. Kitu kikubwa kinachowaumiza wananchi wa Mikoa ya Kusini ni kwamba Kusini ni chanzo cha gesi ambayo pia inatumika huku katika miji mingine kwa ajili ya kusambazia umeme, kwa nini tuna shida kubwa kwa kiwango hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa napitia mpango, sioni mahali ambapo kuna mpango wa kuimarisha au kufufua viwanda vyetu vya korosho. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza, binafsi nimemwandikia barua Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na pia nimepeleka barua Wizarani kwake na kumkabidhi Katibu, tunaomba maelezo ya kina kwa nini Kiwanda cha Korosho cha Masasi hakifufuliwi? Nani kapewa kiwanda kile na mamlaka gani imemfanya akifanye kuwa ghala la kuhifadhia korosho badala ya kuleta mitambo na kubangua korosho. Tunaomba Serikali ihakikishe kwamba inalitatua na inalishughulikia kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niseme kidogo katika suala la kilimo, tunashukuru Serikali watu wa Kusini tukizungumzia kilimo tunazungumzia korosho, tunaishukuru sana Serikali kwa hatua iliyofikia, korosho inauzwa vizuri lakini zipo changamoto ambazo tungependa Serikali iziangalie. Kwa mfano, tumepata changamoto kubwa ya uhaba wa pembejeo katika mwaka wa fedha uliopita lakini ninaposoma mpango huu sioni mahali ambapo Mheshimiwa Mpango ameonesha usambazaji wa pembejeo aina ya *sulphur* utakavyokuwa kwa mwaka wa fedha wa

2018/2019. Tunaomba eneo hilo liingizwe ili tuweze kuona namna gani sasa Serikali inawasaidia wakulima wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo eneo lingine ambalo ningependa kuikumbusha Serikali, tunayo miradi ya barabara ambayo inaendelea na mengine inaendelea kwa taratibu mno, tunayo barabara yetu ya kutoka Nanganga kuelekea Nachingwea – Masasi, barabara hii hatuoni kazi inayofanyika kwa kweli, tungeomba Serikali iongeze juhudi na kutoa fedha za zakutosha barabara hii ikamilike ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara ya kutokea Mtwara inakwenda Tandahimba, inakwenda Newala, inakuja Masasi nayo hii hatuoni Serikali kama ina kasi kubwa ya kutaka kuimaliza tunajua kazi imeanza, tunaomba Serikali iongeze fedha za kutosha katika mwaka wa fedha ujao na mwaka wa fedha huu ili tuweze kukamilisha barabara hizi kwa ufanisi zaidi na kwa haraka ziweze kupitika tuwe tumetekeleza tuliyowaahidi wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wetu kuna eneo la kufunganisha maendeleo ya watu na shughuli za kiuchumi. Nataka niseme kidogo katika eneo la elimu, mwaka wa kwanza nilichangia na jambo hili nililisema halikuwepo katika mpango mpaka *last version,* mwaka wa pili nilichangia tena na mwaka wa tatu huu nachangia. Hakuna nchi inayoweza kuendelea duniani katika sekta ya elimu bila ya kufikiria namna ya kuendeleza sekta ya elimu isiyo rasmi, elimu nje ya mfumo rasmi. Jambo hili nalieleza mara nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matamko yanatolewa na viongozi wetu, kwa mfano mtoto akishapata mimba haruhusiwi tena kusoma, tunajiuliza mtoto yule anatakiwa aende wapi? Wapo watoto ambao wanashindwa kumaliza elimu ya Sekondari kwa sababu mbalimbali zikiwemo za utoro, umaskini uliotopea na mambo kadha wa kadha. Wapo ambao pia wameacha kusoma shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na wingi wa wanafunzi tulionao katika elimu rasmi watu ambao wanahitaji elimu walio nje ya mfumo wa elimu rasmi ni wengi zaidi. Nataka nikupe tu mfano mdogo, kwamba katika sensa ya watu iliyofanyika mwaka 2012 watu milioni 5.5 sawa na asilimia 22.4 ya Watanzania walionekana hawajui kusoma na kuandika. Ukisoma ripoti ya *UNESCO* ya mwaka 2014 inaonyesha kwamba tatizo hili linaendelea siku hadi siku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Daktari. Mheshimiwa Felister Bura, ajiandae Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama na kuchangia Mpango wa Maendeleo uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu wake Dkt. Ashatu Kijaji pamoja na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wameionesha kuhakikisha kwamba mpango huu unakuja mbele yetu nasi kama Wabunge tuchangie na kuongeza nyama pale ambapo tunaona panahitaji kuongezwa nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa uamuzi mgumu wa kuamua Serikali sasa ihamie Dodoma rasmi, watumishi wote wa Wizara zote zihamie Dodoma sasa, yeye mwenyewe, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwishahamia na tunawakaribisha wageni wote ambao mnakuja; Dodoma hakuna foleni, Dodoma ni salama, waje wafanye kazi ya ujenzi wa Taifa hili kwa umakini na kwa wepesi zaidi kwa sababu hakuna foleni katika Mji huu wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yanatakiwa na yanahitaji utekelezaji wa haraka katika suala

la kuhamia Dodoma. Mpaka sasa hakuna sheria inayotamka kwamba Dodoma ni Makao Makuu na nadhani kuna mambo yanaweza yakakwama kama hakuna sheria ambayo inatamka Dodoma ni Makao Makuu. Kwa hiyo, niiombe Serikali sasa Sheria iletwe Bungeni itakayotamka rasmi kwamba Dodoma ni Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali ya Awamu ya Tano, kabla ya kazi zote zilizokuwa zinafanywa na *CDA* kukabidhiwa Manispaa, *CDA* walikuwa na bajeti yao ya takribani shilingi bilioni 47 kwa ajili ya kuendeleza Mji huu wa Dodoma. Kwa sababu hatuna sheria inayoiruhusu Manispaa kutumia au kutoza tozo kwa ajili ya uendelezaji wa Makao Makuu ya Dodoma, Manispaa ina bilioni tisa tu za fedha za maendeleo. Zile bilioni 947 ambazo zilitengwa kwa ajili ya *CDA* kuendeleza Mji huu bado hazijapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu shughuli za uendelezaji wa Manispaa ya Dodoma ni kubwa sana na hatutaki kuingia kwenye matatizo ya msongamano wa magari kama Dar es Salaam na Arusha na Miji mingine, tunataka Mji wetu upangwe vizuri na mji wetu usiwe na *squatter,* Mji wetu uwe na barabara za kutoka na kuingia zisizoruhusu msongamano. Manispaa hawawezi kufanya kama hatuna fedha za maendeleo za kutosha kwa ajili ya kuendeleza Mji huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda tuwe na wataalam pia wenye uwezo ambao watasaidia kupanga Mji wa Dodoma. Tunataka Mji wa Dodoma uwe tofauti na Miji Mikuu ya Barani Afrika kwa sababu mji huu unajengwa kwa wakati muafaka na kwa fedha ambazo naamini kabisa kwamba tutazipata. Tunataka barabara za mabasi yaendayo kasi, tunataka malori yasiingie mjini, hatuwezi kufanikiwa kama hatuna bajeti. Tutafanikiwa tu pale ambapo tutakuwa na bajeti, lakini la muhimu tuwe na sheria inayotamka Dodoma kama Makao Makuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani *CDA* walikuwa wanatoza tozo ya asilimia 35 kwa ajili ya kuendeleza Mji.

Mamlaka ya Manispaa hawana huo uwezo. Tunaomba sasa tukumbukwe katika hilo ili Mji wa Dodoma upendeze kwa barabara, kwa mipango ya mitaa kuwa maeneo ya masoko, stendi na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema mengi pia niipongeze Serikali ya CCM kwa maamuzi makubwa ya kuangalia kwamba yale ambayo yalikuwa yamesimama sasa yanafanyiwa kazi. Sisi watu wa Dodoma tunashukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano, reli inakuja mpaka Dodoma, sio reli iliyokuwa *standard gauge* inayoishia Morogoro, wameshapatikana Wakandarasi na wanaendelea na upembuzi yakinifu na taarifa ya Waziri imeonesha kwamba hawa watu wamekwishapatikana, wanafanya upembuzi na mwisho wa siku tutakuwa na reli ya mwendokasi mpaka Dodoma. Kutoka Dodoma mpaka Dar es Salaam itakuwa aidha saa moja au masaa mawili na wananchi watafaidika na reli ambayo inajengwa sasa kwa *standard gauge.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaona kwamba ilikuwa kuja Dodoma lazima ukodi ndege yako, sasa hivi ndege ya Serikali inakuja Dodoma bila shida. Waheshimiwa Wabunge wengi nawaona mnapanda *Bombadier* bila kujali wewe ni wa Chama cha Mapinduzi au wewe ni wa Upinzani au wewe huna chama au wewe una chama. Kila Jumatatu asubuhi *Bombadier* ikitua hapo ina wananchi wengi wanaoshuka Dodoma, kwa hiyo, naishukuru sana Serikali ya CCM kwa kununua ndege na ndege sasa inawahudumia wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Spika na niwapongeze kwa kile walichokifanya. Mheshimiwa Spika, aliunda Kamati mbili zilizoshughulikia madini na ikatungwa sheria ya kushughulikia madini na sasa wizi tuliokuwa tunafanyiwa haupo tena, fedha zile ambazo tulikuwa tunaibiwa na wawekezaji hazitakuwepo tena! Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa haya mambo makubwa ambayo tumeona wamefanya kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuhusu suala la kilimo. Asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima lakini hawapati mbegu bora kwa wakati. Pembejeo za kilimo ni ghali mno na hata viwanda tunavyotaka kuanzisha tunaanzisha malighafi tutapata shambani. Niishauri Serikali yangu, pembejeo zipatikane kwa wakati kwa wakulima lakini zipatikane kwa bei nafuu anayoweza kumudu mkulima. Wakulima wetu baadhi bado wanakwenda kununua mahindi sokoni, wanakwenda kupanda mahindi waliyonunua sokoni. Wananunua mtama sokoni, wanakwenda kupanda mtama walionunua sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa wahakikishe kwamba pembejeo zinafika kwa wakati. Hata hivyo, bado hatujatilia mkazo suala la kilimo cha umwagiliaji. Kufuatana na tabia nchi kuharibika, sasa hivi mvua hazieleweki zitanyesha wakati gani, kwa hiyo ni vizuri pia tukakazania kilimo cha umwagiliaji, mabwawa yale ambayo yalichimbwa na mengine hayajafikia hatua za mwisho, basi Serikali ione namna ya kupeleka fedha. Sisi Dodoma tuna bwawa la Farkwa, lingetusaidia kwa kilimo cha umwagiliaji, lingetusaidia hata kwa masuala ya maji katika Wilaya zetu ambazo zinapakana na Mto Farkwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo, mifugo na uvuvi sijaona kama limetiliwa mkazo sana kuhusu suala la mifugo na uvuvi. Kuna ng'ombe wengi sana hapa nchini lakini hatuna viwanda vya nyama, hatuna viwanda vya ngozi, hatuna viwanda vya maziwa ya kutosha. Niiombe Serikali kama kuna uwezekano wa kuingia ubia na wananchi wawekezaji wakafungua viwanda vya nyama, migogoro ya wakulima na wafugaji itapungua, kwa sababu wafugaji watauza mifugo yao kwenye viwanda vya kuzalisha nyama, wakulima watakuwa na viwanda kwa ajili ya mazao yao. Pia suala la uvuvi tuna viwanda vichache sana vya samaki, Serikali iangalie suala hilo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami ili niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mezani. Pia nimshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii. Moja kwa moja naunga mkono hotuba ya Upinzani iliyowasilishwa kabla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa maendeleo huu utatekelezwa na Watumishi wa Umma, utatekelezwa na wananchi kwa ujumla. Ili Watumishi wa Umma waweze kutekeleza huu mpango wanahitaji kwanza kupata stahili zao zile wanazostahili, kama ni posho, kama ni mishahara, kama ni kupandishwa vyeo ili wawe na morali ya kuweza kufanya kazi kwa kujituma. Vilevile wanahitaji kupata *refresher courses* za kuwajengea uwezo wa kuweza kufanya kazi zao kwa utaalaam zaidi na hapa linakuja suala la mafunzo kwa ajili ya *in service* ambayo kwa muda mrefu yamesimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile watumishi wa umma wanahitaji kutiwa moyo wajue kwamba wanafanya kazi zao, wanaweza kufanya maamuzi bila kuogopa kutumbuliwa. Vinginevyo tutakuwa na utumishi wa umma wenye hofu ambao hauwezi kufanya kazi kwa kujituma na kwa ukamilifu kwa hofu ya kuchukuliwa hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile watumishi wa umma kama hawapati zile stahili zao kwa wakati tutarudi kule tulikokuwa zamani kwenda kufuga kuku – kukimbilia kufuga kuku, kukimbilia kuangalia ng'ombe kazi zinaachwa kufanyika ofisini. Kwa hiyo ni jambo muhimu sana kuangalia suala la Watumishi wa Umma ambao kwa kweli kwa muda sasa hawako vizuri na huo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengine ambao watatekeleza huu mpango ni wananchi wenyewe na wananchi wanahitaji amani, wanahitaji utulivu. Kuna hawa watu wasiojulikana ambao sasa hivi wamekuwa ni tishio

kwetu. Ni lazima Serikali iingilie kati kuwahakikishia wananchi wake usalama wao. Nilikuwa Mkuranga juzi na katika kikao nilikuwa na wananchi tunafanya kikao, wanaogopa hata hizi bodaboda saa 11 hawawezi tena kwenda kwenye maeneo yao wanayoishi kwa sababu ya hofu. Kwa hiyo, tunahitaji Serikali itoe kauli ya kuwahakikishia wananchi usalama wao ili waweze kufanya kazi zao vizuri, kwa sababu bila kuwa na uhakika na usalama hata shughuli za kiuchumi hazitafanyika kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo Serikali za Mitaa na *Local Government* inayo historia. Tulipopata uhuru tulikuwa na *Local Government* ambayo ilikuwa na nguvu sana, lakini Serikali ya wakati huo ikaona kwamba pengine ni ku-*centralize,* tuka-*centralize* Serikali, tukaua *Local Government* lakini hatukufanikiwa. Serikali ikarudisha tena *Local Government* kwa sababu Tanzania ni nchi kubwa sana, ina kilometa za mraba 945,000 ni kubwa sana haiwezekani ikatawaliwa kutoka Serikali kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo sasa matokeo ambayo yamekuwa yanaendelea kutokea sasa hivi inaelekea kuziua Serikali za Mitaa na kuzipunguzia nguvu za kuendesha shughuli, wakati tunajua wazi kabisa kwamba Serikali za Mitaa ndiyo kwenye huduma za afya, ndiyo kwenye barabara, ndiyo kwenye elimu na maji. Kama Serikali za Mitaa hazitapewa uwezo wa kutosha, uwezo kwa maana ya rasilimali watu na uwezo kwa namna ya rasilimali fedha, huu mpango ambao tunauleta hauwezi kufanikiwa kwa sababu utekelezaji uko kwenye Serikali za Mitaa na ndiyo kwenye wananchi. Ina maana basi huu mpango hautafanikiwa na maendeleo tunayotaka kuleta Tanzania ya viwanda haitaweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu kwanza mwaka huu ilipangwa bajeti kama *(approximately)* ya bilioni 12, lakini iliyotoka ilikuwa ni bilioni moja tu na *point* ambayo ni *about 11 percent.* Sasa kwa mtindo huu, sijui kama kweli huko tunakokwenda Serikali hii itafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwenye *Local Government* kama nilivyokwishasema awali na wengine pia wameshachangia, tumenyang'anya *Local Government property tax,* tumewanyang'anya ushuru wa mabango, ruzuku haiji kwa wakati sasa hiyo *Local Government* ambayo tunataka ifanye kazi itafanyaje kazi kama haipati *resources?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba *Local Government* inafanya kazi kwa niaba ya Serikali kwa sababu Serikali kuu imekasimu madaraka kwa *Local Government.* Kwa hiyo kama Serikali ya Mitaa inafanya kazi, inafanya kazi kwa niaba ya Serikali, kama Serikali ya Mitaa ikishindwa ina maana Serikali Kuu na yenyewe imeshindwa. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuimarisha Serikali za Mitaa ziweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kwenye rasilimali watu tunahitaji kwa ajili ya huu mpango kufanikiwa. Katika mpango ule wa mwaka 2016/2017 - 2020/2026 wa mwaka jana ambao uliwasilishwa kulikuwa na taaluma ambazo ziliainishwa, kulikuwa na Wahandisi, watu wa *construction,* watu wa *agriculture* na yalitolewa malengo. Kwa mfano, katika *agriculture* na zingine lengo lilikuwa ikifika mwaka 2025 wataalam 145,000 wanategemewa kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika mpango wa sasa hivi kuna maeneo kwenye *training* kuna taaluma mbalimbali ambazo watu wanakwenda kusomeshwa. Swali langu ni kwamba tumeweka *target* hiyo ya 2025 na *intervention* 2015/2016 kwa mfano kwenye *agriculture* tulitegemea tuwe na wataalam 4,475, sasa napenda kujua, tukifananisha lengo lile la 2025 na tulivyoanza 2015/2016 kwa kuainisha kada zile ambazo zinatakiwa kufikiwa, je, tumekwenda vipi mpaka sasa hivi huu mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia Wabunge tuweze kufuatilia utendaji kazi wa Serikali katika kufikia yale malengo ambayo yameainishwa. Kwa hiyo, nitapenda sana kujua Serikali imefikia wapi katika kuainisha hayo malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kila siku kilimo ni uti wa mgongo na sio uti wa mgongo tu, kilimo ndiyo kitatoa malighafi kwa ajili ya uchumi wa viwanda. Nimeangalia katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri, ameainisha tu *activities* ambazo zinatakiwa kufanywa kwa ajili ya kilimo lakini sijaona mahali popote ambapo ameainisha kwa mfano, watalaam wa kilimo hasa Maafisa Ugani ambao ndiyo wanaokwenda kuwasaidia wakulima katika uzalishaji, sijaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hata katika sikumbuki ukurasa wa hii ripoti ya sasa hivi ambapo imeainishwa taaluma mbalimbali nimeona watu wa *VETA*, sijui watu wa mambo ya hoteli, sijaona popote wameainishwa Maafisa Ugani ambao ni muhimu sana kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kuweza kulima vizuri na kwa kitaalam waweze kupata mazao ya kutosha. Kwa hiyo, ningependa kujua ni kwa namna gani Maafisa Ugani watapanga ili tuweze kupata Maafisa Ugani wa kuweza kwenda kusaidia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishauri Serikali tuwe na Maafisa Ugani wa kutosha kama ambavyo tulivyo na Madaktari kwa *ratio* tunasema kila Daktari mmoja anatakiwa kutibu wagonjwa 10,000. Tuwe na *ratio* pia kwa ajili ya Maafisa Ugani kwa ajili ya wakulima kusudi Afisa Ugani aweze kuwafahamu wakulima wake kwa umakini na shida zao, wawezeshwe kwa kupewa hata pikipiki waweze kuwafikia wakulima, ndiyo tutaweza kuleta kweli mapinduzi ya kilimo katika nchi hii. Bila hivyo itakuwa ni kuzungumza hapa kila siku, tutaondoka, mambo yatabaki hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la mikopo ya wanafunzi. Kama tunavyojua sasa hivi wanafunzi wengi hawajapata mikopo. Naishauri Serikali iangalie tena upya hii Sera na utekelezaji wa mikopo. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu, kwanza na-*declare interest* kwamba mimi ni mmojawapo walioanzisha Bodi ya Mikopo, sababu ilikuwa ni kuwasaidia wanafunzi wenye uhitaji....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuru. Muda wetu umekwisha. Jioni tutakuwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, tutakuwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Ally King, Mheshimiwa Hongoli na tutakapopata majina mengine tutawatangazia.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali, pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

### KAMATI YA MIPANGO

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, mchana nilitoa majina ya watakaotuvusha jioni hii, tukianza na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae. Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Mpango wa Maendeleo ulioko mbele yetu wa mwaka 2018/2019. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima nikaweza kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwenye mpango wa Waziri ameweka vipaumbele vichache. Nami naomba nijaribu kuangalia vile vipaumbele kwa namna ambavyo vinaweza kuboreshwa zaidi. Kwanza naanza na hii ya kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu na hasa nikianza na suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio yetu Wabunge na ni matarajio ya Watanzania kwamba, angalau mpango wa bajeti ujao uweze kwenda kuondoa kilio cha maji cha muda mrefu, kwa sababu kilio kimekuwa ni cha kila mahali. Kila Mbunge ndani ya Bunge hili Tukufu ana kilio cha maji na kiukweli maji ni uhai, maji ni uzima. Tunapokwenda kugusa suala ambalo tunagusa uhai wa Watanzania tusitegemee tunaambiwa kwamba, tunasubiri kupata wafadhili au tunaomba wafadhili, tutenge fedha ya ndani kwenda kukamilisha miradi ya maji ambayo imeanzwa ili tuweze kupata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango ujao nategemea kabisa miradi mikubwa ile ambayo ilikuwa kwenye bajeti inafanyiwa upembuzi yakinifu na mambo mengine inakwenda kuwekewa fedha ya kutekelezwa ikiwepo mradi wa maji kutoka Malagarasi Mkoani Tabora kupeleka Wilaya ya Kaliua na Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye bajeti ijayo kuwepo na fedha ya kutosha kuhakikisha kwamba, mradi huu unakamilika kwa sababu, Serikali inajua kwamba, ndani ya Mkoa wa Tabora ardhi haina visima vya maji kwa hiyo, njia pekee ni Mradi huu wa Maji wa Malagarasi na Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kuweza kupeleka katika Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la usimamizi wa rasilimali ya misitu. Katika kipindi ambacho misitu yetu inateketea ni kipindi hiki. Nilitegemea kabisa kwamba, baada ya kuanzishwa kwa Wakala wa Misitu angalau lengo la Wakala wa Misitu, ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, misitu inalindwa, inahifadhiwa, lakini inatunzwa kwa njia ambayo ni endelevu na matumizi endelevu. Sasa hivi tofauti na hapo Maafisa wa Misitu kwa maeneo mbalimbali kazi wanayofanya ni kugonga mihuri kwenye magogo, kwenye mbao, magogo yanaondoka tunabakiwa na vichaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye mpango ujao namna gani Serikali itahakikisha kwamba, inaweka mpango endelevu wa kulinda na kutunza misitu yetu, tunaenda kuwa jangwa. Leo tunapata madhara mengi sana ndani ya nchi yetu kutokana na mabadiliko ya tabianchi, hatujui chanzo ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchomaji wa mkaa umezidi na bahati mbaya sana leo Serikali imeweka mabango sehemu maeneo mbalimbali kuhalalisha mauzo ya mazao ya misitu wakati uvunaji wa misitu na utunzaji, kupanda miti ni tofauti. Tunapanda kidogo sana, hatutunzi, haikui, tunavuna kwa *speed* ya 100 *percent,* tuendako tunaenda kuwa jangwa. Naiomba sana Serikali tuhakikishe tunaweka mpango endelevu wa kutunza na kuhifadhi misitu yetu kwa sababu hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia chanzo kikubwa cha uharibifu wa misitu ni ukataji wa mkaa na hatujawa na mpango mbadala wa matumizi ya nishati, tunasema kila siku. Nimeona kwenye Mpango wa Serikali kwamba, tunakwenda kuwekwa kiwanda cha makaa ya mawe ya Mchuchuma. Ni miaka 15 tunasikia makaa ya Mchuchuma – makaa ya Mchuchuma, kwa nini hautekelezwi, miaka 15?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine ingekuwa ni *solution* kuhakikisha kwamba, watu wanapata nishati ya kutumia kwa sababu, umeme huwezi kupikia, gesi wanatumia

wachache, mafuta ya taa hayashikiki, ni kuni na mkaa. Asilimia 80 ya Watanzania wanatumia kuni na mkaa, hebu Serikali mwakani itujie na mpango namna gani Watanzania wanatumia nishati tofauti na mkaa, ili kulinda misitu yetu, tunakwenda kuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la umeme. Nashukuru kwamba, umeme wa *REA* umeanza kusambaa maeneo mbalimbali, lakini ule umeme sasa hivi umekuwa ni 'kimulimuli' kwa sababu, ikinyesha mvua umeme hamna kwa sababu, *speed* yake ni ndogo na nguvu yake ni ndogo. Tunaiomba Serikali kwenye mpango wa maendeleo ujao uje na mpango mkakati wa kujenga *sub-stations* maeneo mbalimbali kwa ajili ya kupokelea umeme na kusambazwa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Kaliua pamoja na kuwa walipata faraja wamepata umeme, lakini mvua ikinyesha unakatika, jua likiwa jingi unakatika kwa hiyo, hauna tija. Tunasema tunazungumzia uchumi wa viwanda, hatuwezi kuwa na uchumi wa viwanda kama umeme siyo wa uhakika. Kwa hiyo, naiomba Serikali ikiwepo kujenga kituo cha *sub-station* pale Kaliua pamoja na Urambo, mpango ambao umekuwepo tangu mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwenye mpango ujao ukatekelezwe huu umeme wa *REA* ambao tunaendelea kuupata uweze kuwa na tija kuendesha viwanda vidogovidogo, lakini pia kuweza kusaidia wananchi kuweza kuutumia, usije ukawa ni kama mapambo, kama ambavyo sasa hivi unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Vitambulisho vya Taifa. Mpango huu umeanza tangu mwaka 2019, mpaka leo ni miaka tisa *speed* yake ni taratibu sana. Tunajua umuhimu wa Vitambusho vya Taifa. Kwanza ni uraia wa Mtanzania, lakini pili tunaweza kutumia kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali. Leo ndani ya Taifa letu kuna watu wanaingia kinyemela kwenye mipaka wanaishi Tanzania kwa amani, kwa furaha, sio raia wa Tanzania. Hiyo

ipo kabisa, ni nchi pekee ambayo unaweza kukuta kitu kama hiki. Kwa nini *speed* ya vitambulisho vya Taifa inaenda taratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitenga fedha nyingi sana zaidi ya milioni 200 kipindi kile, lakini mpaka leo *speed* ni taratibu sana. Bahati mbaya sana sasa hivi wananchi wanadaiwa fedha, ili uweze kuandikishwa utoe sh.5,000/=, sasa hivi mtu ananunua hata uraia wake kwa kweli, *is nonsense.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali, kwanza suala la kuwalipisha wananchi kujaza fomu kwa ajili ya Vitambulisho vya Taifa liondoke, lakini pia mchakato huu ufike mwisho. Tuambiwe kabisa kwamba, idadi ya Watanzania wangapi mpaka leo wamepata vitambulisho vya Taifa, ni haki yao na siyo ombi. Tunaomba litekelezwe tuache kwenda *speed* ya taratibu kiasi hiki kwa suala la umuhimu kama kupata Vitambulisho vya Utaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la uanzishwaji wa Bandari ya Samaki. Tumekuwa tunaongea na kwenye mpango wa Waziri haipo. Tumekuwa tunasema njia tunayopoteza mapato mengi sana ni njia ya bahari kuu, uvuvi wa bahari kuu *almost* ni shamba la bibi, wanakuja wanavuna wanaondoka; hatujui wamevuna wangapi, mafuta wanajaza hukohuko, tumekuwa ni rasilimali ambayo hatuilishi iko pale ni kuiuza, kuisimamia na kupata fedha, tumeshindwa Serikali. Tunaiomba kwenye bajeti ijayo Serikali ije na Mpango wa Kujenga Bandari ya Samaki tuweze kuhakikisha bahari kuu samaki wale wananufaisha Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache kuwa wazembe kiasi hiki. Ni miaka mingi, lakini kila mpango ukija haipo. Kwa hiyo, ni matarajio yangu kwamba, mwakani kwenye mpango huu unaokuja Waziri atatujia na mpango mkakati, mpango maalum kuhakikisha kwamba, tunakuwa na Bandari ya Samaki tuweze kuongeza Pato la Taifa, lakini pia tunufaike na rasilimali ambayo wenzetu wananufaika nayo wanakwenda kutajirika, sisi tunaendelea kuwa ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo. Ni kweli kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu, lakini kilimo chetu hakiendani na neno lenyewe uti wa mgongo. Kwanza kilimo cha Tanzania bado ni kilimo ambacho kinatumia jembe la mkono kwa kiasi kikubwa, lakini ni kilimo ambacho hata mazao yanayopatikana hayana masoko. Leo imekuwa ni kilio sasa mwananchi ananunua pembejeo mwenyewe, ananunua kila kitu mwenyewe, hata masoko ya mazao hakuna. Imekuwa ni maumivu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ndani ya Mkoa wa Tabora *particularly* Wilaya ya Kaliua na maeneo mengine watu wanalia machozi, wamelima kwa jasho, wamevuna, leo tumbaku iko kwenye ma-*godown* haina soko, inaharibika, inashushwa thamani. Leo Serikali inasema habari ya kilimo, utasema nini kwa habari ya kilimo?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tuwe na mbinu na mikakati ya kuandaa masoko ya kilimo mapema kwa sababu, tunakwenda kwa takwimu ni lazima tujue tuna wakulima idadi gani, watazalisha kitu gani, tuwe tumejipanga kupata masoko ya uhakika kupitia kilimo cha mbaazi, kilimo cha mahindi, ni kilio kwa sababu tunahamasisha kilimo, lakini tuwe na mikakati ya masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni lazima tuhakikishe kwamba, kilimo cha Watanzania kinakuwa ni kilimo ambacho kinatumia *mechanization* siyo kilimo cha jembe la mkono ambacho ni cha muda mrefu na pembejeo zipatikane kwa wakati ili watu walime kwa tija na waweze kunufaika na kilimo ambacho asilimia zaidi ya asilimia 75 kubwa ya Watanzania inategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ujao ni lazima kila zao la biashara tuwe tumeambiwa kwamba, masoko yako wapi ya uhakika. Sasa hivi naiomba Serikali sana tatizo la tumbaku ambalo liko sasa hivi Serikali ihakikishe namna yoyote kuhakikisha tumbaku ile inapata masoko, pia itafute madawa ipeleke kwa ajili ya kwenda kuitunza isiendelee

kuharibika na ikiwezekana Serikali iinunue iitunze kwenye ma-*godown* yake wananchi wapewe fedha waendelee na maisha yao. Leo watoto wao hawaendi shule, leo wameshindwa hata kumudu vyakula, lakini tumbaku iko ndani na ni zao ambalo walihamasishwa walime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana majibu anayotoa Waziri wa Kilimo yanasikitisha sana kwamba, watu walilima bila kuwa na makisio na anajua ni kwa nini watu walilima bila makisio. Sio majibu ya Waziri ya kutoa. Kwa hiyo, tunaomba aje na majibu mazuri, Serikali ije na majibu mazuri ni kwa nini tumbaku ya wakulima Tabora na mikoa mingine hainunuliwi wakati walihamasishwa kulima na wamelima kwa nguvu zao peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la utafiti. Huwezi kuwa na nchi ya maendeleo endelevu, ukawa na kilimo endelevu, ukawa na viwanda, ukawa na elimu nzuri bila kuwa na utafiti. Tumekuwa wazembe kama Taifa kuwekeza kwenye utafiti. Tunaomba bajeti ijayo tuhakikishe tunawekeza vizuri kwenye utafiti, vyuo vyetu vya utafiti nchi nzima viko hoi, miundombinu imeharibika, tunao wataalam wako pale wana elimu nzuri, hatuwatumii kwa sababu, hatuwekezi kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima kama Taifa tuwekeze kwenye utafiti tuweze kufanya kila kitu kwa kutumia utafiti, watu walime kwa utafiti, watu wauze kwa utafiti, watu wasome kwa kufanya utafiti. Suala la mwisho katika utafiti, vituo vyote vya utafiti vikarabatiwe pia, kuwepo na nyenzo na vitendeakazi elimu ambazo ziko pale na wataalam wale waweze kutumika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la mikopo kwa elimu ya juu. Kiukweli kuna matatizo makubwa na wananchi wa Tanzania, wonyonge, maskini, wanalia sana. Nilifikiria kwamba, Serikali iliposema kwamba, kila mtoto anayekidhi vigezo atakwenda kupata mkopo, ni kweli ingekuwa hivyo, lakini leo wako wengi wamekidhi vigezo, lakini wamekosa mikopo. Unaposema unawapa watoto elfu

30 wakati umeacha elfu 37, *majority* wamerudi mitaani wanakwenda kufanya nini, hakuna mitaji ya biashara, wameshamaliza kusoma *Form Six,* kilimo hakilipi, wakilima biashara hamna, wakilima masoko hamna. Kiukweli hawa asilimia zaidi ya 30,000 ni wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali ifanye utafiti wa kutosha kila mwaka ihakikishe kwamba, mwaka ujao wana-*pass* wanamaliza vyuo wanafunzi wangapi, *form six* na wataingia wangapi, ili ijipange kuendana na idadi ya watu ambao wanakidhi vigezo vya kuweza kupata mikopo. Vinginevyo itaendelea kuwa ni vurugu kwa sababu, kila mwaka watoto wetu wanaandamana, wanapigwa kwa sababu, ni haki yao wanadai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa kuwa watoto wanatamani kusoma na kitu pekee ambacho mzazi au Taifa unaweza kumpa mtoto wako ni elimu, vingine vyote ni bure, ukishindwa kumpa elimu ni basi. Kwa hiyo, pale ambapo watoto wetu wanamaliza shule wana matarajio ya kupewa elimu, basi Serikali ijipange vizuri iweze kutoa mikopo, ili kila mtoto mwenye kigezo cha kuweza kupata elimu apate elimu kwa ajili ya maisha yake ya hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, hayupo. Mheshimiwa Mtuka, Mheshimiwa Deo Ngalawa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mtuka yupo.

Sawa, Mheshimiwa Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mpango huu. Kwanza nitangulize tu kutoa shukrani zangu kwa Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Magufuli, amefanya mambo makubwa na kila mtu anaona. Kwa mfano, kwangu kule Manyoni hatukuwa na

miradi ya maji, lakini sasa tuna miradi ya maji, fedha imeanza kutoka tunashukuru sana angalau mradi hata mkubwa wa wastani mmoja unaendelea. Sina budi kutoa shukrani zangu kwa niaba ya wananchi wa Manyoni Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nizungumzie jambo fupi tu. Tulikabidhiwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, lakini pia hata wenzetu wanatumia Ilani hiyo. Katika Ilani hiyo nimeigawa katika makundi makubwa mawili ya kusimamia. Eneo la kwanza ni la huduma za jamii, tunapozungumzia maji, afya, elimu, miundombinu, hizo ni huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti,eo nizungumzie suala la kuboresha uchumi kwa wananchi wetu, wamepata maji sawa, natoa mfano, lakini uchumi wao ukoje? Vile vikundi vyetu vya ujasiriamali vikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na maoni ya Kamati katika ukurasa ule wa tano, kipengele cha pili kinasema, "Kuzingatia maeneo yanayogusa wananchi walio wengi kwa ajili ya kukuza kipato na kupunguza umaskini, hususan kilimo, uvuvi, upatikanaji wa pembejeo na mitaji." Mimi nijikite kwenye eneo la kilimo. Manyoni kwa mfano, Mbunge pamoja na Madiwani wenzangu tunalala na kusugua vichwa ni namna gani tupate kuwawezesha wananchi wetu kupata ajira, tufanye nini, lakini tumekuja na tunayo mambo matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza; hivi ninavyozungumza Manyoni Mashariki eneo linaloitwa Masigati tumetenga ekari 3,200 kwa ajili ya kuanza ukulima wa korosho baada ya wataalam kutoka Naliendele kupima ule udongo na kutuambia mkilima korosho hapa mtapata korosho nyingi na bora kuliko zile za Lindi na Mtwara. Tumeshatenga ekari 3,000 hivi ninavyozungumza tunachangishana fedha kwa ajili ya kupata *grader* la kufyeka ule msitu, ili tuanze kupanda korosho na miche imeshaanza kuoteshwa kwenye vitalu, ekari 3,000. Tumeshachanga fedha

shilingi milioni 36 mpaka sasa hivi kwa ajili ya mafuta, ila hatujui *grader* tulipate wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa bajeti hii inayokuja tukitenga fedha kidogo angalau kuwaunga mkono wananchi, Serikali tunaomba ipitishe ile bajeti ya watu wa Manyoni kwenye eneo hili la kilimo, ili tuweze kuajiri watu wengi zaidi pale Manyoni. Kama kiongozi, lazima tulale na kuota namna gani tutaweza kuongeza ajira kwa watu wetu. Manyoni tumeanza na tunaendelea, tunaomba Serikali ituunge mkono kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu huu sasa tungefurahi kusikia Serikali inasema angalau kuna kafedha ka dharura au kuna *grader* ambalo lipo mahali fulani kwenye Wizara labda ya Ujenzi, fedha tumeshakusanya ya mafuta, wakatusaidie kufyeka ule msitu tupande korosho, tutaajiri watu wengi sana kwenye eneo hilo, zaidi ya watu 3,000 watapata ajira Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine hapo Manyoni kuna Kijiji kinaitwa Solya, ni katika kupambana tu kutafutia watu ajira, kuna eneo tumelitenga ni la mfano tunataka tuanze shamba darasa, tuna heka 10 pale. Tumeshachimba mabwawa ya urefu wa mita 10 kwa 20 yapo nane ya samaki. Pia tuna heka mbili tumeshaanza ni shamba darasa kwa ajili ya bustani, tunataka vijana wote ambao hawana ajira kwenye eneo lile waanze kupata ajira. Shamba darasa lile litasaidia sana kwa vijana wa Manyoni na maeneo mengine yote watakuwa wanajifunza pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo, maji yale ni ya kuchimba chini, tumechimba kisima kwenye shamba darasa pale na umeme tumevuta kwa nguvu zetu wenyewe. Hata hivyo, lakini kuna eneo ambalo tumelitenga ni kubwa pia la hekari 20, tunahitaji visima vitatu na wameshapima visima maji yapo lakini hatuna uwezo wa kuchimba vile visima. Kikubwa miundombinu ya umeme kwa sababu lile eneo ni nje kidogo ya kijiji. Tungeomba Serikali ituunge mkono, itusaidie zile nguzo zitoke pale, ni kama kilometa moja na

nusu hivi zitoke kwenye sehemu ya umeme watupelekee umeme kwenye eneo hilo la shamba. Tunaomba sana Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni mbinu ambazo Kiongozi yeyote ambaye anaweza kuona mbele, lazima afikirie kuongeza ajira na kutafuta ajira kwa watu wake na hasa vijana, akinamama na watu wote. Manyoni viongozi tunakosa usingizi kwa ajili ya kuongeza ajira, kumsaidia Mheshimiwa Rais anahangaika sana, Serikali mtuunge mkono, Manyoni tumeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo eneo pia la machimbo ya chumvi, eneo linaitwa Kijiji cha Kinangali, tunayo chumvi nyingi sana, tunaomba sana msaada kwenye mambo ya kitaalam namna ya kuchakata ile chumvi, tunatumia mbinu za kizamani, tunakata miti sasa tunaharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali mtusaidie utalaam, tumejaribu sana lakini tunaomba sana Serikali hasa sehemu ya Wizara inayohusika na mambo ya ajira na vijana, hebu watusaidie wataalam ile chumvi inavyochakatwa hasa kwa njia za kitaalam, tunayo chumvi nyingi sana. Tutasaidia ajira vijana wengi sana na akinamama kwenye lile eneo. Manyoni sisi tumeanza, tunaomba Serikali ituunge mkono kwenye maeneo haya ambayo nimeyataja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikihama kwenye eneo hilo la kuongeza ajira kwa watu wetu, labda la mwisho tu. Jamani ndugu zangu haiwezekani katika nchi hii kila mahali ikawa ni sehemu ya kuishi, msitu mnene unakuta umefunga, mtu anatoka atokako anakaa katikati ya msitu. Kule Manyoni wanatuvamia watu wahamiaji, anakaa katikati ya msitu, miti minene ile imekua kwa miaka mingi, karne na karne mizuri katikati ya msitu anaanza kufyeka anajenga, anafyeka shamba na sehemu ya kulishia mifugo. Haiwezekani kila mahali pakawa pa kujenga tu, lazima tutunze mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia ule mpango wa matumizi ya ardhi ambao tumeusema tangu mwaka juzi, mpango huu unachelewa mno. Naomba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mtusaidie kuharakisha huu mpango jamani, wakulima na wafugaji wapate maeneo yao, sehemu ya kujenga na viwanda pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuipime Tanzania, tuhifadhi mazingira jamani, ni sawa na mtu ambaye amepanda juu ya mti, amekalia tawi anafyeka kwenye shina kule, likidondoka lile tawi anatangulia yeye chini. Hawezi mtu kukaa katikati ya msitu anaanza kufyeka eti natafuta shamba ama anatafuta sehemu ya kujenga, haiwezekani. Anaacha vijiji vingi tu anaruka anakuja kujenga katikati ya msitu, haiwezekani! Tuipime Tanzania katika mpango huu wa matumizi bora ya ardhi, tuiokoe nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema hata mwaka jana nilisema hivi kwa mfano, hata hii migogoro ya mkulima na mfugaji tulisema tupime, sijui mpango umeishia wapi? Kwamba tupime, kuna maeneo mengi tu tunawanyanyasa wafugaji bure, kuna maeneo mengi ambayo tukijipanga vizuri tukayapima kila mmoja atakaa sehemu na mifugo yake kwa raha mustarehe wala haina shida, eneo tunalo kubwa tunakosa mpango tu. Ni mpango tu ndugu zangu tunaokosa ndio maana tunagombana, haiwezekani mfugaji au mkulima anakuja anachukua heka 1,000, wengine wanapata wapi? Ni lazima kila mmoja apate eneo ambalo atakaa nalo kwa kudumu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo hifadhi za misitu au za wanyama ambazo zimekuwa *redundant* ambazo zimekosa sifa, zile tungezipima tukazigawa hata kwa wakulima na wafugaji. Tunazo ranchi zetu ambazo zimekuwa *redundant* tuzipime tuweke miundombinu, malambo, mabwawa na wataalam wa mifugo ili watu wafuge kule. Jenga hata viwanda vya kuchakata/kusindika nyama kule; tunayo maeneo makubwa tunakosa mpango tu, utaratibu mzuri wa kupima, tuipime Tanzania jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mafupi, mimi sina cha zaidi, naunga mkono mpango huu, tuyazingatie haya mawili niliyoyazungumza, tulale na kufikiria kuwatafutia watu wetu ajira. Serikali ituunge mkono lakini tukaipime Tanzania kila mmoja apate mahali pa kufanyia kazi bila kugombana, kuharibu mazingira wala vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Deo Ngalawa, ajiandae Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kutoa shukrani zangu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais John Pombe Magufuli kwa mambo yafuatayo ambayo yanafanyika sasa hivi kule Ludewa. Kuna barabara ya lami kutoka Njombe kwenda Ludewa - Manda, umeme wa Gridi ya Taifa ambao unatoka Makambako kwenda Songea unakatisha pale Madaba unakuja Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna miundombinu wezeshi ambayo inaweza ikaifanya chuma Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma kuanza kwa maana ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara za Madaba kwenda Mkiu na barabara kutoka Nkomang'ombe kuelekea Liganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo kuna baadhi ya mambo ambayo napenda kuyaelezea kidogo hasa kuhusu makaa ya mawe Mchuchuma na chuma cha Liganga. Chuma Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma ni miradi kielelezo katika Serikali hii ya Awamu ya Tano lakini bado hatujaona mpango ambao unaweza

ukaonesha kwamba chuma Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma yanaanza lini. Kwa sababu hii *project, project* inatakiwa iwe na mwanzo pia iwe na mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado haijaweka ule utaratibu mzuri wa kusema kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano, mwaka huu tunafanya kitu hiki, mwaka wa pili hiki, mwaka wa tatu mpaka ule wa tano. Kwa hiyo, *statement* ambayo inakuja ni *statement* ya jumla sana kiasi ambacho sasa hata ku-*access* huu mpango ambao ni mradi kielelezo cha Taifa inakuwa ni mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa Serikali sasa ianishe kwamba kwamba kwa sababu huu leo ni mwaka wa pili unakwisha tunaelekea kwenye mwaka wa tatu, bado hatujaona zile *activities* ambazo zinatakiwa zifanyike katika huu mradi husika. Tukiweka na kuainisha maana yake tutakuwa tumeweka vizuri kiasi ambacho unaweza sasa kufanya tathmini kwamba mwaka huu tunafanya hiki, mwaka wa pili tunafanya hiki na hata kama tunakwama sehemu tunakuwa tunajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye hilo ningependa tu Serikali ije na ile mipango kwa sababu kuna eneo pale ambalo wananchi wetu wamepisha mpaka leo bado hawajalipwa fidia na wala hatujui fidia ile italipwa lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huu mpango ambao tumesema kuna *Power Purchase Agreement,* ni kweli tunapata maelezo lakini hatujui kwamba sasa hiyo *Power Purchase Agreement* itakamilika lini kiasi ambacho sasa itapelekea ile *Government Notice* kutoka. Naamini kwamba hii yote ipo ndani ya uwezo wa Serikali, Serikali ikijipanga haya mambo yanaweza yakaisha na mwisho wa siku hata hawa watu ambao wamepisha ile miradi kwa sababu yale maeneo waliyoyapisha ni makubwa kiasi ambacho sasa wanashindwa kufanya kitu chochote na hawajui kwamba fidia yao watalipwa lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulichangia ni juu ya suala la zao la mahindi. Nyanda za Juu Kusini ambako Ludewa ipo, zao la mahindi ni zao la biashara. Kwa wengine wanaweza wakasema kwamba ni zao la chakula, lakini hakuna zao kubwa na muhimu ambalo linatiliwa nguvu kubwa na wananchi wetu kama zao la mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba tunapolima mahindi yanapotosheleza kwa chakula, mengine yanayosalia ndiyo ambayo yanaenda kwenye biashara ambazo zinawafanya watu wetu walipe ada, wajenge nyumba na wafanye maendeleo yao mengine. Kipindi cha sasa wananchi wetu wame-*stuck* na walikuwa wanaitegemea Serikali kwa kiasi kikubwa kununua yale mahindi, sasa hivi mahindi hayanunuliwi na mwisho wa siku sasa inabaki kwamba uchumi wa wananchi mmoja mmoja na uchumi wa maeneo husika unabaki ku-*stuck.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali ije na mpango wa kuhakikisha kwamba mahindi yale ambayo wakulima tuliwahamasisha walime kwa kiasi kikubwa basi yanunuliwe sasa. Hali ni ngumu kwa wananchi wetu kule na tunaulizwa maswali mengi sana na bahati mbaya zaidi sasa hivi Serikali imezuia kuuza haya mahindi kwenye maeneo mengine. Tunaweza tukasema hivyo kwa sababu kuzuia kwake hatujapewa sasa *altelnative* kama lipo soko la ndani basi soko hilo lipo wapi ili mwisho wa siku hawa watu wetu waweze kuuza mahindi yao ili tupate faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya suala la maji. Maeneo ya kusini kuna ufadhili mkubwa sana ambao wananchi au Serikali inapata kutoka kwa *donor funded.* Kwa hiyo, katika ufadhili huo kuna sehemu ambayo Serikali inatakiwa ichangie, tunajikuta sasa kuna miradi mingi, kuna *proposal* nyingi tunaziandika lakini inapofika sasa kuchangia Serikali tunakwama sana na wale wafadhili wanatupa *support* ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sasa Serikali

pindi tunapokuwa tunaleta kwenye meza zenu kwa wataalam na kwenye mamlaka husika, basi tupewe ushirikiano wa kutosha ili tuweze kutatua hili tatizo la maji kwa sababu hawa wadau wana-*support* kwa kiasi kikubwa ili mwisho wa siku matatizo na kero za maji ziweze kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia uchumi wa viwanda maana yake ni lazima twende kwenye mapinduzi makubwa ya kilimo. Sasa kitendo cha kutokununua mazao ya wakulima au kutokutafuta masoko, uwezekano ni mkubwa sana wa kuona kwamba hatutaweza kufanikiwa kwa kiasi kile ambacho tumekilenga. Hii ni kwa sababu wananchi wanakosa matumaini, wanakata tamaa na mwisho wa siku sasa *drop* inakuwa kubwa katika kuhakikisha kwamba hawa watu wanaendelea ku-*concentrate* na ile *motivation* inakuwa hamna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sasa Serikali ije na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba tunatengeneza utaratibu mzuri *(platform)* ya kuhakikisha kila ambacho kinazalishwa kinakuwa kipo *motivated* ili mwisho wa siku tuweze kuendelea na kuhamasisha hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara kandokando ya Ziwa Nyasa; kule wananchi wamejitolea kwa kiasi kikubwa kulima kwa majembe ya mkono. Kwa hiyo, pindi mara nyingi tunapoomba msaada kwamba hawa watu wasaidiwe kutokana na kero ambayo inawakuta mpaka imefikia kipindi wao wenyewe wanaamua kuchukua uamuzi tuwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru *TASAF;* tumelima barabara ya kilometa 28 lakini tunashukuru *TASAF* kwa kuweza kutu-*support* na matokeo yake sasa tunatumia zana ambazo ni mashine kwa maana ya *grader* na *excavators* ili kuhakikisha kwamba tunazipanua hizi. Vilevile katika maeneo mengine ambako wananchi wanajitolea zaidi, tunaomba mkono wa Serikali ufike kwa sababu kero hiyo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ludewa kuna Vijiji 15 ambavyo havijawahi kuona gari toka kuumbwa kwa ulimwengu. Sasa imefikia wananchi wameamua sasa kushika majembe na sululu ili waweze kupata hizo barabara. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwenye maeneo kama hayo tunapokuja kuomba msaada kwa sababu ile ni kazi ya Serikali na wananchi basi tushirikiane na wananchi hawa kuwatia moyo kuhakikisha kwamba haya malengo yanakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo nalizungumza ni lile eneo ambalo ni kando kando ya Ziwa Nyasa ambalo ni mpakani mwa Malawi na Tanzania, ni eneo muhimu kiulinzi na kiusalama. Kwa hiyo, wananchi wanapochukua hatua hizo tunaamini kwamba Serikali ije nayo ituunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuishukuru Serikali lile eneo la mwambao wa Ziwa Nyasa ambalo ni eneo kubwa kuliko eneo lingine lolote, tulikuwa hatuna mtandao wa mawasiliano ya simu; tunaishukuru Serikali sasa hivi angalau asilimia 75 ya eneo hilo sasa kuna mtandao wa simu. Nipongeze na niweze kuishukuru kwa hayo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono mapendekezo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hongoli, ajiandae Mheshimiwa Keissy.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa kupewa nafasi hii kuchangia kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019. Nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambazo anazifanya katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Niwapongeze Mawaziri kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya na wanashirikiana na Rais kuhakikisha kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa vizuri, niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa jinsi anavyosimamia shughuli nzima za mapato na matumizi kwa maana ya uchumi wa nchi hii na amekuja na hotuba nzuri ambayo inaleta matumaini kwa Watanzania, nikupongeze sana Waziri na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuiangalia sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo ndiyo sekta ambayo ni mhimili wa uchumi wa nchi yetu na sekta hii inachangia takribani nusu ya pato la Taifa letu kwa maana ya uchumi wa Taifa. Hivyo basi, Watanzania wengi ndio walipo huko, wameajiriwa huko wanafanya shughuli za kiuchumi, kwa hiyo ni lazima tuiangalie kwa namna ya pekee sana ili angalau iendelee kuchangia zaidi hata kuliko kuishia kwenye nusu pengine iende mpaka kwenye robo tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja ni kwamba katika kilimo kuna mazao ya aina mbili, kuna mazao ya chakula na mazao ya biashara. Niseme kidogo juu ya mazao ya biashara, tuna pamba, tumbaku, kahawa na mazao mengine kama chai. Mazao mengi ya biashara yanapewa ruzuku na Serikali na angalau sasa hivi tunaona mazao mengi yanapata bei nzuri, tukiangalia kwenye korosho bei ilikuwa chini lakini sasa hivi imepanda kwa sababu ya ruzuku ambayo inatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado kuna mazao mengine hatujayapa kipaumbele wakati mazazo hayo yanaweza yakatuingizia fedha nyingi sana za kigeni kama tukiamua kuwekeza huko na kuhakikisha kwamba tunawasaidia wakulima wetu waweze kuzalisha kwa wingi na kwa ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue mfano wa zao la chai, sijaona likitiliwa mkazo sana, ikumbukwe kwamba zao hili katika miaka ya 1990 kurudi nyuma ndiyo zao ambalo lilikuwa linaingiza fedha nyingi sana za kigeni. Lilikuwa ni zao ambalo ni mtetea uchumi mzuri sana lakini sasa hivi ni kama tumelitelekeza hivi bado halisimamiwi vizuri na wakulima

bado bei zao zipo chini na hakuna usimamizi mzuri kutoka kwa mkulima anavyoichuma chai kupeleka kiwandani na hatimaye kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima hajui chochote, akishauza chai yake pale kwenye banda au kwenye kituo chake anachouzia hajui chochote nini kinapatikana mwisho wa siku. Kwa hiyo, ufuatiliaji katika *chain* nzima ya ukamilishaji wa zao la chai haupo na matokeo yake bei ya chai imeendelea kuwa chini, sasa hivi inalipwa kati ya Sh.230/= mpaka Sh.250/= ukilinganisha gharama za uzalishaji wa zao hili ni kubwa kuliko kile anachokuja kukipata mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majani mabichi sasa hivi kama nilivyosema ni Sh.230/= mpaka Sh.250/=, lakini gharama za uzalishaji zinazidi Sh.450/=. Ukiangalia kwa nchi za wenzetu, ukiangalia kwa mfano Kenya, mwaka jana kwenye kilo moja ya chai ambayo tayari ni majani makavu waliweza kupata kwa kila kilo dola 266, kwa hiyo ukii-*convert* katika fedha za Kitanzania pengine ni kama Sh.5,000/= hivi na zaidi. Kwa hiyo, kumbe inawezekana tukiisimamia vizuri hii sekta, tukisimamia vizuri zao linaweza likatuletea uchumi mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba kwanza inaisimamia Bodi ile ya Chai vizuri ili bei ziweze kupanda kadri ya muda unavyozidi kwenda. Ukiwauliza wenyewe wanaozalisha chai, wale wanao-*process* chai, wanasema haina faida lakini ukiuliza nje ya nchi kule wanakouza chai wanasema wanauza kwa bei nzuri sana. Kwa hiyo, tunajiuliza sisi wakulima wa chai kuna nini pale katikati, kwa nini bei ya chai haipandi. Bei iliyopo sasa hivi kwa mara ya mwisho iliongezwa mwaka 2012, mpaka sasa hivi bado bei ni ileile. Tunasikia tu kwamba hivi karibuni Bodi ya Chai itaenda kutangaza bei elekezi, basi tuombe hiyo bei itangazwe mapema ili wakulima wajue na waweze kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tozo ilitolewa kwenye chai, tozo ya shilingi mbili; lakini wakulima hawaioni hiyo, haiendi kwa wakulima mpaka sasa hivi. Kwa hiyo

niiombe Serikali, nimwombe Waziri wa Kilimo ajaribu kusimamia ili kuhakikisha kwamba kila tozo zinavyokuwa zimeondolewa lazima zi-*reflect* wakulima tu na zionekane kwa wakulima ili waone kwamba zile tozo zina tija kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuombe sana tusimamie hili na tusaidie hili, ili wananchi hawa waweze kupata fedha hizo ambazo zinawasaidia kusomesha watoto wao, zinasaidia kujenga nyumba nzuri na zinasaidia kufanya mambo mengine makubwa na mwisho wa siku kiuchumi kama wa wakulima unakuwa, lakini uchumi kama nchi pia unaongezeka. Kwa hiyo ni lazima tuanze kusimamia haya mazao tunayofikiri ni madogo ili baadaye kwa ujumla wake ndiyo yaweze kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema viwanda, viwanda vitaongezeka kama uzalishaji utaongezeka lakini ilivyo sasa hivi kwenye zao la chai ni kama watu wanakata tamaa kwa hiyo hata viwanda havitakuwepo. Tukiongeza usimamizi katika uzalishaji wa zao la chai, naamini hata wakulima watafurahi, watazalisha kwa wingi, mashamba yataongezeka na ajira nyingi zitaongezeka kupitia mashamba na viwanda na viwanda vitaongezeka. Kwa hiyo, wazo la kufikia kwenye uchumi wa viwanda tutafika kama mazao haya ya biashara yanasimamiwa vizuri kuanzia mwanzoni mkulima anapozalisha lakini mpaka mwisho wa soko mkulima aonekane kwamba kuna faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa kunakuwa kuna malipo ya pili baada ya kuuza yale majani mabichi lakini wananchi wengi hawayapati haya. Kwa mfano, wakulima wangu wa Lupembe kule hawapati mauzo ya pili au ile fedha inayokuja baada ya kuuza majani makavu, wakilipwa tu yale majani mabichi inakuwa ni mwisho wa malipo. Kwa hiyo, niiombe Serikali, niombe Wizara isimamie vizuri jambo hili ili wakulima hawa waweze kuongeza uzalishaji na wakione kilimo kama kina tija na mwisho wa siku tutaongeza uchumi wa nchi lakini pia tutakuwa tumeongeza Pato la Taifa kupitia hili zao la chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nije kwenye upande wa kilimo cha mazao ya chakula, niseme kidogo kuhusu zao la mahindi. Kama walivyosema wenzangu kwamba zao la mahindi kwetu sisi sio zao tu la chakula bali ni zao la biashara. Kuna wananchi wanalima mahindi kwa ajili ya chakula, lakini pia kwa ajili ya kuuza kuweza kupata fedha kwa ajili ya kusomeshea watoto wao. Hivi sasa baada ya hili zuio, kama walivyosema wenzangu zuio la kuuza mahindi nje ya nchi, wakulima wetu wamebakiwa na mahindi na wengine wanauza kwa bei ndogo sana kati ya Sh.3,000/= mpaka Sh.5,000/-.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ukipiga hesabu ya gharama za uzalishaji wa zao la mahindi na bei wanayouzia mahindi kwa gunia kwa maana ya Sh.20,000/= mpaka Sh.25,000, bei hiyo inawapa hasara kubwa sana. Kwa hiyo sasa hivi wanashindwa kununua mbolea ambapo msimu wa kuanza kilimo cha mahindi ndiyo huu umeanza, sasa hivi wameshaanza kulima mashamba, mwisho wa mwezi huu wanatakiwa waanze kupanda. Hata hivyo, hawawezi kulima vizuri na kupanua kilimo chao kwa sababu hawajauza mazao yao kwa bei nzuri na hawajapata fedha za kutosha za kuweza kununulia hizi mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Wizara, mbolea imeshafika na bei imepungua tumeshaiona, lakini wakulima wetu hawawezi kununua zile mbolea kwa sababu hawana fedha za kutosha. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Serikali kwa ujumla wakae wajaribu kulitafakari hili na wajaribu kuangalia jinsi gani tutawasaidia wale wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Serikali imenunua kupitia Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* imenunua mahindi, lakini imenunua kiasi kidogo sana. Mahindi yapo mengi, sisi Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine tulihamasisha wananchi walime kiasi cha kutosha ili waweze kuuza tuki-*refer* soko la mwaka jana, kwamba mkiuza mtauza kwa bei nzuri na mtapata faida kubwa. Hata hivyo, sasa hivi ilivyo inaonekana kama sisi Waheshimiwa Wabunge na

viongozi wengine tulikuwa tunawadanganya. Hivyo, wawakilishi wa wananchi na viongozi wengine tunalaumiwa kwa sababu wananchi hawana sehemu ya kupeleka yale mahindi na kuweza kuuza ili waweze kupata fedha na kuweza kufanya mambo yao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Waziri, hebu wajaribu kuliangalia kwa jicho la pekee ili wajaribu kujadili na tuweze kuangalia jinsi gani tutaweza kuwasaidia wale wakulima wetu waweze kuuza yale mazao yao lakini wauze kwa bei nzuri. Ikiwezekana, wakifungua mipaka inakuwa rahisi kwetu kwa sababu wafanyabiashara wakubwa wanakuja na bei inapanda kwa sababu kunakuwa na ushindani wa ununuzi wa mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe sana Waziri na niiombe pia Serikali kwa ujumla wajaribu kutafakari hili na tuangalie jinsi gani tutaweza kuwasaidia wale wakulima wa mahindi waweze kuuza mazao yao ili wakishauza waweze kupata fedha za kununulia mbolea, lakini pia wapate fedha za kuweza kusomeshea watoto wao. Januari shule zinafungua wanategemea wauze hayohayo mahindi, watashindwa kupeleka watoto wao kwa sababu ya ada na michango mbalimbali ambayo inatakiwa kwenye shule kwa kule watakakokuwa wamepeleka watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme juu ya miundombinu. Kilimo au shughuli zote za maendeleo zinategemeana sana na miundombinu. Kwa hiyo miundombinu kama barabara, reli, mambo ya viwanja vya ndege na mambo mengine vikiboreshwa vizuri ndiyo vinasaidia kukua kwa uchumi. Niipongeze Serikali na nimpongeze Rais kwa jinsi ambavyo anapigania uboreshaji wa barabara, uboreshaji wa miundombinu ya reli na uboreshaji wa viwanja vya ndege, ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna baadhi ya maeneo bado uboreshaji haujafanyika sana. Kwa mfano kwenye Jimbo langu mimi la Lupembe; nishukuru kwamba barabara kwa maana ya zile za vumbi zinapitika sehemu

kubwa, lakini kuna tatizo la barabara ile ya lami ambayo ilitakiwa ijengwe. Ilikuwa ni ahadi kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015, kwamba Barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tunaitumia sana sisi wananchi wa Lupembe kwa maana ya kusafirisha mazao mbalimbali, hasa mizigo mizito kama ya mbao, kusafirisha mizigo kama ya nguzo za umeme na kusafirisha mazao ya mahindi, maharage, matunda – mananasi, maparachichi na mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii barabara ikifika wakati wa kifuku huwa inakuwa ni ngumu sana kusafirisha mizigo kama hii. Wakati wa kifuku, wakati inaisha mvua ndivyo mazao haya yanapotolewa. Kwa hiyo, niombe katika bajeti ya mwaka jana, mwaka 2016/2017 zilipitishwa bilioni nane lakini bado haikutangazwa na mwaka huu tumepitisha bilioni mbili kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami lakini bado haijatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Waziri mwenye dhamana atusaidie kutangaza barabara hii ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami ili tuweze kuhakikisha kwamba mazao yaliyopo kule kwenye maeneo yetu, kule vijijini, yaweze kusafirishwa kuweza kufikia soko. Maana yake nguzo kwa kutumia barabara za vumbi zikishapita gari ndani ya wiki moja au mbili tayari barabara zimeharibika, lakini ikiwa lami tunaamini kwamba mazao haya yatasafirishwa na uchumi wa maeneo haya utakuwa lakini mwisho wa siku, uchumi la Lupembe utachangia uchumi wa Taifa na uchumi wa nchi kwa ujumla utakua kupitia uzalishaji unaofanyika kwenye maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niseme juu ya umeme. Nnashukuru sana kwamba mpango wa umeme, hasa umeme vijijini, unaendelea vizuri kwa maana tumeshaanza kuona baadhi ya maeneo kuna nguzo zinachomekwa, lakini kwetu sisi ujenzi wa *line* bado

haujaanza. Tunashukuru kwamba kuna *line* ile ya Makambako – Songea, wameshapitisha *line* lakini bado hawajaanza kusambaza umeme kwenye vile vijiji kadiri tulivyoahidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, katika mipango ya fedha ya Serikali hii nayo tuiwekee kipaumbele ili sasa umeme huu uweze kwenda huko vijijini, vijiji vingi viwe na umeme. Tunajua kwamba umeme unachochea maendeleo, unachochea shughuli za kiuchumi nyingine kwa sababu tukiwa na umeme itakuwa rahisi kuanzisha viwanda vidogovidogo, tukiwa na umeme itakuwa rahisi hata kusukuma maji. Kwa mfano, Lupembe maji yapo chini – kusukuma maji yaweze kupandisha majumbani na kuweza kufanyia shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo umeme una manufaa makubwa sana endapo vijiji vyetu hivi vitakuwa na umeme. Namwomba Mheshimiwa Waziri, hebu tupate utaratibu mzuri, maana yake sasa hivi ni kama haieleweki vizuri ni lini umeme utaanza kusambazwa. Tukipita huko tunaulizwa na wananchi kwamba mlituahidi umeme wa *REA* lakini hatuoni hata nguzo zikisambazwa kwenye vijiji vyetu zaidi ya ile *line* ambayo imepita inayokwenda Songea. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atusaidie haya, katika mipango ijayo angalau maeneo haya ile mipango ambayo tumeipanga kwamba itatekelezwa kuanzia mwaka huu, wananchi waanze kuiona ikitekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana na naunga mkono hoja iliyopo Mezani kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Keissy, ajiandae Mheshimiwa David Silinde.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama Serikali haina makosa, Serikali inaleta pesa lakini tatizo ni kwa wafanyakazi wa Serikali. Mfano, natolea wazi kabisa miradi ya maji Wilaya ya Nkasi. Serikali inapeleka pesa, ukiuliza kule pesa zinakwenda, Namanyere zipo pesa za kutosha, cha ajabu ukimuuliza Mkurugenzi, Mhandisi wa Maji wa Mkoa, Mhandisi wa Maji wa Wilaya, TAKUKURU na kila kitu, pesa zinakuja lakini hizo pesa zinarudi Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafanya mikakati, wanawapa wazabuni ambao hawana uwezo. Mzabuni uwezo wake, *license* yake ni bilioni 750, anapewa mradi wa bilioni saba. Tumemwambia juzi mradi wa maji Namanyere, Mfiri, mradi uko chini ya kiwango, tumezuia pesa asilipwe mkandarasi kwa ushahidi kabisa, tumeleta taarifa, lakini cha ajabu amelipwa milioni 320 bila Mkurugenzi wa Namanyere kufahamu. Baada ya muda wa siku mbili tu yule msimamizi wa mradi, mfanyakazi wa Serikali, meneja wa mradi ametoa *notice* ya kustaafu kazi, inaonesha wizi wa hali ya juu, mkakati mnyororo unatoka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tu Namanyere kaenda Mkandarasi ambaye aliiba milioni 200 Namanyere na kitu chochote hakionekani, anataka kupewa tenda mradi wa maji Kirando, wanasema mpeni huo mradi kwa sababu tutamkata zile milioni 200, wakati milioni 200 hata chembe ya kazi haikuonekana. Nilizungumza hapa Bungeni kwa uchungu wa hali ya juu. Hizi pesa Serikali inakusanya kwa hali ya juu lakini bado kuna wizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Dokta Magufuli anajitahidi kukusanya pesa lakini bado wezi hawaogopi. Wakaone mfano Namanyere miradi ya maji inavyoibiwa, ni uchungu wa hali ya juu. Kodi ya wananchi inaibiwa, milioni 800, milioni 300, bilioni moja mradi wa maji Namanyere, lakini hakuna chochote kilichofanyika. Tukiulizia malipo, tunaambiwa malipo yanalipwa kutoka Wizarani moja kwa moja. Ndiyo kuna mafisadi Wizarani huko, hawana uchungu na nchi hii, wala hawaogopi kuiba katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchunguze na miradi ya gesi *Pan African* na *Songas* wanatuibia kwenye miradi ya gesi. Miradi ya gesi tunaibiwa kuliko makinikia ya dhahabu, hatuna faida na gesi, tunaibiwa. *TPDC* inakopa pesa lakini asilimia yake ndogo, sijui hawa ndugu zangu wasomi, wanasheria mikataba ikiandikwa wanakuwa wapi. Tunaibiwa mchana kweupe wala mikataba haisainiwi usiku, saa tatu asubuhi ofisi ziko wazi lakini tunaibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi tukikusanya pesa hazionekani kwa sababu mafisadi bado wapo. Hawa mafisadi tulishazungumza kila mara, hawa mafisadi ndugu zangu tuwe kama Korea, tuwe kama China, wataogopa. Wizi uko palepale, nguvu zote tunakusanya lakini wizi uko palepale; chunguza mwenyewe. *EFD machines* kila sehemu inakusanya pesa, ziko wapi? Kama mafisadi bado, mapanya wapo katika Serikali kwa nini tunaoneana huruma, tusiseme ukweli. Tuwe na uchungu, maana yake haiwezekani miradi ya hela inakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ndugu zangu siwezi kuilaumu Serikali. Hela zinakuja, zinatiririka, lakini hakuna chochote kinachoonekana. Namanyere hela zimekuja lakini hakuna maji, hakuna mabomba yanayotoa maji, wizi uko palepale. Sasa tutafika? Hatuwezi kufika. Nataka Serikali ichunguze miradi yote ya maji. TAKUKURU nilishaandika ripoti yote mpaka imefika kwa Mkuu wa TAKUKURU lakini hakuna hatua inayochukuliwa. Tunalindana ndugu zangu, tunalindana! Kuna mnyororo wa kulindana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa *REA;* Sumbawanga, miji imeongezeka, leo tumesema nchi ya viwanda. Ndugu zangu viwanda vya namna gani wakati umeme hautoshi? Leo viwanda vya kusaga tu Sumbawanga Mjini vinafungwa, vinasimama kwa sababu umeme hauna nguvu, umeme hautoshi, kiwanda kikubwa cha kusaga unga kikubwa Sumbawanga kinashindwa. Leo ndugu zangu tunasema uchumi wa viwanda, tumuinue mkulima, asilimia

75 ni wakulima, mkulima gani atalima mahindi mwaka kesho au mwaka huu wakati mahindi yameshindwa kuuzika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza lakini Waziri anatujibu kama vile yeye hana habari, hana uchungu na wakulima. Mkulima hata hawezi kununua mbolea wala hawezi kulima mwaka huu, mahindi yameshindikana kuuza. Tunazungumza kila siku mtu auze mnasema asage, apeleke unga wapi, watu wenyewe wengine wanataka kula dona, wengine wanataka kula kande, utamlazimisha mtu kula sembe? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, kwa hiyo naomba waangalieni wakulima ndio wapiga kura, asilimia 75 unasema ni wakulima, nani atalima shamba sasa? Kazi ya ajira hapati, kwenda shambani mnamnyanyasa mkulima, mbona ninyi mishahara yenu mnatumia mnavyotaka?

**MBUNGE FULANI:** Una akili!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara yenu mnanywea pombe, mnaongeza wake hakuna mtu anawauliza! Mkulima akilima hukumsaidia kupanda, hukumsaidia kupalilia, hukumsaidia kuvuna, akivuna unampa masharti ya ajabu ajabu kwa nini? Kwa nini unampa masharti mkulima wakati hukumsaidia kulima? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kazi ngumu kama kilimo, mvua isipokuja hapati kitu, mbolea unamuuzia, sasa ndugu zangu, tutafika? Ninyi aah, mnapata posho hapa mnaingia kwenye mabaa hakuna mtu anawauliza!

**MBUNGE FULANI:** Una akili wewe!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwaonee huruma wakulima wetu wauze mahindi. Hawana cha kuuza katika Mkoa wa Rukwa. Mnaona wivu akiuza mahindi ajenge nyumba ya bati, kitu cha ajabu

kabisa. Hatuwezi tukakutana na Waziri, sijui tukakutana na wanaolima mahindi, tuambizane ukweli hapa wananchi wajue kama mwaka kesho njaa itakuja kwa sababu ninyi mmeshindwa kununua mahindi na mkulima hana hela ya kununua pembejeo wala hana uwezo wa kulima. Tusianze kutafuta mchawi hapa, mchawi ni ninyi kwa sababu mmezuia kuuza mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Zambia wanauza mahindi mpaka 20,000 wanaingiza kule sehemu za Matai, Kalambo, wanauza mahindi wanavyotaka sisi tunazuia mahindi. Kulikuwa na njaa Kenya, kuna njaa tumesikia *DRC Congo,* kuna njaa Sudan, kwa nini mmeshindwa kupeleka mahindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sijakosea jana, kazungumza Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa kuhusu Rais kutoa tenda. Ndugu zangu, wapi Rais anatoa tenda? Mimi nimeshangaa, toa ushahidi. Unasema kwamba Rais anampa rafiki yake au ni kampuni yake, toa ushahidi. Naomba aliyesema jana, *Hansard* ipo atoe ushahidi. Kama Rais anahusika na kutoa tenda ya uwanja wa ndege wa Geita na kama Rais ni rafiki yake, atoe ushahidi. Sio kwenye Bunge hapa kuropoka kuhusu Rais, ni makosa ya hali ya juu. Huna ya kuzungumza kaa, weka akiba ya maneno, siyo unakuja hapa Bungeni unaropoka wewe unavyotaka kwa sababu ni Bunge, hapana. Toa ushahidi, Kamati ya Maadili ikuite utoe ushahidi, kama hukutoa ushahidi uchukuliwe hatua za kinidhamu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unazungumza kuhusu Rais, Rais ana makosa gani? Vitanda vya Muhimbili Rais hakuchukua hela kupeleka kule Dar es Salaam? Muhimbili ni Kanda ya Ziwa kule? Amejenga *flyover* Dar es Salaam ni Kanda ya Ziwa? Ndugu zangu, tuwe tunaweka akiba ya maneno, siyo unazungumza, unabwata kama uko Manzese, hapa siyo Manzese. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia ukweli, utoe ushahidi. Mimi nashangaa, Waziri anasema anaropoka

kuhusu Rais hakuna mtu alisema tukakaa kimya kama tumepumbazwa. Nashauri Mheshimiwa Waziri atoe ushahidi kamili kama Rais alihusika na tenda. Naishukuru Serikali, wananchi wangu wa Kazogo walikuwa hawaoni gari, mwaka huu wanaona gari. Tangu uhuru hawajaona gari, nimepewa hela wanaona gari, nikose kuishukuru Serikali? Barabara ya lami imekwisha toka Tunduma mpaka Kibaoni kupitia Namanyere, sitaishukuru Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ndugu zangu inafanya kazi, tatizo ni wasimamizi wanakula hela kama watu wa maji. Kuna wizi mkubwa kila Wilaya, kila Mkoa, tena wanaohusika ni Wizarani moja kwa moja. Nataka mfuatilie wala sina utani na hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, Rais siku akija Namanyere, nitawasema waondoke na wafanyakazi ambao wanakula hela katika Wilaya ya Nkasi wakiongozwa na Idara ya Maji. Haiwezekani hela inafika Namanyere inarudi Dar es Salaam wanagawana Wakandarasi. Wanawapa Wakandarasi tenda wana *briefcase,* hawana uwezo, hata tipa hana, wala mashine hana, unampa tenda ya milioni 500 au 600 kwa sababu mjomba wako au shangazi yako, hilo haliwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi/ Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Ali King ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019. Mapendekezo ya mpango ambayo tunayajadili leo hayana tofauti na mapendekezo tuliyopitisha mwaka jana, hakuna tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hauna tofauti kwa sababu *tone* yake ni ileile ya mwaka jana, ndiyo ambayo ipo katika kitabu hiki cha mwaka huu, ukikipitia chote kama kilivyo, kina *tone* inayofanana. Sasa changamoto yake ni nini? Changamoto ya mpango wote ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakwenda kwenye hoja ambazo zipo kwenye kitabu. Mimi leo najadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Serikali ya Awamu ya Tano ina sifa moja imejinasibu kama Serikali ya kubana matumizi, lakini kwenye kitabu hikihiki unarudi unakuta deni la Taifa limeongezeka toka dola milioni elfu 22 mpaka dola milioni elfu 26115.2 ambayo ni sawasawa na trilioni hamsini na tisa. Sasa wewe unasema umebana matumizi, deni limeongezeka, unawachanganya wananchi, kwa hiyo sasa ndiyo vitu tunavyokwenda kuvijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kuuliza sababu za kungezeka kwa deni ni nini Mheshimiwa Waziri amekuja sababu za kuongezeka kwa deni la Taifa ni ujenzi wa reli ya *standard gauge, SGR, Strategic Cities* mradi wa Usafirishaji *Dar es Salaam (DART),* sasa *the question* ni nini? Mheshimiwa Rais anapozunguka huko mtaani anatueleza kwamba tutajenga reli kwa fedha zetu za ndani, unakuta kwenye kitabu, kitabu kinasema tofauti kwamba tutajenga reli kwa mkopo, tuelewe nini, yaani tuelewe nini, kinachoandikwa na kinachozungumzwa ni vitu wiwili tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ni mambo lazima tukubali kuyarekebisha, yaani siasa siyo kupiga fiksi muda wote au siasa sio kutafuta kiki muda wote hamna, wakati mwingine wananchi wanahitaji kuelewa ukweli. Tuwaeleze tu ukweli, tutajenga reli kwa mkopo, tutakopa kiasi hiki zitalipwa na wananchi, unapata sifa kwa sababu wananchi wanachotaka ni miradi ya maendeleo, sasa unawaambia tutajenga, kitabu kimeandikwa na ushahidi wetu unaotumaliza ni hiki kitabu. Hilo nimelimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni matumizi ya fedha nje ya bajeti tulizozitenga. Tumekaa hapa zaidi ya

miezi mitatu tunapitisha bajeti, tunapitisha vifungu na mwisho wa siku kuna kitu kinaitwa *Appropriation Bill,* Sheria ya Matumizi ya Fedha. Ile sheria inatufunga kwamba tutumie kulingana na kile ambacho tumekipanga humu ndani. Sasa unakwenda kwenye kitabu unakuta sasa kuna miradi mipya tu kwamba miradi ya ujenzi wa bwawa wa mitambo ya kufua umeme *Stiegler's Gorge* siyo jambo baya wala sikatai, lakini unarudi Sheria ya Bajeti inataka nini? Ukiangalia kifungu cha 43 cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 inataka Serikali inapotaka kuongeza bajeti ije hapa. Ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Chato sio kosa, ni nia njema ile, lakini usipofuata sheria...

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Nasimama kwa kanuni ya 68(1), nataka nimpe taarifa mzungumzaji maana yake imezungumzwa hapa juu ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Chato, lakini katika bajeti iliyopita niwakumbushe ndugu zangu kwamba kulikuwa kuna *allocation* ya fedha kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwenye viwanja kumi na moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja hivyo kwa ruhusa yako nivitaje; tunakwenda kujenga Musoma, Moshi, Tanga, Songea, Iringa, Lindi, Njombe, Singida, *Lake* Manyara, Kilwa Masoko, Simiyu na Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na upotoshaji kwa sababu maandalizi ya ujenzi wa viwanja yanahusisha upembuzi yakinifu na kiasi kilitengwa kwa ajili ya kufanya zoezi hilo. Sasa ile gharama inayoonekana kwenye ujenzi wa uwanja wa Geita ambao utasomeka Chato, gharama hizo zinazochukuliwa hapa zinaonesha kama matumizi.

Kwa hiyo nampa taarifa mzungumzaji kwamba kiasi hicho ni kile ambacho kimesomeka kwa ajili ya gharama hizo ambazo ningeweza kuzitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa Geita zitahusu usanifu, ujenzi wa jengo la abiria, ufungaji wa mitambo ya umeme, kazi ya upande wa *airside* zinazohusisha ujenzi wa maegesho ya barabara na maungio. Sasa hizo ndio gharama ambazo zimeonekana kwenye usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba katika bajeti iliyopita tulikuwa tumetenga kiasi hicho cha fedha ambacho ni bilioni 1.912 pamoja na dola za Kimarekani 1,103 milioni. Kwa hiyo, hizo ni gharama za usanifu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Silinde.

## TAARIFA

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ni vizuri nimweleze kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, mimi sipingani na kutenga fedha ya bilioni mbili ipo kwenye bajeti. Hiyo ilikuwepo na ndio maana hakuna mtu anayejadili, lakini sisi tunachojadili ile bilioni 39, ambayo iko nje na kinyume cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunajadili. Ni mambo mema Sheria ya Bajeti kifungu cha 43(1) ya mwaka 2015 inaruhusu Serikali kuomba nyongeza ya bajeti na inawekewa mkazo na Sheria ya Fedha za Umma, kifungu namba 18(3) na cha (4) ya mwaka 2000; vyote hivyo inataka Serikali inapotaka kufanya jambo kwa mfano unataka labda kuli-*allocate* ama kuongeza jambo lingine jipya ambalo halikuwepo kwenye bajeti unaleta ndani ya Bunge. Sasa mambo mengi hapa ndani yanayofanyika sasahivi na Serikali hayajapitishwa na hili Bunge, hayajapitishwa na tumekaa humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoeleza ni nini? Leo unayafanya haya *in good* faith unasema unatumia kwa nia njema, lakini kesho atakuja Rais mwingine, Mheshimiwa Mpango utakamatwa kwa kutumia madaraka yake vibaya

huo ndio ukweli. Kwa sababu hapa Mheshimiwa Simbachawene juzi alijiuzulu kwa sababu tu aliingia mkataba wa *TANZANITE,* lakini kwenye maelezo yake alisema kabisa ametumwa juu, lakini leo amewajibika yeye. Kumbukeni watu wanaowatuma wana kinga, wao hatuwafungi, wala hatutawakamata. Kesho nakueleza ukweli sio lazima atoke Upinzani huyo Rais, atakwambia nani alikupa mamlaka ya kuidhinisha fedha za Stiegler's Gorge**,** nani alikupa mamlaka ya kupitisha fedha nanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunachotaka sisi hapa, tunataka tu Serikali ifuate utaratibu, kwani tatizo liko wapi? Ni jambo jema, ni kwa nia njema tunakutakia mema na tunakuonea huruma wewe kwa sababu baadaye mimi nitakuwa shahidi kwamba ulikuwa unakataa ushauri ndani ya Bunge na nitataka, hiyo kamati ya uchunguzi utakapokuwa unaenda ndani mimi nitakuja kutoa ushahidi kwa sababu tulishauri, kwa sababu tunayajua haya, sheria zipo na uzuri wa hii nchi ni kwamba sheria zipo, *unless otherwise,* leo Sheria ya Manunuzi iko likizo yaani iko likizo kabisa hakuna mahali inapotumika yaani mambo yanajitokeza tokeza tu huko, unashangaa tu kitu kimefanyika, baadaye *procedure* ndio zinafuata, yaani unaanza ku-*take action* halafu baadaye unafuata *procedure.* Haya yote yataundiwa Kamati ya Uchunguzi na tawala zinazokuja, miaka minane au mitatu sio mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili nataka tu nimwambie Mheshimiwa Waziri. This is *politics, politics* lazima ujue namna ya kui-*handle,* kwa sababu *politics ina repercussion,* utabaki peke yako na hakuna mtu atakayekuja kukuangalia muda huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukijadili hapa *issue* ya maji, maji ni kero kwa nchi nzima. Unapitia Mpango hapa unakuta imeandikwa sijui visima kumi na tano; Mpiji, *issue* za Halmashauri tu, hizi ni *issue* ndogondogo kabisa. Sera ya Maji inazungumzaje, sera ya maji inataka Mtanzania akichota maji mbali ni mita mia nne, lakini sasa hivi uhalisia ni upi? Wananchi wanapata shida, ukija ukisoma takwimu

za Wizara watakwambia maji mijini wanapata kwa aslimia zaidi ya themanini; maji vijijini zaidi ya asilimia sitini na tano, lakini je hali halisi maji yanapatikana? Kauli mbiu ya Serikali inasema tumtue mama ndoo kichwani, ndoo hiyo imetuliwa, tuwe wakweli, ndoo imetuliwa? Jibu unakuta kwamba haijatuliwa na kila mmoja anatafuta mahali pa kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ni mambo tunayohoji ya msingi kwa nia njema tu, tengenezeni bajeti ambayo inatekelezeka. Sasa haya yote haya ndio mambo ambayo tumekuwa tukiwaeleza humu ndani na nafikiri Waziri wa Maji aliyekuwepo anajua haya mambo, nini kimemtoa pale sasa hivi? Sasa haya yote ndiyo haya tunayoyazungumza watu wanataka maji, hawataki stori za kwenye vitabu, hizi tumeshachoka nazo. Kwa hiyo sasa hayo ni mambo yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Sekta binafsi, Serikali imeijadili kidogo sana yaani ka-*paragraph* kamoja tu, lakini ukweli Sekta binafsi imeporomoka. Mabenki yanapata hasara, mzunguko wa fedha umeshuka, mikopo chechefu imeongezeka, watu wanashindwa kulipa madeni, Serikali haijajadili mpango wa namna ya kuiwezesha Sekta binafsi ili iweze kuwa imara, inakuja na sheria, sasa hivi kila siku wanaleta sheria, sasa hivi wanaleta Sheria ya *NASACO,* yaani kila kitu unataka Serikali ifanye biashara na Serikali yenyewe. Hiyo *principle* ya wapi, duniani ilishashindwa, kama unafuata *policy ya China* hawaendi namna hiyo na namna China walivyobadilisha uchumi wao sio kwa staili tunayokwenda nayo, hii ni staili ya kutuvuruga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya yote hatutaki kuyasema lakini ni kwenye vitabu, leo unazungumza ili uchumi ukue ni lazima watu wakose hela, hiyo siyo *interpretation* sahihi. Kufanya biashara na sekta binafsi sio chanzo cha ubadhirifu wa fedha, kunatakiwa kuwe na namna ya ku-*handle* wale watu, kuna namna ya kufanya nao kazi na tueleze tu ukweli watu wanahitaji ajira wote tumekuwa

tukijadili hapa kuna tatizo kubwa sana la ajira nchini, lakini ajira sio lazima ajiriwe na Serikali; mtu hata akiajiriwa benki pale *CRDB* anasema nimeshapata ajira yangu; mtu akiajiriwa pale na Mohamed Dewj anasema mimi nimepata ajira; mtu akiajiriwa na *Coca Cola* anasema mimi nimepata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo nenda kwenye hayo Makampuni yote *Coca Cola* wamepunguza wafanyakazi, ukienda Mabenki wanapunguza wafanyakazi, lakini yote hapa bado Serikali haijaja na mpango makini wa kuhakikisha kwamba sasa tuna-*revamp* sekta binafsi iweze kusaidia kwenye uchumi wetu. Sasa haya yote tunajaribu kumwelimisha lakini anakuwa mgumu wa kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimweleze Mheshimiwa Waziri *this is politics* na ndio iko hivihivi, utakuwa hapo utaondoka, utawala uliopo uko leo, kesho utaondoka, ndiyo maisha yanavyokwenda, tusikilizane, tuelimishane ili tuweze kuelewa wapi tunapotaka kuelekea, kwa sababu tunataka uchumi imara. Sasa hizi sera mnazokuja nazo hizi na *NASACO* kila siku tunapitisha sheria mpya sisi tunawaangalia tu, zinafukuza wawekezaji, lakini haziruhusu mazingira ya watu kurudi nchini kuwekeza ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya yote ni masuala ya kiuchumi ambayo tunayakwepa kwa sababu na bahati mbaya nchi yetu tunataka nchi ya kijamaa halafu tunataka matunda ya kibepari, haiwezekani! Ni biashara ambayo haipo yaani na hicho ndicho ambacho mimi nakiona kwamba tuko wajamaa lakini tunataka matunda ya kibepari, biashara hiyo haipo.

Sasa Mheshimiwa Waziri lazima akubali na nasoma hotuba yao, tumekwenda tumefuata mpango wake kwa umakini sana na uzuri kitu kimoja tu Mheshimiwa Mpango ndiye yeye aliyeandaa mpango alikuwa Katibu Mkuu wa Mipango, makosa yote anayoyakosoa ya Serikali ya nyuma yeye ndiye aliyeyafanya. Kwa hiyo, akifitisha fito au kufanya nini ni yeye ndiye mwenye haya makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifurahia sana Mheshimiwa Rais alivyomweka Mheshimiwa Mpango pale, nikajua sasa huyu aliyetengeneza mpango sasa atausimamia vizuri. Eeh, bwana eee, kila kitu hamna kitu, biashara hakuna, yaani mambo yanafanyika chini ya *standard*. Bahati mbaya sana wanataka sifa, yaani kakitu kadogo wanataka wasifiwe, tulieni mambo yanajifanya yenyewe, tekeleza wajibu wako, watu watakupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nashukuru sana. Nafikiri elimu imemwingia, atayafanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante**.** Mheshimiwa King, jiandae Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. ALI HASSAN. OMARI KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, nashukuru sana kupata nafasi hii na la kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai tumekuwa wazima, tumekuja humu kwa pumzi ambayo ametupa yeye watu wanaongea kwa sauti kali kwa pumzi ya Mwenyezi Mungu, tunamshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mpango ambaye amekuja na mpango huu mimi naweza kusema kwamba ni madhubuti, kwa yule ambaye alikuwa hana sikio alilopewa na Mungu la kusikia hawezi kusikia, aliyekuwa hakupewa jicho la kuona hawezi kuona. Kwa hiyo, haya mengine yatazungumzwa lakini sisi Dkt. Mpango tunampongeza, mpango ni mzuri na mwaka jana tumeona jinsi ya utekelezaji wake unavyokwenda mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa *speed* anayoenda. Hii kasi hii haiwezi kuzuilika kwa vitendo vile ambavyo Wapinzani wanaweza wakafanya ni kasi ambayo wao wanajaribu kupuliza kwa maneno kwamba izimike lakini haiwezi kuzimika, haiwezi kuzimika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfano mmoja kuna kidege kidogo kilitua juu ya mgongo wa kobe, kilivyotua juu ya mgongo wa kobe kile kidege kikawa kinamwambia kobe, kobe jiandae mimi nataka kuruka sasa. Eeh, kidege wewe? Juu ya mgongo wa kobe ulipotua kobe hajawa na habari! Leo sasa hivi unataka kuruka ndio utakuwa na nguvu za kumshtua kobe? Gamba lote lile la kobe? Kwa hiyo, haya maneno yatasemwa kutaka kuzima nuru ya Serikali hii inavyokwenda, lakini tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya maneno ya kupotosha kusema *data* za uongo watu kuzungumza vitu ambavyo labda vya kupingapinga tu vinajulikana. Kuna msemo wa Kiarabu unasema *khalif tawrab,* wewe ukitaka kujulikana nenda kinyume, ukienda kinyume utajulikana, wewe ukiambiwa uchumi unakuwa kwa 7% wewe sema unakuwa kwa 4% utajulikana kwasababu utaandikwa zile 4% unazozisema wewe, lakini hata siku moja hajatokezea mke mwenza akasifu kaburi la mke mwenziwe, umeshapata kuona hiyo na yule tayari ameshakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilitokea kisa kmoja kwamba mke mwenza kapita katika kaburi la mke mwenziwe akaliona kwamba liko vizuri, alivyoliona lipo vizuri akalisifu, akaambiwa kazikwa nani hapa, aah! Alozikwa hapa ni yule mke mwenzio aaa! Kumbe kaburi baya, kaburi linanuka, hayo ni yale majibu ya maneno yenu ambayo mnaongea, mimi ninachozungumza mtoto akinyea kiganja hakikatwi, lakini tunaongeza mbele kidogo, mtoto akinyea kiganja kwanza unakosha kiganja, unamwosha na yeye na nyie ni watoto mmenyea kiganja, sasa tunakuosheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huohuo katika hotuba ya Upinzani mlizungumza kwamba katika utawala bora, mkazungumza nyie nyote, kila aliyetoa makelele humu alizungumza hivyo kwamba mkasema polisi hawajafuatilia mpaka leo kesi ile ya Mheshimiwa Tundu Lissu lakini mnajisahau, ukiwa mwongo usiwe msahaulifu kwani si ndio nyie manaotaka polisi wa Kimataifa au sio? Sio nyie

mlioambiwa mumlete dereva shahidi wa mwanzo mkasema ana msongo wa mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni sawasawa na mtu mwenye busha, mtu mwenye busha, busha linamtatiza na daktari kamwita amfanyie *operation,* yeye akakataa. Halafu akasema mmeona akasema nitafanyiwa *operation* na madaktari wa nje, halafu anasema mnaona busha hilo madaktari wenu hawajanitibu, ndio nyie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia deni la Taifa ambalo limesemwa humu sisi tunakuwa kwa 32% ya deni la Taifa, lakini ilitakiwa tuwe na asilimia zaidi 55% kwa hiyo, kiwango hicho kinakidhi tusome na ripoti za sehemu nyingine. Deni la Taifa linapimwa kwa uhimilivu wake kwa hiyo tusipotoshe watu katika masuala hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa hivi labda nizungumze kitu kimoja kuna kitu kinazungumzwa kinapotoshwa ambacho kipo katika mpango huu. Hususani kwamba kuna watu wanasema kwamba tunategemea maendeleo ya nchi hii kwa fedha za nje wakati kwamba trilioni 12.2 ndio zinatakiwa lakini trilioni 9.5 ni za ndani. Sasa wanaozungumza hivyo wanapotosha hawataki kusema ukweli, ndio hao wa kaburi la mke mwenza. Asilimia 77% ya mpango huu fedha zinatoka ndani, kwa hilo asiyejua nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie vipaumbele vya Serikali, katika vipaumbele vya Serikali cha kwanza ni viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda. Naipongeza Serikali viko viwanda vimeanzishwa na sisi wenyewe tunaona viwanda chungu mzima vinaendelea sasa hivi. Tumepita katika ziara tumeviona viwanda, watu waliokuwemo katika Kamati tofauti tofauti wamekwenda wameona hiyo tofauti, lakini bado watu wanazungumzia kwamba hakuna maendeleo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa, wanabeza juhudi hizi lakini mwenye macho haambiwi

tazama, tumeenda, tumeona. Wewe umeshaona mkia wa ng'ombe halafu unauliza ananyea wapi na wakati wewe mwenyewe umeenda ukakagua viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili natoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri; kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyotaka, hivi viwanda vyetu tunavyovitaka ni lazima vitumie malighafi inayotoka hapa nchini kwetu ili viweze kukuza ajira, viweze kuleta *multiplier effect* katika wananchi wetu. Pia kupunguza kuuza malighafi nje tukaletewa bidhaa tukauziwa kwa bei kubwa, nayo pia ni tatizo kwa hiyo sisi wenyewe tuongeze thamani, tujaribu kuongeza fursa hizo katika maeneo hayo.

Pia kuna fursa za masoko ya Tanzania sisi wenyewe tunaweza kununua pia Afrika Mashariki, *SADC, AGOA* endapo tutazalisha, hivyo, tukizalisha tutapata kitu kizuri kabisa. Kwa hiyo, naunga mkono suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao waliokuwa wanasema kwamba hili jambo la viwanda haliko vizuri kama ilivyozungumzwa katika hotuba ya Wapinzani kwamba hawa wafanyabiashara na wenye viwanda wananyanyaswa siyo kweli. Wafanyabiashara na wenye viwanda hawanyanyaswi kwa sababu kituo cha wawekezaji sasa hivi, Mkurugenzi Mkuu wa *TPSF* yumo mle ni Mjumbe na wanapanga kwa ushahidi wao wenyewe wamesema kwamba vile vikwazo vya biashara sasa hamna na vimeondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, Baraza la Biashara ambalo Rais mwenyewe ndiye Mwenyekiti katika baraza hili, wao wanakaa na wanapanga na wao wenyewe wametoa ushahidi, wafanyabiashara na wawekezaji binafsi. Llingine, Rais mwenyewe amewaita wafanyabiashara katika siku zake za mwanzo kabisa akawaeleza. Kingine ambacho kwamba maneno yenu mnayosema ni ya uongo, kila mgeni katika viongozi wa nchi za nje wanaokuja hapa wanakutanishwa na wafanyabiashara, sasa wananyanyaswa vipi hawa watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Rais kila akizindua mradi wa kiwanda Mheshimiwa Rais naye pia huwa anawapa nafasi na anatoa changamoto kwa watu wanaotaka kuanzisha viwanda na yeye yuko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo katika vipaumbele ni ujenzi wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji; kwanza hapa niipongeze Serikali, mazingira ya uwekezaji sasa hivi yanajengwa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa hizo Taasisi ambazo zipo zinafanya kazi ikiwemo Baraza la Biashara, ikiwemo Tanzania *Investment Center (TIC).* Kwa hiyo, hivi vinafanya kazi vizuri; Pili, pia kuanza kwa reli hii ya *standarg gauge* itakuza; na tatu ndege ambazo tumewekeza, ujenzi wa viwanja vya ndege na vitu vingine hivi vyote vinakuza mazingira ya biashara. Kwa hiyo hapa naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza kwa mpango wa kuja kuendeleza katika mpango huu. Wataendeleza *Stiegler's Gorge,* wataendeleza reli ya kati, viwanja vya ndege, Shirika la Ndege litaendelea kuimarishwa na mengine ambayo yanazungumzwa, kwa hiyo haya yatatengeneza mazingira ya biashara na uwekezaji. Kwa hiyo, wakati yamo humu na mwanzo yameshaendelea kufanyika katika kipindi kilichopita ina maana kwamba tunajua kwamba, haya mazingira yatakuwa. Hivyo, ukilinganisha haya mazingira ya biashara na ukuaji wa kipato chetu. Sasa naomba tulinganishe na ukuaji wa kipato chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa kipato chetu sasa hivi *per capita* ni dola 979, tumetoka hapo tumekuwa kwa 2017 kwa dola 1,025 na sisi tunataka kufikia katika lengo mwaka 2020 - 2025 kwa dola 3,000. Kwa hiyo ili tuweze kwenda *speed* kama hiyo, sekta binafsi hapa ishirikishwe na ikishirikishwa sekta binafsi tutakwenda vizuri na pia Serikali iweke mazingira katika sekta ya miundombinu. Wakiweka mazingira mazuri hayo pia yatatusaidia katika kufikia mambo ambayo tunaweza tukayafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine ni ushauri mbalimbali katika sehemu ya mapato; Mashirika ya Umma yale ambayo yanajiendesha kwa hasara tunaiomba Serikali kwanza ifanye utafiti ikihisi kwamba wanaweza wakaendelea nayo yanaweza yakageuka, sawa, lakini ikiona hayawezi kugeuka, yabinafsishwe ili yatakapobinafsishwa Serikali itakuwa inakusanya kodi na Serikali itakapofanya *study* itajua nini ifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mfumo wa tozo za *wharfage* katika Bandari; Bandari yetu inazalisha mapato zaidi ya asilimia 40, lakini mfumo wa *wharfage* unaweza ukaturudisha nyuma. Sasa mfumo wa *wharfage* urekebishwe lakini kwa kufanya utafiti. Tufuate njia ipi? Tutakapofanya utafiti tukaona njia tutakayoweza kufuata, hiyo njia inaweza ikatusaidia, inaweza ikawa ni mwarobaini katika kuzidisha mapato. Tunashukuru kwamba bandari itaongezeka na itajengwa. Tulipita Mtwara kule tumeona Bandari inaendelea, Dar es Salaam sasa hivi tumeona. Kwa hiyo, kwa mazingira ya kujenga Bandari tuweke na mazingira mengine katika mambo ya *wharfage* ili tuweze kupata kipato kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni katika urasimishaji wa sekta binafsi na urasimishaji wa biashara ndogo ndogo. Kwenye urasimishaji huu tunaomba ufanyike katika ngazi za mikoa kwa sababu utakaposema unafanya katika ngazi ya Taifa kwamba ni lazima *TRA* ndiyo awe anashughulika na suala hili kidogo itakuwa tabu na ndiyo maana sasa hivi katika huo urasimishaji imefanyika kwa Dar es Salaam peke yake, mikoani bado haijaweza kufika. Kwa hiyo zoezi hili lifanyike mpaka mikoani ili tuweze kuona ile *convenience* na *economy* ya kukusanya kodi na wale ndiyo wanaowajua, mkaa na mgonjwa ndiyo anamjua mihemo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu Tukufu ifanye haya, vinginevyo nawapongeza sana na Mwenyezi Mungu atatusogeza mbele ili jambo lingine ambalo watu wanazungumza haya maneno kwa ajili ya kupata umaarufu, tuyasikilize tu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, jiandae Mheshimiwa Rhoda.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya mimi kutoa mapendekezo yangu katika mpango wa maendeleo ya Taifa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika karne ya 17 hadi 18, Nchi ya Uingereza ilifanya mapinduzi makubwa katika kilimo. Mapinduzi haya baadaye katika karne ya 18 kwenda ya 19 ndiyo yaliyosababisha mapinduzi ya viwanda yaani *Industrial revolution.* Sasa maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, kama tunataka kwenda kwenye uchumi wa kati, uchumi wa viwanda, nashawishika kusema kwamba ni lazima tujitahidi tuwe na viwanda ambavyo vinatokana na malighafi za kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapojikita kuzungumzia viwanda hivi vya uwekezaji wa kutoka nje ambavyo havitakuwa na malighafi kutoka ndani ya nchi, bado tutakuwa hatujasaidia nchi hasa katika suala zima la ajira. Kama tutawekeza kiasi cha kutosha katika kilimo, tija itaongezeka katika uzalishaji, malighafi itapatikana na mwisho wa siku tutapata hivyo viwanda ambavyo tunavikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na kilimo kinachotupeleka huko kama tutakuwa tunaendelea kusubiri kudra ya Mwenyezi Mungu ya mvua. Ni lazima tuwe na mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na mabwawa ya umwagiliaji. Hatuwezi tukaendesha kilimo chochote ambacho ni *sustainable* kinachoeleweka ambacho viwanda vitakuwa vinasubiri malighafi kama mvua zenyewe ni hizi ambazo lazima kwanza tusubiri miezi kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nishauri kwamba katika mpango nimesoma, sikuona mahali popote panapoonesha kuhusu kuyatumia Mabonde haya nane ambayo tunayo katika nchi yetu. Kwa hiyo niombe sana

kwamba kuwe na mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba mabonde yale makubwa; Bonde la Mto Rufiji, Malagarasi, Mabonde ya Mto Ruvuma, Mabonde ya Mto Pangani na Mabonde mengine yote yanatumika vizuri kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili likifanyiwa vizuri ndilo litakalosaidia pia na vijana wengi kupata ajira kwa kujiajiri katika kilimo. Tutakapowezesha vijana kujiajiri katika kilimo maana yake tutapata malighafi ya mazao mbalimbali, hilo nalo litakuja kuchochea kwenye lile suala la viwanda kwa sababu mazao mengine yatahitaji kuchakatwa ili yaweze kudumu kwa muda mrefu, mazao mengine yatahitaji kufungashwa katika vifungashio vilivyo bora ili kuweza kupata masoko yenye tija na hapo moja kwa moja tunaongeza mnyororo wa thamani na kuongeza tija katika mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumze suala ambalo limeandikwa katika mapendekezo ya mpango ambalo ni suala la uvuvi. Katika ukurasa wa 29, uvuvi wanakusudia kuzalisha na kusambaza kwa wakulima vifanga 421,368 na katika maeneo ambayo wameyataja kujenga mabwawa hayo ya samaki 159; Mikoa ya Geita, mabwawa 23; Mkoa wa Ruvuma, mabwawa 51; Mkoa wa Mara, mabwawa 14; Mkoa wa Pwani, mabwawa 52; Mkoa wa Tanga, mabwawa mawili; Mkoa wa Dodoma, mabwawa matatu; Mkoa wa Morogoro, mabwawa matatu; Mkoa wa Tabora, mabwawa saba; Mkoa wa Dar es Salaam, mabwawa mawili na Mkoa wa Kigoma, bwawa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina wasiwasi kwamba wametumia vigezo gani lakini nataka nitoe *concern* yangu hapa. Mimi natoka Mkoa wa Tanga katika Wilaya ya Lushoto, sisi katika Wilaya ya Lushoto, Wilaya ya Korogwe, Wilaya ya Muheza, Handeni na Kilindi, Wilaya zote hizi hakuna mto ambao unaweza ukawafanya watu wakapata samaki. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa tulitaraji kwamba na sisi angalau haya mabwawa yangekuja kwa wingi angalau kufika hata

10 na lakini mabwawa mawili kwa mkoa mzima sijui hata utalipeleka upande gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hapa niliseme wazi; Mheshimiwa Naibu Waziri mwenye dhamana ya Mifugo na Uvuvi amesema hii ni *blue economy* sasa tunataka tuone unapokwenda kulitekeleza hili. Kule Lushoto kuna upungufu mkubwa wa madini chuma ambayo madini haya yanapatikana kwenye bidhaa za samaki na ndiyo maana sisi kule ukivunjika mguu, ili mguu huo uungwe unaweza ukachukua hata miezi miwili tofauti na watu walioko katika Mikoa ya Pwani ambako wanapata samaki kwa wingi, miguu inaunga haraka kwa sababu madini ya chuma yanapatikana katika samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili tunaona kwamba, upande mmoja Serikali ikilifanya vizuri inakuja kutibu tatizo ambalo linaweza likatokea siku za mbeleni. Kwa hiyo niombe sana kwenye mpango hili la mabwawa kwa Mkoa wa Tanga yaongezwe ili tupate mabwawa ya kutosha zaidi. Kama nilivyosema ni Wilaya tatu pekee, Kilindi, Tanga Mjini na Pangani ndiyo ambazo ziko pembezoni mwa bahari hizi Wilaya nyingine zote zilizobaki ziko mbali na bahari kwa hiyo tunahitaji na sisi mabwawa kwa ajili ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la miundombinu. Miundombinu ya barabara ni suala muhimu sana ili kuwezesha mazao kuweza ku-*flow* kutoka vijijini na kwenda kwenye masoko au kwenda kwenye viwanda. Hata hivyo, nataka nitoe sikitiko langu kwamba, katika mvua za masika za mwaka huu tulipata tatizo kubwa la maporomoko katika Wilaya ya Lushoto. Barabara ilijifunga kiasi cha wiki moja kwamba hakukuwa na mawasiliano katika ya Lushoto na maeneo mengine ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma katika mpango sikuona hili suala mahali popote ambapo limegusiwa kwa sababu tulishazungumza kwamba tunahitaji ile barabara iboreshwe, iongezwe upana pia tupate barabara mbadala

ya kuweza kuunganisha Lushoto na maeneo mengine. Hii inawezekana tu kama ile barabara ambayo tunaiomba kutoka Korogwe kwenda Mashewa kwenda mpaka Bumbuli itafanikiwa na barabara hii iko katika Ilani ya Chama lakini mpaka sasa bado hatujaiona katika mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika Wilaya ya Lushoto inaweza ikaunganishwa na Wilaya ya Mkinga kwenda mpaka Tanga. Kwa hiyo hili nalo ni muhimu kwamba liingizwe katika mipango ya baadaye ya Serikali, tuunganishe Wilaya ya Tanga Mjini, kuungana na Mkinga, Mkinga iunganishwe na Lushoto lakini wakati huo huo Wilaya ya Lushoto iunganishwe na Same kwa maana ya Mkoa wa Kilimanjaro ili kuweza kuunganisha mikoa hii kwa pamoja na kuweza kufikia yale malengo ambayo tutayakusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitoe rai sana kwamba kwa upande wa barabara kwa Wilaya ya Lushoto bado tunauhitaji wa barabara ya kutoka Lushoto kwenda Mlalo kwa kiwango cha lami. Kwa sasa hivi barabara hii inajengwa kilometa mbili mbili kila mkoa kiasi kwamba itachukua miaka mingi, kilometa 42 ina maana itachukua zaidi ya miaka 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi hii kwa sababu sisi ni wazalishaji wa mboga mboga na matunda na ni mazao haya ambayo ni rahisi sana kuoza, tunahitaji tupate barabara madhubuti sisi viazi hatulimi vya vuli. Tunalima viazi kwenye vitivo, tunalima viazi ambavyo vinapatikana mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo viazi, *carrot*, *spices* zote ambazo unaziona zimejaa katika *super market* na masoko makubwa nyingi sna zinatoka katika Wilaya ya Lushoto, lakini tatizo kubwa ni barabara. Barabara inatia watu umaskini kwa sababu kama barabara itakuwa siyo madhubuti ndani ya siku moja tayari mtu anaweza akapata hasara kubwa kulingana na aina ya mazao ambayo tunalima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la usambazaji umeme vijijini. Nimezungumza na watu wa *REA* wametuhakikishia kwamba wao wako vizuri, wamejipanga na Makandarasi wa kutosha wapo, tatizo kubwa ni Serikali haiachii pesa. *Disbursement* ya pesa bado siyo nzuri na hapa tunazungumza kwamba ikifika mwaka 2020/2021 mradi wa *REA* utakuwa umefika mwisho, tujione sasa kutoka sasa ni miaka mingapi imebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwamba Serikali iachie Mafungu, Mheshimiwa Mpango tafadhali sana aachie mafungu ili tuweze kukamilisha hii program ya umeme vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *program* muhimu sana kwa hili suala zima la kuleta mapinduzi ya viwanda kwa sababu tutakapokuwa na viwanda vidogo vidogo hata haya mazao ambayo tunasema kwamba ni rahisi kuoza, yataweza kuchakatwa na kuongezewa ubora yaweze kudumu kwa muda mrefu zaidi. Kwa hiyo suala la watu wa *REA* kuwezeshwa ili waweze kwenda na kasi ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa nizungumzie katika mpango ni suala zima la usafiri wa anga. Hapa inazungumzwa kwamba katika ile mikoa kumi na moja na sisi Mkoa wa Tanga upo. Niombe sana kwa Wizara husika ya Uchukuzi kwamba tunaomba sasa na sisi tuanze kuingizwa katika ratiba ya kupata ndege hizi za *ATCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu hili tumeona mapinduzi makubwa yamefanyika, sasa ni rahisi kwenda Mikoa ta Ruvuma, kwenda Mkoa wa Dodoma, Tabora, Kigoma, Bukoba na kule Songwe, lakini bado tunataka tupate *connection* kati ya Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga mpaka Mombasa. Hii ni muhimu sana na itasaidia sana kwamba kwa kuwa sisi tuko mpakani na nchi jirani ya Kenya, uwepo wa kiwanja cha ndege ambacho kinafanya kazi na ndege kutua itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tuna mradi mkubwa wa bomba la mafuta, sasa tunataraji kwamba kwa namna yoyote ile Makampuni mbalimbali ambayo yamewekeza katika ujenzi wa hili bomba watahitaji kusafiri. Sasa tusingetaraji kwamba waanze kupoteza muda mrefu wa kusafiri na mabasi kutoka Dar es Salaam kuja Tanga. Kwa hiyo, hili nawaomba sana mliingize katika taratibu zenu na sisi tuweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la ufugaji hasa huu wa ng'ombe kwamba bado kama Taifa hatujasimama mahali sahihi kuwahudumia wafugaji. Wafugaji kama bado wanaonekana kama ni wageni katika hili Taifa. Sera zetu ziko wazi lakini bado naona Wizara inapata kigugumizi pamoja na Serikali kutoa miongozo mahususi hasa kuanzia katika ngazi za Halmashauri kuainisha maeneo mahususi kwa ajili ya kulisha mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kila mtu ambapo anaenda kutafuta eneo anaonyeshwa eneo lililo wazi lakini unakuta hakuna eneo ambalo liko wazi. Maeneo haya ambayo yako wazi ndiyo maeneo ambayo wafugaji wanayatumia lakini kama leo mtu anakwenda *TIC* kuomba eneo la uwekezaji anaelekezwa kwenye Halmashauri fulani, matokeo yake ni kwamba anapewa maeneo ambayo kimsingi ni maeneo ambayo yalikuwa yanatumiwa na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba sasa kuwe na utaratibu mzuri wa kuweza kuwa-*accommodate* hawa wafugaji wetu ili tuweze kuona na wao wanatoa mchango gani kwa Taifa hili. Mimi katika Halmashauri yangu nina Kata tatu ambazo zina wafugaji. Naweza nikatoa ushahidi namna gani ambavyo wafugaji hawa wamsaidia katika pato la Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, kwanza ni wepesi sana kushiriki katika shughuli za maendeleo, lakini namna bora ya kuwawezesha ni kuwajengea malambo, kuwajengea sehemu za majosho na kuwatengea maeneo mapana

ambayo hasa wakati wa kiangazi wanaweza wakapata eneo zuri la kulisha mifugo yao. Sasa pale Serikali inaweza tu ikawa na wajibu mdogo wa kwenda kukusanya mapato na ushuru katika watu hawa. Lakini ni suala muhimu sana tunapozungumza uboreshaji wa Kiwanda cha Gereza la Kalanga kule Moshi sasa kama hakuna ngozi sijui kama watafanya kazi ya namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado pia tunahitaji kuwa na Taifa ambalo watu wanakunywa maziwa, bado Watanzania wanaokunywa maziwa ni wachache sana tena wengi wanakunywa baada ya kushauriwa na daktari. Isifike hatua kwamba hili ni Taifa ambalo watu wanakunywa maziwa baada ya kushauriwa na daktari, liwe ni Taifa ambalo lina tamaduni hizo za kuongeza vitu vyenye vitamini katika miili yao na kuweza pia kuondoa maradhi mbalimbali ambayo yatatupunguzia hata gharama za matibabu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana naomba hili alichukue kwa umakini mkubwa ili tuweze kuwasaidia wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rhoda, baada ya Mheshimiwa Rhoda jiandae Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. RHODA E. KUMCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwanza nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu pia nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Tundu Lissu huko aliko Mungu amponye kwa haraka ili arudi katika majukumu yake ya Kitaifa. Pia nitoe shukurani kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama Taifa Mheshimiwa Mbowe kwa kazi ya kujenga Taifa hili, pia namna anavyotetea na kujenga demokrasia katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia maendeleo ya uchumi wa Taifa hatuwezi kuacha kuongelea demokrasia ya nchi hii. Hatuwezi kuzungumzia uchumi wa Taifa hili bila kuzungumzia demokrasia na maendeleo katika Taifa hili, haiwezekani leo hii wafanyabiashara wakubwa,

wachumi mbalimbali wanatoa takwimu namna gani wanatoa taarifa ili Taifa hili liweze kwenda mbele, wanatoa taarifa na kuisaidia Serikali, wanatoa taarifa ambazo kimsingi zingeweza kulisogeza Taifa hili mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii watu wakipambana, wakitoa taarifa, wakikosoa Serikali, wanakwenda kupata shida na misukosuko mingi katika biashara zao na wengine wamefukuzwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa kwenye hoja za msingi. Nataka nizungumzie kidogo namna gani ya kuboresha mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato pamoja na kuzuia matumizi mabaya ya fedha katika taasisi za Umma. Tumekuwa tukipitia taarifa nyingi katika mashirika mablimbali ikiwepo *TPA* pamoja na Bandari; mifumo ya ukusanyaji wa kodi, mifumo ya namna gani wanatunza taarifa za fedha imekuwa ni kizungumkuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimwambie tu mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Ashantu Kijaji, kwamba tukishindwa kuboresha mifumo hii ya ukusanyaji wa fedha, namna gani ya kusimamia matumizi ya fedha katika taasisi hizi. Tunakwenda kupoteza fedha nyingi na leo hii tukiendelea kutoa taarifa hizi tutaonekana wabaya, tutaonekana tunaongea sana lakini lengo hasa ni kuhakikisha tunatoa taarifa ambazo zitaisaidia Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia taarifa kuhusiana na masuala ya matumizi ya *EFD* mashine. Imekuwa ni kero, unakuta mfanyabiashara wa mahindi anatoka Mkoa wa Katavi anakuja kuuza mahindi yake Dar es Salaam mpaka afike Dar es Salaam ameshakutana na vizuizi vingi, lakini upatikanaji wa hizi mashine hizi *electronic* mashine imekuwa ni mtihani. Mfanyabiashara anatoka Wilaya ya Mlela anakuja mpaka Mpanda kutafuta tu hiyo risiti ili aweze kusafirisha mzigo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri katika suala zima la kuboresha hii mifumo

ya namna gani ya ukusanyaji kodi, tuachane na mfumo wa kutumia *manually* kwa sababu watumishi wengi bila kuwasimamia vizuri unakuta tunapoteza mapato katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba tu kupitia mpango huu ambao kimsingi sijaona kwamba kuna sehemu imeandikwa kwamba mtakwenda kuhakikisha kila maeneo kila *point* ambayo itakuwa na ukusanyaji wa mapato mwongeze hizo mashine lakini kumekuwa na kero kubwa kwa hawa matrafiki. Sisi ambao tunasafiri kutoka Dar es Salaam mpaka Katavi unakutana na trafiki anakwambia umetembea *over speed*, ume-*overtake* lakini ukimwambia sasa *okay* nilipe Sh.30,000/= niendelee na safari yangu anakwambia sina mashine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini anakwandikia karatasi fekifeki tu unapita haijulikani hizo pesa zinakwenda wapi, leo tunapiga kelele watu wanakufa na njaa, watu wana shida ya maji, leo hii mngeweka mifumo hii mizuri na hizi mashine zikawepo za kutosha, pia kusimamia hii mifumo ya *EFD* kwamba kila *center* wanaposimama hawa matrafiki basi kuwe kuna hizi mashine ili kuondokana na huu udanganyifu ambao upo katika taasisi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya *procurement entity,* kumekuwa na udanganyifu mkubwa, tumekuwa tukipitia taarifa katika taasisi mbalimbali unakuta masuala ya *documentation* imekuwa ni *issue* imekuwa ni tatizo, unamuuliza *procurement officer* kwamba ni kwa nini kwenye masuala ya *procurement* masuala ya uingizaji wa bidhaa na utoaji wa bidhaa unakuta hakuna *document* ambayo inaonesha kwamba amepokea bidhaa kiasi gani na ametoa bidhaa kiasi gani, lakini unauliza unaambiwa kwamba mimi sina utaalam, tunakwenda kutengeneza Taifa gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu katika maeneo ambayo nafahamu kwamba tunapoteza vifaa vingi, tunapoteza pesa nyingi ni katika masuala ya *procurement*

*entity especially* katika ofisi zetu ambao kuna *Department* za *Procurement.* Kwa kuwa kuna shida nyingine unakuta katika taasisi katika ofisi unakuta hakuna kitengo cha *procurement* ni mtu tu hata kama ni mhasibu anaamua tu kwamba leo sasa na-*issue,* natoa, nanunua, naagiza vitu natengeneza tenda, hatuwezi kwenda hivi bila kuboresha mifumo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia watendaji wetu katika hii *procurement entity* wanatakiwa wasimamie, pia uhifadhi wa *documentation* katika hizo *strong room* wanatakiwa wapewe, ili leo tunapotaka kumwajibisha mtu tujue kabisa tunaanzia wapi. Watumishi wengi wamekuwa wanashughulikiwa wengine wanafukuzwa kazi kwa kosa hili tu, kutokuwa na *documents* za kimsingi ambazo wangeweza kuonesha na akajitetea, pia kumekuwa na shida katika masuala yaku-*handleover* ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamuuliza *Procurement Officer* katika hizi taasisi zetu unamuuliza kwamba inakuwaje umepokea *documents* za ofisi bila kuoneshwa kwenye hiyo *store* umeacha vitu gani. Unamuuliza *Procurement Officer* anakwambia kwamba mimi nimepokea tu na kukabidhiwa ofisi, haiwezekani na ukiomba taarifa ya vifaa ambavyo vinakuwepo katika *store* hizi unakuta kwamba hakuna taarifa za ukweli. Sasa leo hii tunakwenda kusimamia vifaa, mali za umma pamoja na pesa za wananchi tunakosa taarifa kupitia kwenye masuala ya *procurement,* tutaendelea kupata shida, tutaendelea kupiga kelele huku wananchi wetu wakipata shida huku wachache wakijinufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la viwanda. Mkoa wa Katavi katika bajeti iliyopita na pia katika mpango huu sijaona mkakati wa kuhakikisha mnatuongezea viwanda katika mkoa wa katavi. Hii ni tatizo, bajeti iliyopita wanatuambia kwamba tunaletewa viwanda zaidi ya nane, viwanda zaidi ya nane vitatusaidia nini Mkoa wa Katavi. Watanzania walioko kule wanahitaji viwanda zaidi ya hivi ambavyo wametupatia, kwa sababu na ukisoma kwa taarifa wanakwambia tumepewa viwanda nane na

kiwanda kimoja kina uwezo wa kuajiri watu watatu, sasa hizo ajira ndio hivyo viwanda vya matamko ambavyo mnavisema , hatuwezi kuendeleza viwanda katika nchi hii bila kuwa na takwimu za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mapinduzi ya viwanda hayawezi kwenda tofauti na upatikanaji wa maji ya kutosha pamoja na umeme. Mkoa wa Katavi tuna visima vya maji zaidi 1000, leo hii watu wa Katavi wanakosa maji safi na salama kwenye mpango huu naona tu mikoa tofauti na Katavi sijaona kwamba kuna mkakati wa kuhakikisha Katavi tunapata maji. Hivi viwanda vya miujiza mnavyovisema kwamba tunahitaji kuingia kwenye mapinduzi ya viwanda ni vipi? Kwa sababu ninavyoelewa tunaposema mapinduzi ya viwanda lazima kuwe kuna upatikanaji wa maji wa kutosha pamoja na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika masuala ya umeme wanatuletea majenereta mawili, tena majenereta mawili ambayo yamechoka. Nilitegemea kwamba kwa kuwa Serikali hii ni sikivu basi wangeongeza hata miundominu ya umeme kama masuala ya umeme wa *REA* lakini wametuletea umeme wa *REA* katika Wilaya ya Mlele, kitu ambacho hata watu wa Wilaya ya Mlele wameshindwa kulipia gharama, gharama zimekuwa kubwa lakini leo tungejikita kuhakikisha tunaweka miundominu katika mabonde yetu ambayo tuko nayo Mkoa wa Katavi leo hii tusingekuwa tunalalamika masuala ya umeme. Watu wa Mkoa wa Katavi, watu wa Wilaya ya Mpanda wanakaa wiki nzima hawapati maji, lakini bili zinakuja wananchi wanalipa, wanaletewa bili watu wana maisha magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia taarifa za *TANESCO* zimekuwa kizungumkuti. Umeme unakuja wanawasha, wanazima, watu wanaunguziwa vifaa vyao kwenye ofisi zao, hatuwezi kuendelea kulea uozo huu ambao unaendelea kwenye Mkoa wa Katavi bila kusema namna gani wanaitenga Katavi lakini namna gani wamekuwa wakitenga bajeti ambayo haijitoshelezi hususani katika masuala ya miundominu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala pia ya umeme leo wametutengea zaidi ya bilioni mbili katika mradi wa maji ambao unatoka Kanoge mpaka kuja katika hospitali ya Wilaya ya Mpanda. Ukisoma kwenye taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Mkoa wa Katavi, wanasema kwamba umefika kwenye hatua ya ulazaji wa mabomba, sasa kwa muda wote huo kweli, watu wanakosa maji, watu wanakunywa maji ya kwenye mito, wanapata hata homa za maini, wanapata *typhoid* kupitia maji machafu ambayo wanakunywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani ungefika Mkoa wa Katavi ukaona namna gani watu wa Katavi wanapata shida, lakini leo hii wamekuwa wanaitelekeza Katavi,watu wanakunywa maji machafu hawaleti pesa kwa wakati. Pia hii yote ni kutokana na kwamba wananchi wengi wamekuwa na uwoga wanashindwa kuhoji wakihofia hawa watu wasiojulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie masuala ya mikopo kwa wanafunzi. Waliahidi kwamba watatoa ajira Rais alipokuwa Moshi tarehe moja hiyo siku ya Meimosi aliahidi kwamba ataajiri watumishi wapya lakini matokeo yake wamefanya *replacement*. Watu wengi walioonewa katika masuala ya vyeti feki au mwingiliano wa vyeti mara mbili, mfano katika shule ambayo ipo katika Wilaya ya Mpanda kuna Walimu ambao walihamishwa kutoka halmashauri moja kutoka Halmashauri ya Nsimbo kuja katika Halmashauri ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa katika mfumo wakajikuta kwamba majina yao yame-*appear* mara mbili leo mpaka hivi ninavyoongea hawajapata mishahara yao, lakini Serikali imekaa kimya, tumepiga kelele za kutosha na Waziri pia nimeshamweleza kuhusiana na tatizo hili lakini leo Serikali imekaa kimya. Sasa ni halali kweli kwa watu ambao wamesoma na wana vyeti mnawasulubu na kuwapa mateso makubwa haya, huku mkimwacha Bashite akila *good time* pale Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusiana na suala la maliasili pamoja na hifadhi. Imekuwa pia ni tabia kwenye hii Serikali ya CCM kuendelea kutumia askari wa wanyamapori hususani katika Wilaya ya Mpanda, Jimbo la Mpanda vijijini Kata ya Isengule Paparamsenga, ni kwa nini Serikali hii ya CCM inashindwa kutenga maeneo au inashindwa kupima maeneo kwa wakati? Leo hii kwa kufeli kwa Serikali hii kwamba wameshindwa kupima maeneo hayo kwa wakati pia kuonesha mipaka ya hifadhi ni ipi na makazi ya wananchi ni yapi, matokeo yake wamekuwa wanawaacha wananchi wanachomewa nyumba zao, wanauliwa na askari wa wanyamapori lakini inafikia wakati mpaka wananchi wanabakwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni Serikali gani ambayo inawaagiza wananchi badala ya kwenda kuwaondoa na kuwapa elimu wananchi kuhusiana na suala la mipaka leo wanakwenda kuwabaka, wanawachomea nyumba zao ni Serikali gani hii ya CCM? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtulia, wajiandae Mheshimiwa Obama na Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia mimi pamoja na Wabunge wenzangu kuonana mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kutoa mawazo yangu kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/19. Tumeletewa mapendekezo nakumbuka Waziri Mpango ametusisitiza sanasana tumpe maoni yetu na mimi kama Mbunge tena Mbunge wa Dar es Salaama tena Kinondoni kwa wajanja, nimefurahi sana kupata nafasi hii na nitayazungumza na nayaangalia kwa kina sana mambo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo napenda tuliangalie kwa kina ni umaskini ambao naamini mapendekezo yetu au mapendekezo yangu nitakayoyatoa yanalenga namna gani tutapunguza umaskini kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mimi kama Mbunge wa mjini napata nalo tabu sana ni ukosefu wa ajira, kwa hiyo nitaeleza namna gani Serikali ikifanya tunaweza tukapunguza au kuondoa tatizo la ajira. Jambo la tatu ambalo ni lengo kuu la msingi ni kuinua au kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kitabu hiki cha Mheshimiwa Mpango, nampongeza ni mtaalam mzuri, lakini baada ya kukisoma sana tumeona mpango wetu maendeleo wa mwaka 2017/2018, tumetekeleza kwa asilimia 50 katika bajeti yetu ya maendeleo. Kwangu mimi naliona hili kama ni dosari kubwa, hivi ikiwa tunatengeneza mpango halafu tunakwenda kwenye utekelezaji, tunatekeleza kwa asilimia 50 tafsiri yake ni nini? Je, ingekuwa wataalam wengine mfano wataalam wa ujenzi Mainjinia nao wakatengeneza mpango wao halafu wakatekelezeka kwa asilimia 50 jengo litakuwepo, barabara itakuwepo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namweleza Mheshimiwa Mpango kama kuna mahali tunatakiwa tujirekebishe katika mapendekezo yangu mapendekezo haya tunayotoa mpango atakaotuletea 2018/2019 ahakikishe hatuwezi kutekeleza chini ya asilimia 80. Kupanga mpango ambao akautekeleza kwa asilimia 50 maana yake ametekeleza chini ya kiwango na kama mpango ni lengo kuleta maendeleo tusitegemee maendeleo kama yatakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ukuaji wetu wa uchumi ukiangalia hapa kuna chati ukurasa wa saba wa mapendekezo ya mpango inaonesha tulivyokuwa tuna *grow* chati inaonekana kuna kipindi tulifika mpaka 9.1; tukashuka, tukapanda mpaka 8.8 mwaka 2014; 2016 tulienda mpaka

7.7, 2017, tumeshuka; 2018 tumekwenda mpaka 7.0; mwaka 2017/2018 sasa hivi tunapanga kwenda 7.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakuwa tunakuwa au tunaongeza ukuaji wa uchumi kwa 7.1 kutoka 7.0 maana yake Mheshimiwa Mpango anatukatisha tamaa kwamba hatuendi. Sasa mapendekezo yangu ni kwamba, lazima tujitahidi tuonekane *curve* inapanda twende angalau basi turudi pale tulipotoka 2016 tuje angalau 7.7 ili ionekane uchumi wetu unakua, kinyume chake atakuwa amekubaliana na matokeo kwamba sasa tunaanza kwenda chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia umaskini kwetu sisi Dar es Salaam, tunazungumza ukosefu wa ajira kwa vijana, vijana wengi hawana ajira. Serikali ukizungumza mpango hapa wanakwambia kuna vijana 1,000 wako *VETA;* kuna vijana 2,000 wako wapi; kuna vijana 3,000 wako wapi! Hivi kwa idadi ya vijana tuliyokuwa nayo Tanzania na kwa takwimu tunazopewa za vijana 2,000, 3,000 au 4,000 tutaondoa ukosefu wa ajira kwa vijana wetu lini? Hivi kama tunashindwa Dar es Salaam kwenye idadi ya watu milioni sita tunakuwa na Chuo cha *VETA* kimoja, idadi ya watu milioni sita, Dar es Salaam una chuo cha *VETA* kimoja, huu ukosefu wa ajira tunauondoaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natamani sana Mheshimiwa Waziri akija, atuoneshe namna gani tatizo la ajira tutalipunguza kwa vijana wetu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu taarifa, ukitembelea Manispaa za mjini leo, Ilala, Kinondoni, Temeke, watendaji wetu (wataalam wetu wa biashara) wamefungua *file* la kufunga biashara...

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68 naomba nimpe

taarifa Mheshimiwa Mbunge. Naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapozungumzia masuala ya ujuzi na masuala ya ufundi katika nchi yetu ya Tanzania na mfumo ambao unatumika katika kutoa mafunzo ya ujuzi na mafunzo ya ufundi hautegemei Vyuo vya *VETA* tu. Ziko programu nyingi ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu tu, Ofisi ya Waziri Mkuu ina bilioni 15 ambazo ni za kukuza ujuzi katika nchi yetu ya Tanzania. Hata hivyo, ukiacha Vyuo vya *VETA* tuna vyuo vingine ambavyo vimesajiliwa kwa sheria ambazo tunazo katika nchi yetu ya Tanzania na vyenyewe vinatoa mafunzo ya ufundi stadi.

Kwa hiyo, naomba nimuarifu Mheshimiwa Mbunge asipotoshe kwamba hapa tumejikita tu kwenye mfumo huo mmoja wa Chuo cha *VETA.* Tunazo mamlaka, tunavyo vyuo vingi, tunazo *program* nyingi ambazo zinakuza ujuzi na ufundi katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia, taarifa hiyo ni nzuri tu.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana mtoa taarifa, dada yangu lakini taarifa yake inanipa tabu kwamba tuna programu nyingi za mafunzo ambazo hazitegemei *VETA,* tunategemea hawa vijana wanapelekwa kwa Profesa Maji Marefu? Si lazima hawa vijana wapate stadi? Namwambia Dar es Salaam tuna *VETA* moja, labda ningepewa taarifa kwamba ziko nane. Sasa hivi tuna Manispaa tano, *VETA* ziko tano, ningeichukua taarifa hiyo, lakini ananipa taarifa kwamba sehemu nyingine tusitegemee ufundi stadi peke yake, sasa tutegemee uganga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mategemeo yangu ni kwamba ajira za vijana wetu zitatokana na weledi na ufundi watakaopewa na Serikali yetu sio kwa ujanja ujanja. Nakushukuru sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la umaskini, katika jimbo langu pamoja na kwamba tuko mjini lakini wananchi wetu ni maskini sana. Umaskini huu unasababishwa wakati mwingine, Serikali haituangalii vizuri. Tuna pesa zimetengenezwa kwa ajili ya kuboresha Mji wa Dar es Salaam, tumeweka mabasi yaendayo kasi lakini tunashindwa kutenga fedha kwa ajili ya kugharamia mifereji midogo midogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mto Msimbazi na wewe unaguswa moja kwa moja, juzi imenyesha mvua ndogo tu watu wana hali mbaya, maji yanaingia majumbani, wananchi wanapata hasara, vifaa vyao vinaharibika. Tuna Mto Kibangu na Dar es Salaam imeshakwisha labda mngetuambia mnataka kutupa viwanja Dar es Salaam mtatupa Dar es Salaam gani viwanja? Dar es Salaam viwanja vimekwisha! Hivi Serikali katika kutupunguzia umaskini inashindwaje kututengenezea angalau mifereji midogo midogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Benki ya Dunia *DNDP* wametuletea mradi wa kutengeneza Mto Ng'ombe au Mto Sinza…

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia, tulia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Mtulia ambaye anasema kwamba Serikali imeshindwa hata kujenga mifereji kwenye Mji wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtaarifu kwamba mpaka sasa hivi tunavyozungumza Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira tunao mradi mkubwa na miradi mikubwa miwili iko kwenye Wilaya ya Temeke ambapo tunajenga mfereji mkubwa wa kutoka Wailes unakwenda mpaka bahari ya Hindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tunajenga mfereji mwingine pia mkubwa wa kutoka pale shule ya viziwi pale Bungoni ambapo ni Ilala kuja kwenye Mto wa Msimbazi. Kwa hiyo, asiseme kwamba Serikali haifanyi chochote. Nilikuwa naomba tu nimpe hiyo taarifa ajue kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli inafanya kazi kubwa na ana kila sababu ya kuipongeza. Ndiyo maana huwa tunashauri kwamba mtu kama huna *information or data* ndiyo sababu wataalam wanasema *you have no right to speak.* Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu nimpe hiyo taarifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Leo wote wanaonipa taarifa ni katika watu ninaowaheshimu sana, lakini kati yangu mimi na yeye sijui nani na *data.* Mimi wikiendi hii nilikwenda Dar es Salaam, kamvua ka juzi tu kale tumeenda kuokoa vyombo. Hivi ninavyozungumza kijiko kinasafisha mto tena kwa hela ya Mfuko wa Jimbo – Mto Kibangu, nazungumza Mto Msimbazi! Sasa nani hana taarifa, ni mimi niliyetoa hela ya Mfuko wa Jimbo na kukodi kijiko kwa hela ya Mfuko wa Jimbo na kukodi kijiko kwa pesa ya Mfuko wa Jimbo? Au Mheshimiwa Waziri anazungumzia Wailes wakati mimi nazungumzia Mto Msimbazi? Nani ana taarifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema nawaheshimu sana viongozi wangu hawa lakini ninachokisema, nasema kitu ambacho nimepata kwenye *field.* Nakushukuru sana na nategemea kwa sababu na wewe unahusika kwenye matatizo haya utakuwa makini sana kulinda muda wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Serikali inaondoa vipi Watanzania kwenye umaskini kwa kudharau kilimo? Hivi tunawaondoa vipi Watanzania kwenye umaskini kwa kuweka masharti yaliyopitwa na wakati kwenye kilimo? Enzi zile za zamani, enzi ambazo Tanzania hatujitoshelezi kwa chakula, enzi zile za wakulima wadogo wadogo wanaolima

kupata gunia sita, Serikali ilikuwa inahakikisha wananchi wakilima wasiuze mazao yao kwa sababu wakiuza hizo gunia sita ndani ya miezi miwili wanahemea njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo Serikali inatoa amri ya kutokuuza mahindi kwa mfanyabiashara kama Sumry aliyeacha biashara ya mabasi akaenda kuwekeza kwenye kilimo, akalima heka 1,000 akalima heka 1,500 amepata mahindi unamwambia asiuze kwa ajili ya njaa? Huyu hakulima kwa sababu ya kutaka kula, alilima kwa sababu akauze! Sasa imefika wakati Serikali tusi-*generalize,* tusitoe *order* ambazo zimepitwa na wakati. Hizi *order* zilikuwa enzi zile za watu kuhemea njaa. Leo watu wanakwenda kulima kama biashara unamzuiaje asiuze? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kaka yangu Harun pale kalima mchele wake unamwambia asiuze atakufa njaa, Harun amelima kwa sababu ya kula? Sasa lazima Serikali iwe wazi, matamko ambayo tuna *generalize* kipindi hiki wananchi wanakwenda kulima kwa ajili ya kufanya biashara, tusiwakatishe tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, hivi utaondoaje umaskini bila ku-*invest* kwenye kilimo? Kilimo ndicho ambacho kina uwezo wa kuajiri watu wetu kwa asilimia zaidi ya 70. Kilimo ndicho ambacho kinaweza kikachukua kwa sababu sisi tuna eneo kubwa, sasa leo Serikali kama tulivyojikita kwenye Shirika letu la Ndege, kama tulivyojikita kwenye miundombinu, kama tulivyojikita kwenye umeme, vile vile Serikali ioneshe nia yake ya dhati kujikita kwenye kilimo kwa sababu huko ndiko vijana wetu watakwenda kupata ajira ya kutosha. Sio kwamba watu wanakwenda kulima halafu unaleta Sheria ambazo sio sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye kilimo hivi Serikali mpaka sasa hivi inashindwa kutuambia Watanzania tulime nini? Leo Watanzania tumewaambia wakalime mbaazi, mbaazi hazina soko. Leo Watanzania wanabuni, kuna watu nimesikia wanatoka mikoa ya mbali wanakwenda Mtwara kununua maeneo kwa ajili nao walime korosho kwa

sababu baadhi ya mazao imeonekana bei haidumu, bei inayumba, sasa kwa nini Serikali isifanye utafiti, ikatuambia Watanzania limeni kitu fulani. Tusishangae baada ya Watanzania wengi kwenda kuamua kulima korosho tutaambiwa nayo korosho imeshuka bei, hili si jambo ambalo tunalitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango yeye ndiye kazi yake, ndiyo kazi yake kutuelekeza Watanzania tulime nini kitu ambacho tutapata maslahi. Leo tunaambizana tulime mbaazi kumbe hata mkataba na Wahindi hamjaingia. Leo kuna watu wanaleta habari hapa kwamba Wachina wanataka mhogo, hivi ninyi Serikali mmeshazungumza na Wachina? Mmefanya nao mikataba? Tumekubaliana? Hivi leo kwenye kilimo hatuwekezi, leo kwenye uvuvi tumeshindwa kuweka mpango wa kununua meli, tulikubaliana hapa uvuvi wa bahari kuu, hamsemi chochote kwenye bahari kuu hapa zaidi ya kutoa elimu ndogo ndogo, hatuna meli hatuna viwanda vya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo wafugaji, wafugaji hawa tunawaambia wapunguze ng'ombe wao, wanapunguzaje? Hilo soko la nyama liko wapi? Hivyo viwanda vya nyama viko wapi? Leo nyama yetu ya Tanzania inafika mahali hata kwenye migodi haikubaliki. Nyama ya Tanzania mpaka sasa hivi inakwatwa kwa shoka, hivi kweli Serikali mnafikiri umaskini huu tutauondoa kimuujiza? Umaskini huu utaondoka kwa Serikali kuhakikisha tunaangalia maeneo ambayo Watanzania wengi wapo tena wanafanya kwa gharama zao na Serikali kwenda kuwasaidia. Kama tutakuwa hatufanyi hivi, tutakuwa tunapotea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo suala la elimu tumelifanya kama biashara. Zamani enzi za mwalimu vijana wote walikuwa wanasomeshwa na Serikali, imefika mahali Serikali ikasema vijana wanasoma wengi hela hatuna tunawakopesha, unamkopesha mtu ili alipe, si lazima achague cha kusoma? Tunawasomesha chochote, hela amechukua ya mkopo, ikishakuwa hela ya mkopo maana

yake ni *business,* hivi sasa wewe umemsomesha mtu kwa hela ya mkopo halafu unamsomesha kutunga mashairi. Haya wamesoma watu 2,000 kutunga mashairi utawaajiri wapi? Unayo *industry* ya watunga mashairi wewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini sasa Serikali hatuji na sera, hatuji na maelekezo, Watanzania wanasoma kwa gharama ya kukopa ili alipe lazima aajiriwe, unamsomesha chochote, lazima tuwaelekeze Watanzania, wasome kitu gani ili wapate kuajiriwa, waweze kulipa zile pesa, lakini tunawaacha tu mtu anakuja anachagua chochote cha kusoma, akienda kwenye soko la ajira, anaambiwa hakuna ajira, halafu huyu mtu anatakiwa alipe mkopo na ndiyo maana haya mapesa...

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mtulia.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kumpa taarifa mtoa hoja kwamba masuala ya mashairi pia ni jambo muhimu kwa sababu lazima katika kusoma tuheshimu fani zote. Kwa hiyo, naomba nimpe taarifa tu kwamba mwanafunzi ana haki ya kusoma kitu chochote ambacho anaona kwamba kinamfaa na kupata mkopo ni haki yake kama amekidhi vigezo. Kwa hiyo, naomba kumpa taarifa kwamba anapochangia aheshimu fani ambazo watu wanazisoma na ni muhimu kwa Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa taarifa nzuri. Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimepata bahati, wote wanaonipa taarifa watu wangu ninaowaheshimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilichokisema; hivi wewe unasema mashairi ni fani nzuri inaheshimika, mimi siidharau lakini je wewe unaheshimu kama unavyoniambia

mie? Unawaajiri wangapi? Kwa sababu ninachosema, huyu mtu umemkopesha na ukishakopa dawa ya deni kulipa! Je, unahakikisha anachokisoma kitamwezesha kulipa? Hawa watu mtawaajri nyie Serikali hawa watunga mashairi? Kwa nini tusisomeshe madaktari ambao tunaweza kuwapeleka Zimbabwe, tunaweza tukawapeleka Malawi, kwa nini tusisomeshe Ma-*engineer* wa gesi ambao wana soko kubwa ulimwenguni, kwa nini tusisomeshe fani za kilimo ambazo zinaenda kutumika. Tunasomesha chochote! Halafu *then* akija kijana anatafuta ajira unamwambia Aah! Unajua hii fani yako hii kwenye ajira kweli haitakiwi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa umenitaja katika hotuba yako, naungana na wewe na Mheshimiwa Makamba na Mheshimiwa Lugola Mto Msimbazi umeshakuwa kazi. *TANROADS* wanafanya kazi sasa hivi na bado liko tatizo kwenye *drainage* ya *breweries* ambayo inakwenda mpaka Salender *Bridge.* Ndiyo maana kuna *club* moja kubwa pale mara nyingi inapata matatizo ya mafuriko kutokana na tatizo hilo. *(Makofi)*

Sasa nawaomba tumeshapata mwekezaji mzuri tu wa kuweza kusafisha pale na akifanya hivyo ata-*complement* na mradi wa *DART* ambao hivi karibuni umeathirika vibaya sana kutokana na mvua zile. Kwa hiyo, *TANROADS* wakimaliza huku tutahitaji ninyi mtusaidie kumaliza huu mfereji ambao unaathiri *club* yetu moja kubwa sana maeneo yale na wananchi wetu kwa ujumla ambao wanateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Obama, tutamalizia na Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia mpango wetu wa 2018/2019. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kupongeza Wizara, kumpongeza Waziri

na Naibu wake kwa kutuletea mpango ili tuweze kuuboresha. Mpango huu umekuja kama mapendekezo kwa hiyo, ni kazi yetu kuuboresha. Badala ya kuuboresha wala tusiweke majembe, tuuboreshe mpango wetu ili uweze kwenda kutekelezwa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niipongeze Serikali hii nzima kwa mafanikio ambayo wameyapata 2017/2018 ni juhudi ambazo zinatokana na michango yetu Wabunge lakini na usimamizi mkubwa wa Serikali. Kwa hiyo, niwapongeze kabisa sitaki kuingia kwa yale waliyoyaandika, yote ni mazuri tusonge mbele, twende mbele!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda tu nirudi jimboni kwangu, kwanza niishukuru Serikali. Wizara ya Uchukuzi kwa kutupandishia hadhi ya barabara zetu ambazo zilikuwa zinatuletea shida, barabara ya Buhigwe-Muyama-Katundu imepandishwa kuwa *TANROADS,* tunawashukuru sana. Pia tunawashukuru kwa kutupandishia barabara nyingine ya Mnanila mpaka Janda ambayo kwa kweli tunategemea fedha nyingi kupatikana ili tuweze kuitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwamba tunajenga hospitali yetu ya wilaya. Tunachokiomba sasa kwenye Serikali ni kutuongezea fedha. Mmetupa shilingi milioni 500, tumeanza na ujenzi, Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa wako wanajenga pale lakini sasa ile milioni 500 ni kidogo. Tunaomba mtuongezee angalau bilioni moja na nusu mkupuo ili twende na ujenzi wa hospitali yetu kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kupongeza kwamba vituo vyetu vya afya vimeendelea kuboreshwa. Tuwashukuru *World Vision* kwa kuendelea kutuchangia sana kwenye kituo chetu kile cha Muyama lakini tuishukuru Serikali nao wametupatia milioni 500 kwa ajili ya kituo chetu cha Janda. Tunaomba kwa kweli mwendelee kutu-*support* ili tuweze kuendelea na ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo la ujenzi wa Halmashauri yetu ya Wilaya, ofisi zetu za watendaji tumewapata hawa *TBA,* tumeshawalipa karibu milioni 400 lakini *speed* yao ya kutengeneza ni ndogo sana. Kwa hiyo, tunaomba kwa sababu tunapowalipa sisi kama Halmashauri fedha zinaenda Benki Kuu. Zinapokwenda Benki Kuu nafikiri wana tatizo la kurudishiwa fedha ili shirika liweze kuendelea na mradi. Kwa hiyo, tunawaomba kwa kweli muweze ku-*release* fedha ili waweze kuendelea na mradi na tunaomba mwendelee kutu-*support.* Tumewalipa pesa zote karibu bilioni moja na milioni 200 tumewalipa *cash* lakini ujenzi unasuasua. Tunaomba Wizara ya Fedha muweze kuruhusu waweze kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi ya maji. Mheshimiwa Waziri kwa bahati nzuri wewe unatokea jimbo langu, mimi ndiye Mbunge wako wa Jimbo. Kwa hiyo, ningetegemea kwamba miradi iliyoko pale na fedha ambazo mnatupa ni kidogo sana tunaomba fedha ziweze kuongezwa kwenye miradi yetu ya maji katika vijiji vyetu mbalimbali tunalo tatizo la maji sitaki kwenda mbali kwa sababu mengine tutayaongea kwa sababu ni mpango; mengine tutayaleta na mengine tutayaweka kwenye bajeti zetu za halmashauri, lakini *generally* tuna matatizo makubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma sasa hivi mnaposikia kwamba, Mpango umeandika kwamba kuleta umeme vijijini. Sisi Mkoa wa Kigoma hatujazindua mpango wa *REA III* na hatujazindua walitupa barua ya kuhudhuria uzinduzi lakini baadaye ukaahirishwa lakini kwa taarifa tulizonazo ni kwamba, kuna mgogoro uliopo kati ya *CCRB* na wakandarasi. Tunaomba Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Fedha, hebu ingilieni mgogoro huu, mkoa mzima unaadhibiwa na mradi wa vijiji haufanyiki, hatuna umeme!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Rais akisema, Wakuu wa Mikoa waangalie ujenzi wa viwanda sasa mkoa mzima hamna umeme unaoenda pale

unategemea yeye hapo afanye namna gani? Kwa hiyo, tunamwomba kabisa Mheshimiwa Waziri na ni kilio cha mkoa. Mkoa wa Kigoma ikifikia maendeleo tunataka kuendelea kuna watu wanatokea ku-*sabotage* maendeleo yetu. Sasa ifike mwisho na Mheshimiwa Waziri yuko hapo na wao ndio wanakaa kwenye Baraza la Mawaziri, hebu ashughulikie hilo, tuna uchungu nalo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tumeanzisha *TARURA*, ni jambo jema, mimi napongeza kwa sababu ubora wa barabara zetu utakuwa mzuri. Tatizo langu, kuna Sheria ya *TARURA* ambayo hairuhusu kupasua barabara mpya. Sasa ningeomba hilo nalo waliangalie. Kwenye maeneo yetu tuna barabara ambazo tunatakiwa kupasua ni mpya kwa sababu wilaya zenyewe ni mpya ili kuleta mawasiliano mazuri, lakini Sheria inawabana kwamba hawawezi kufanya namna hiyo. Kwa hiyo, tunaomba Sheria nayo ya *TARURA* ya kupasua barabara mpya iweze kuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upande wa elimu, kwenye mpango tunakokwenda sasa hivi watu wa kidato cha nne wanafaulu vizuri, kwa hiyo, watatakiwa kwenda kidato cha tano. Sioni kama Taifa kwenye mpango na kupitia kwa Waziri wa Elimu kama tuna bajeti ya kuweza sasa kujenga majengo ya kidato cha tano angalau kila kata kwa sababu sasa tumeshatoka kwenye sekondari kila kijiji sasa angalau kidato cha tano kila kata. Kwa hiyo tunategemea mpango huu uweze kuongeza bajeti ya ujenzi wa madarasa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti iliyopita *hotel levy* tuliitoa, tulisema kwamba, haitakuwepo, lakini sasa nimeona kwa Dar-es-Salaam na sehemu nyingine kuna waraka ambao unafuta ile *waive* tuliyoitoa ndani ya Bunge letu. Sasa tungependa Waziri atuambie *hotel levy* bado ipo au ameifuta? Maana upo waraka, watu wanatozwa hela, watu hatuelewi, tunaomba a seme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukumo wa viwanda nakubaliana nao na hakuna ambaye anaubishia, ila wito

wangu ni kwamba, *intelligence* ya masoko na ubora wa mazao ambayo sasa yataanza kuzalishwa ni lazima uwe makini kwa sababu, tutakuja kuwa na bidhaa ambazo watu wataanza kulia hawana mahali pa kuuza. Kwa hiyo, ni vizuri sana sasa watu wa masoko waweze kuwa macho na kuanza kujua namna ya ku-*market* bidhaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya *SIDO. SIDO* tumeipa jukumu kubwa sana la kusimamia viwanda vidogo vidogo, lakini ubora wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya *SIDO* ni mdogo. Kwa hiyo, tungependa eneo hilo Waziri wa Viwanda aweze kulisimamia vizuri ili ubora wa bidhaa zetu uweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho sijaona kwenye mpango wa Mheshimiwa Mpango kwenye kilimo, msukumo wa zao la michikichi. Sioni akiliongelea kabisa na ni zao ambalo linawafaidisha watu wa Kigoma, watu wanaokula mawese pamoja na kahawa. Kwa hiyo, ni vizuri nayo iweze ku-*reflect* kwenye mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa barabara za lami ambavyo tumeahidiwa na Mheshimiwa Rais. Kwanza tunampongeza, tunamtia moyo, nia yake ya kuufungua Mkoa wa Kigoma tunaipongeza kwelikweli. Tunamshukuru alikuja kwenye ziara, tulimpokea vizuri, kwa hiyo, tunaomba msukume maendeleo na watu wa Kigoma waweze kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii tuweze kwenda na maendeleo zaidi. Nakushukuru sana.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza kabisa niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inazoendelea kuzifanya kwa kuweza kunipandishia barabara ya halmashauri ambayo iko kwenye jimbo langu yenye urefu wa kilometa 80 na kuipeleka Serikali Kuu

*(TANROADS).* Pia, kuweza kunipandishia Kituo cha Afya Nzela na sasa kuwa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa mfano kabla sijachangia. Jamaa wawili walikuwa wanabishana mchana kweupe, saa sita. Mmoja anamwambia mwenzie hili joto lililopo linaletwa na lile jua pale juu, mwingine anasema lile sio jua ni mwezi. Sasa wakati wanabishana jua na mwezi, wamevaa vizuri na suti na tai, akapita mama mmoja wakamuuliza mama tunaomba utuamue, hili ni jua au ni mwezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mama akawaangalia wamevaa vizuri kabisa wastaarabu, akaona dawa yao ni kuwaambia jamani mimi sijui akaondoka. Wakaendelea kubishana akapita baba mwingine, walivyomwona wakasema awaamue wakamuuliza baba tusaidie, hili ni jua au ni mwezi? Saa sita mchana, akawaangalia juu mpaka chini, ni wastaarabu kabisa, akawapa jibu tu kwamba, jamani mimi hapa ni mgeni, akaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachosumbuka nacho humu ndani ni huo mfano kwamba, wanaona kabisa hili ni jua, lakini wanang'ang'ana kusema huu ni mwezi. Hata mngejitetea vipi Mheshimiwa Mpango hawawezi kukuelewa hawa, watakwambia ni mwezi na wakati ni saa sita mchana. Kwa hiyo, dawa yao wewe waambie hapa ni mgeni, ili uende vizuri na safari ya kutuletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme nchi hii ina misingi mizuri sana na sisi wenzenu tumekuwa wavumilivu toka miaka ya sabini na kitu wakati nchi hii inatengenezwa. Leo ukienda Kanda ya Kaskazini utakuta lami zinaenda kuishia kwenye migomba ambako hakuna uhitaji, sisi watu wa Kanda ya Ziwa hatukupiga kelele kwa sababu, tulijua Serikali inatengeneza maendeleo kwa awamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Kilimanjaro unakuta kuna *KIA,* ukienda Moshi Mjini kuna uwanja mdogo, ukienda Arusha kuna uwanja mdogo. Sasa hapa kumetokea

mambo watu wanapiga kelele katika Uwanja wa Ndege wa Chato. Nataka niwaambie, Mheshimiwa Waziri hizi kelele ziache waambie wewe hapa ni mgeni. Napendekeza mkimaliza kujenga ule uwanja wa mkakati wa Chato, jengeni mdogo Geita, kama ulivyo wa Moshi, ili tuwe na viwili hesabu ya kulilia uwanja ujengwe Geita iishe, kinachowauma mimi sikioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Serikali inisikilize katika viwanja ambavyo ni vya mikakati, ukiwemo na Uwanja wa Chato, Songwe na Mtwara, imarisheni. Huwezi kwenda kujenga uwanja wa ndege Iringa, kuna ndege inabeba magogo hapa? Tunatengeneza viwanja vyenye kupandisha uchumi wa nchi. Geita tuna dhahabu, tuna samaki ambao hata ndege ikitua itabeba, hakuna *Boeing* inabeba magogo kupeleka China, kwa nini tunaanza kuchambana humu ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Chato, nawashangaa sana Wabunge wa Kanda ya Ziwa, Mbunge wa Biharamulo, Mbunge wa Karagwe, Mbunge wa Kasulu, Mbunge wa Muleba, mnaacha watu wanashambulia uwanja wa Chato. Sisi tungekuwa na tamaa tungeujenga uwanja ule Geita Mjini, lakini *impact* ya uwanja ni biashara, hawa wote hamuwezi kwenda tena Bukoba mnakaa humu watu wasiojua hata ramani wanashambulia kwa ku-*google* kwenye mtandao, kwa nini msisimame mkatetea? Leo mtu wa Biharamulo utaenda Bukoba uwanja uko Chato? Mtu wa Ngara? Mtu wa Muleba? Mtu wa Kasulu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa tabia zetu Wasukuma hatuna upendeleo tunagawanaga keki na ndio maana tumeweka katikati kama mlivyoweka ninyi pale *KIA.* Kwa hiyo, nawaomba sana suala la ku-*discuss* Uwanja wa Chato acheni Mpango wa Serikali ufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Chato kilometa 30 tu kuna hifadhi pale inaitwa Rubondo, lakini tuna dhahabu pia, palepale Chato. Hata ukiangalia historia, msiofahamu, Chato, Mkoa wa Geita kila mahali kuna uhitaji muhimu;

ukienda Geita sisi eneo lote la Geita mnalolipigia kelele kuna wazungu wanachimba *under ground* sasa hivi, ukienda kwangu sisi tunavua na kulima. Sasa kama tumechagua eneo ambalo lina usalama angalao wa miaka 200 mbele mnapiga kelele bila kujua, mnataka uwanja ukawekwe kwenye mahandaki yanayochimbwa *under ground?* Acheni Mpango wa Serikali ufanye kazi, jadilini matatizo ya mikoa yenu. Hamjatumwa humu kuja kutetea uwanja wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri ameliweka vizuri kwamba, mtajenga na Moshi, mtajenga na Tanga; yote haya uwanja huu ungekuwa unajengwa Moshi wala kulikuwa hamna kelele humu, lakini niwaambie tumekuwa wavumilivu vya kutosha. Chuo Cha Madini ambacho kimejengwa na *GGM, GGM* iko Geita, kwa kuwa tu ninyi mlikuwa kwenye madaraka mka-*divert* mkapeleka chuo kikajengwa Moshi; dhahabu itengenezwe Geita mkajenge chuo chetu moshi, tumekaa kimya. Tusianze kufukua makaburi humu tunaelewa mengi sana. Tusianze kufukuliana makaburi na nawaona watu wa Kanda ya Ziwa mnasimama kubwabwaja kuhusu mambo ya Kanda ya Ziwa, mnatumika kama matela. Tutakutana 2020 labda ule mtindo wenu wa kunini na kunini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusiana na suala la mahindi. Naiomba sana Serikali ishikilie msimamo wake wa kutokuruhusu mahindi yasiende nje, mimi nakuwa tofauti na Wabunge wenzangu. Nataka niwaambie na Serikali ina *system,* hebu tumeni *system* huko kunakolalamikiwa kuna mahindi kama utakuta mahindi ya mnyonge yako pale. Tunakuwa na Bunge la kujadili mabwanyenye walanguzi, wakulima wa mahindi..

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mnisikilize nyie mmechangia mie nimekaa kimya; wakulima wa mahindi kuna mabwanyenye wanaowekesha gunia 15,000/= wakati

wanaanza kupanda, wakishamaliza kuvuna yanachukuliwa yale mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hata huko Sumbawanga kuna watu tunanunua nao mahindi 35,000/=. Yaani tunakuja na katimu ka kutetea mabwanyenye, tumeni watu mkaone mkulima mwenye magunia 150 au 30, 10 kama ana mahindi. Halafu mimi ni Mbunge wa Kanda ya Ziwa ambapo mahindi yalikuwa yanauzwa Sh.110,000/= leo tunauziwa mahindi Sh.60,000/=, nikubali mahindi yaende nje ili turudi kwenye Sh.110,000/=? Shikilia msimamo, mtu anayetaka kufanya biashara koboa unga, peleka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Keissy ametoka, wakati tunatetea ng'ombe alisema mang'ombe yauzwe, sasa yeye kwenye mahindi hatutoi mahindi, Serikali isilegeze kaza uzi. Mnaona kama mzaha, ruhusuni, fanyeni hesabu… *(Makofi)*

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Kuyaruhusu haya mahindi yaende nje, yakienda nje haya mahindi mwezi wa kwanza hili Bunge tunaanza kujadili njaa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji anayeendelea sasahivi, sisi ndio Wabunge tunaotoka maeneo hayo, tunajua hata idadi ya wakulima ambao wana mahindi zaidi ya 100, 200. Namshangaa mzungumzaji anaacha kuzungumza ajenda za maeneo ya kwake, anazungumza maeneo ambayo hayajui, sisi ndio tunatoka katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo, Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimi sana. Mimi ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania na bahati nzuri kwenye jimbo lake mimi nanunua mahindi. Hawa watu muwe mnatafuta *reference* twende ukatuoneshe, mkulima tunayemtetea humu ndani ni mkulima anayelima kwa jembe la mkono, hatuwezi kutetea walanguzi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Uende shule umjue vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kidogo suala la mazao na maliasili. Nimpongeze sana Mheshimiwa Kigwangalla ameanza vizuri, hakuna Waziri atakayepambana na wanyonge akabaki kuwa Waziri. Wanyonge wana machozi na machozi yanasikilizwa na Mungu na mifano mmeiona. Simamia uzi huohuo wa kutetea wanyonge. Kumeibuka mambo tunaomba atusaidie; watu wana miaka 10 wanaishi maeneo ya porini, halafu leo wanaibuka tu wataalam wanaenda wanachoma nyumba, tunakubali chomeni nyumba, chakula ambacho kimebakiza mwezi mmoja kivunwe wanafyeka na kuchoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Waziri asipodhibiti hili, hii ndio laana yake ya kwanza kabisa. Awaambie wawaache wananchi wetu wavune kwanza chakula ndani ya miezi miwili, halafu wawadhibiti kuingia mle ndani. Sisi kama Wabunge wawakilishi hatuwezi kuwa na wananchi ambao wana njaa. Bahati mbaya sana tumetoka kwenye njaa, Mungu ametupa neema watu wamelima, chakula kimebaki miezi miwili, mitatu *DC* anaonekana kwenye *TV* anafyeka chakula na kuchoma tena kama shujaa, halafu sisi Wabunge tumekaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri Kigwangalla tumeona aliyoyafanya Loliondo. Achunguze, hata hizi *operations...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Musukuma, kengele ya pili tayari.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza hiyo, namalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja basi, dakika moja.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kwenye dhahabu. Niliwahi kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, mzee huwezi kupambana na wafanyabiashara wadogowadogo ambao wanatorosha dhahabu yetu ambayo ni nyingi kuliko hata inayosafirishwa na migodi. Ushauri wangu, hebu aondoe ile asilimia tano ya kodi ya wachimbaji wadogowadogo, a-*deal* na watu wa migodi mikubwa ambao wao hawawezi kukwepa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wa mifukoni kuwadhibiti ni ngumu sana na yeye kwenye bajeti yake aliwahi kukusanya milioni 88 tu, hebu aruhusu dhahabu iwe *free market* kama ilivyo Dubai, kama ilivyo Uganda, watu wa Kongo, wa Zaire, wa Burundi walete dhahabu Tanzania, sisi tupate asilimia moja peke yake ya kusafirisha dhahabu, hatapambana na hao watu anaowakamata bandarini na watu watamwonesha kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshauri sana watalaam wake wakubali kuachia *free* kwenye dhahabu humu ndani liwe soko la uhuru, Waganda walete. Leo hii Uganda ni asilimia 0.5 nani atakubali kuja kulipa asilimia 6.0, si afadhali niifiche kwenye soksi, sasa atakamata wangapi kwa mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ajaribu kuangalia kama anaweza kutoa hiyo asilimia tano abakize asilimia moja tu ya kusafirisha. Hatakamatana na watu tutamletea dhahabu kama anavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu imekwisha na niwashukuru wote kwa michango. Pia niwapongeze Mheshimiwa Jenista na Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Anapochangia mchangiaji halafu mnatoa taarifa *immediately* inasaidia kuleta takwimu sahihi na inapendeza. Mnapojibu mambo haya baada ya siku tano watu wana tabia ya kuyasahau majibu yenu, wanakumbuka haya ya leo, kwa hiyo, mmefanya kazi vizuri sana, hongereni sana. *(Makofi)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi/Kicheko)*

*(Saa 1.34 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Novemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*